**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tano – Tarehe 5 Februari, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*(Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MILTON M. MAHANGA):**

Taarifa ya mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 *[The Annual Report and Audited Accounts of the National Board for Materials Management for the Year ended 30th June, 2005]*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2006.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA YA MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa Mwaka 2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 54

**Muungano wa Tanzania**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:

Kwa kuwa Muungano wa Tanzania wa mwaka 1964 umekuwa ni mfano katika Bara la Afrika:-

(a) Je, nchi za Kiafrika zina mtizamo gani kuhusu Muungano huo?

(b) Je, kuna kasoro gani katika Muungano wetu ambazo kwa namna moja au nyingine zimekuwa ni kikwazo kwa nchi nyingine za kiafrika kutojiunga na Muungano huo na hivyo kuufanya ukose nguvu?

(c) Je, Serikali ina jitihada gani za makusudi za kuukarabati Muungano huo ili uwe kigezo kwa nchi nyingine za Kiafrika kujiunga nao ili kuufanya uwe mpana zaidi kwa maslahi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa wananchi wa nchi husika?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Muungano wetu ni Muungano wenye historia ya pekee Barani Afrika na Duniani kote. Hapana shaka kuwa Muungano wetu ni moja ya misingi muhimu kwa Taifa letu na kwamba umeijengea Tanzania heshima kubwa katika Bara la Afrika na Duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, faida ya nchi zetu kuungana ni kubwa na umuhimu wa Muungano wetu umeendelea kuwa mkubwa ambapo Afrika inazungumzia kuungana na kuwa na umoja wenye nguvu ili kuweza kuleta ushindani na Mabara mengine katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, ukiwa umedumu kwa takriban miaka 43, Muungano wetu ni mhimili mkubwa wa amani na utulivu katika nchi yetu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema Muungano wetu ni mfano wa pekee katika Afrika na Duniani. Kwa hivi sasa nchi nyingi Zinazungumzia kuungana zikianzia katika kuungana kimajimbo kama *SADC,* Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC), ECOWAS,* n.k. na baadaye kuwa Muungano imara wa nchi zote za Afrika.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu unazidi kuimarika siku hadi siku na haujawahi kukosa nguvu. Aidha, si ajabu kuwepo kwa changamoto mbali mbali ambazo Serikali zetu mbili kwa kushirikiana na wadau wa Muungano zinashughulikia. Kimsingi Muungano huu unahusu watu, hivyo changamoto ni lazima ziwepo kutokana na mabadiliko na mawazo mbali mbali yanayotokana na watu walioungana.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali zetu mbili zimekuwa zikichukua hatua za makusudi kuzishughulikia changamoto za Muungano wetu. Serikali ya Awamu ya Nne imechukua hatua kuhakikisha kuwa changamoto zinazojitokeza katika Muungano huu zinashughulikiwa katika vikao vya pamoja vya ushirikiano katika sekta husika ambavyo vinafanyika mara mbili kwa mwaka. Na endapo kuna maeneo ambayo sekta husika

haziwezi kuzitatua, zinawasilishwa katika vikao vya pamoja kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi ambao wanakutana mara tatu kwa mwaka.

Lengo na madhumnuni ya jitihada hizi ni kuimarisha Muungano wetu kwa kuongeza ushirikiano katika sekta ambazo si za Muungano na kutatua kero katika sekta za Muungano. Si nia yetu kuufanya Muungano huu kuwa mpana zaidi kwa nchi nyingine kujiunga kwani hilo linafanyika katika Jumuiya za Ushirikiano kama vile *EAC, SADC* na *AU* kama nilivyosema awali.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Muungano wa Tanzania iliamua kuungana kwa Serikali mbili na kwa kuwa muundo wa Serikali hizi mbili ni wa kipekee Duniani; na kwa kuwa muundo huu umeleta matatizo mengi na kero nyingi kiasi kwamba hata baada ya miaka 43 ya Muungano hatujaweza kuyatatua yote. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba tatizo la msingi la muundo ndilo ambalo limefanya hata baadhi ya nchi zile za jirani ambazo zingependa kujiunga na Muungano wetu zimeshindwa kufanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa nini Serikali haitumii nafasi ya mjadala unaoendelea hivi sasa baina ya pande mbili za Muungano kutatua kero za Muungano, kuanzisha majadiliano ya kuifanya Tanzania iwe Shirikisho la Serikali tatu, kabla ya kwenda kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki kwa sababu ikipatikana hilo, maana yake ni kwamba kwanza sisi tutaweza kuondoa matatizo yetu ya ndani yote. Lakini la pili sisi tutakuwa mfano wa kuigwa hapo wakati Shirikisho la Afrika Mashariki litakapoundwa?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, kwamba tatizo la Muungano ni muundo wake.

Mheshimiwa Spika, Muundo tulionao wa Serikali mbili si kwamba haupo katika sehemu nyingine Duniani. Zipo aina nyingi za Muungano kama alivyosema Mheshimiwa, ipo aina moja ya Shirikisho lakini kuna aina kadhaa za Muungano. Mifano mizuri ni Uingereza, ambapo nchi ya *England* haina Bunge lake, lakini *Scotland*, *Wales* na *Northern Ireland* zina Mabunge yake. Kwa hivyo huo Muungano unaofanana na wetu. Vile vile kuna Miungano mingine kama Jumuiya ya Falme za Kiarabu n.k. Sasa sisi tuliamua kwa makusudi kuwa na Serikali mbili na kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba yapo matatizo ambayo kwa kiwango kikubwa yanashughulikiwa kwa kasi kubwa na sioni kwa nini tusiwezwe kuyatatua pamoja na kwamba tuna muundo wa Serikali mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano tu, katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja toka Serikali ya Awamu ya Nne imeingia madarakani tumeweza kutatua matatizo mengi sana ya Muungano. Suala la Uvuvi katika Bahari Kuu tumelipatia muafaka, suala la Tume ya Haki za Binadamu kufanya kazi Zanzibar limepatiwa muafaka, suala la matatizo ya ushuru kwa pande zetu mbili yamepatiwa muafaka, suala la mafuta tumekubaliana atafutwe Mshauri Mtaalam ambaye hatimaye tutapata muafaka vile vile.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu (b), kwa nini Serikali haianzishi mjadala wa kuanzisha Shirikisho la Serikali tatu; kwa kweli niseme tu kwamba hiyo siyo nia na madhumuni ya Muungano wetu. Serikali zetu mbili zinafanya kazi vizuri na matatizo kama nilivyosema yanashughulikiwa kwa kasi kubwa. Kwa hiyo, hakuna tatizo la kuendelea na muundo tulio nao.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa nchi, nataka kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wengi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa maoni ya Serikali moja, mbili au tatu, wengi walikubali mfumo wa Serikali mbili. Je, Serikali iko tayari kuheshimu uamuzi wa Serikali mbili na Serikali tatu wasiwape nafasi? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani jibu ni dhahiri na lilikwishajibiwa. *(Kicheko)*

Na. 55

**Kupeleka Umeme kwenye Mashamba ya Kilombero na Ulanga**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameagiza Mkoa wa Morogoro uingizwe kwenye Mikoa yenye kuzalisha chakula cha ziada nchini; na kwa kuwa mbinu mojawapo ya kufanikisha changamoto hiyo ni kuingia kwenye kilimo shirikishi cha mashamba kwa njia ya wawekezaji wakubwa wa ndani na nje:

Je, Serikali itakuwa tayari kupeleka umeme katika mashamba makubwa yaliyoko katika Wilaya ya Kilombero na Ulanga ili kuwavutia wawekezaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatvyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya njia ya kuzalisha umeme kujengwa ni lazima chambuzi za kifundi, kiuchumi, kifedha na athari za kijamii na kimazingira zifanyike ili kubaini ubora wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaangalia uwezekano wa kupeleka umeme kwenye mashamba makubwa iwapo wenye mashamba watawekeza kwenye mashamba hayo. Tunashauri wamiliki wa mashamba katika Wilaya hizo wajitokeze kwanza na kubainisha mipango yao Serikalini na *TANESCO* ili kuruhusu upembuzi yakinifu kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki ambacho Serikali kupitia *TANESCO* haijapokea maombi kutoka kwa wenye mashamba, ni vigumu kupeleka mtandao wa

umeme. Wakati huo huo tumewaagiza *TANESCO* wawasiliane na wahusika ili kufahamu mipango iliyoko.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza: Kwa kuzingatia azma ya Mheshimiwa Rais kwamba Mkoa wa Morogoro uingie kwenye Mikoa inayozalisha chakula kwa wingi, Vijiji viko vingi vinavyozunguka mashamba hayo makubwa ninayoyaongelea, Sasa, siyo lazima mashamba yalete maombi, ninachoomba tu ni kwamba Wizara ifikirie kuwapa vijiji hivyo vinavyozunguka mashamba hayo kuanzia Ngalimila, Chita, Chonde, Mbingu, Kisegese na Mawala mpaka Idete ambayo mashamba hayo makubwa ninayoyaongelea ambayo tunaweza kutafuta wawekezaji yapo. Ninachoomba ni ahadi kwamba kama Wizara inaweza kutusaidia kutupatia umeme katika kipindi 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa vile Wilaya yangu ndiyo inayozalisha umeme katika migodi miwili ya Kidatu na Kihansi – hili siyo swali, ni ombi kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri namuomba aje tutembelee Wilaya hiyo nimwonyeshe…

**SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali tu!

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, swali ni kwamba Je, atakubali Mheshimiwa Waziri mwaliko wa kuja kwenye Wilaya yangu ili atembelee maeneo hayo ninayoyazungumza ayaone kwa macho?

**SPIKA:** Ahsante sana! Sasa umetimiza Kanuni inavyohitaji. Kipindi hiki ni cha maswali, siyo cha maombi!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza nimkaribishe lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo anawashughulikia wananchi wake. Lakini pia niseme tu kwamba atakapokuwa ofisini tutajadili mambo mengi ikiwepo mambo ya kuelekezana kwa ajili ya jinsi gani tunaweza kuona kufanikisha mradi wa huduma ya umeme kwa vijiji ambavyo amevitaja pamoja na kufikia mashamba ambayo tunaweza kupata wawekezaji mbele ye safari.

Mheshimiwa Spika, la pili, nakubali kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kwamba nitatembelea maeneo hayo na niwapongeze tu wananchi wa Kilombero kwa wema wao ambao wanauonyesha kupitia kwa Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Kwanza, nianze na kumpongeza mwenzangu kwa kupata nafasi hiyo ya Naibu Waziri kutoka Mkoa wangu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi, amesema kwamba wanaohitaji umeme ni vema watume maombi kwanza Wizarani ili waweze kufanya upembuzi yakinifu na kutoa msaada huo. Kuna maeneo kama

Rwamgasa, Katoro, Bukoli ambako kuna wachimbaji wadogo wadogo na maombi yao wameishaleta muda mrefu sana na nadhani na *TANESCO* wameishapita. Je, Mheshimiwa, tunapenda kuelewa, utekelezaji wake umefikia wapi, kwa sababu maombi yameishafika?

**SPIKA:** Kabla hujajibu, ningemwomba Sajenti atusaidie, nimesikia Mzee wetu George Kahama yumo humu na amekaa mahali pasipomstahili, alistahili kukaa kwenye *Speaker's Gallery* na wageni wake. Kwa hiyo Sajenti ushughulikie hilo. Mzee George upo sijui? Oh! Ahsante, Mzee George kwa unyenyekevu mkubwa! Mnatupa mifano ya namna ya kushi vizuri kama wanasiasa**.** *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kwamba kuna maombi mengi ambayo yameishaletwa, lakini naomba niendelee kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali kupitia Taasisi *TANESCO* na Taasisi zingine tunaendelea kuhakikisha kwamba huduma ya umeme inafikia watumiaji wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba kwa mara nyingine tena niliombe Bunge hili Tukufu na wananchi kwa ujumla wawe wavumilivu kwa sababu *TANESCO* tunakabiliwa pia na upungufu wa vifaa, ni tatizo la kiuchumi. Lakini nia ya dhati ipo ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma ya umeme inafikia maeneo mengi. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri; na kwa kuwa tatizo la umeme la huko Kilombero linafanana sana na tatizo la umeme lililoko katika Jimbo la Bukombe; na kwa kuwa katika bajeti hii tunayoendelea nayo, tulipitisha 5.7 *billion* za kupeleka umeme Wilaya ya Bukombe na sasa ni zaidi ya nusu mwaka, sijaona hata gari ya *TANESCO* linakuja kule. Je, Serikali inaweza ikawahakikishia wananchi kwamba ndani ya bajeti hii umeme utafika Bukombe na Makao Makuu ya Wilaya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mipango ipo ya kutekeleza miradi ambayo fedha zilitengwa kwenye bajeti ya fedha. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema kwenye swali la nyongeza lililopita lililoulizwa na Mheshimiwa Kabuzi, tutaendelea kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezeka ndani ya kipindi ambacho kimepangwa ambacho ni kipindi hiki cha bajeti ambacho kinaendelea. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira lakini tunahakikisha kwamba tutatekeleza mradi huo kwa sababu pesa tayari tumeishatenga. *(Makofi)*

Na. 56

**Ukosefu wa Umeme Kharumwa**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni Sera ya Serikali ya Awamu ya Nne kupeleka umeme Vijijini; na kwa kuwa, Kijiji cha Kharumwa Jimboni Nyang'hwale kina wafanyabiashara wengi, Kituo kikubwa cha Afya, Mnara wa Simu *(CELTEL)*, Shule ya Sekondari, Shule mbili za Msingi, Kituo kidogo cha Walimu *(TRC)*, Kituo cha Polisi na Mahakama ambapo wote hao wanahitaji umeme wa *TANESCO*; na kwa kuwa, tayari kuna nyumba zaidi ya 100 zinazopata umeme wa jenereta ya mfanyabiashara mmoja; na kwa kuwa, mwaka 2001 umeme wa *grid* ya Taifa kutoka Ibadakuli (Shinyanga) kwenda mgodi wa Bulyanhulu *(KMCL)* ulipita Kharumwa na pia mradi wa umeme kutoka *KMCL* kwenda kwenye Mradi wa kupeleka maji Shinyanga na Kahama kutoka Ziwa Victoria ulipita Kharumwa na kukifanya kijiji hicho kiwe katikati ya alama "V":-

Je, Serikali inatoa majibu gani juu ya kilio cha wananchi wa Kharumwa kuhusu kupatiwa umeme wa *TANESCO* ikiwa ni pamoja na wananchi wa vijiji vya Ikangala, Kitonga, Kakora, Nyamtukuza na Parokia ya Nyarubele ambapo umeme unapitia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa James P. Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kusambaza umeme kwa wananchi wengi zaidi ili kuongeza kasi ya maendeleo kwa kutumia nishati hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kharumwa, kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge, kipo pembezoni mwa njia ya umeme inayotoka Ibadakuli kwenda Bulyanhulu. Mipango ya awali wakati njia ya umeme wa kilovoti 220 inajengwa ilikuwa ni kujenga kituo cha kupozea umeme kwa ajili ya kupeleka umeme Kharumwa, Geita na vijiji vya jirani. Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa fedha, mipango hiyo haikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Wizara ya Maji iliwasiliana na *TANESCO* kuona uwezekano wa mitambo ya maji ya Ihelele kupatiwa umeme kutoka kituo cha Bulyanhulu kwa kujenga njia ya umeme wa kilovoti 33 ambayo itapita katika Kijiji cha Kharumwa mpaka Nyamtukuza ambapo waya wa umeme utawekwa chini ya maji kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye mitambo ya maji ya Ihelele.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa James P. Musalika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme wa kilovoti 33 utapita katika Kijiji cha Kharumwa, Serikali itatafuta fedha zinazohitajika kusambaza umeme katika kijiji hicho na vijiji vya jirani. *TANESCO* wameagizwa wapeleke wataalamu kwenye vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge na kufanya upembuzi yakinifu ili kuona namna bora ya kutekeleza mradi na kupata makisio ya gharama za mradi. Upembuzi yakinifu ukikamilika hatua itakayofuata ni kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kwenye vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Karumwa kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge, kipo pembezoni mwa njia ya umeme inayotoka Ibadakuli kwenda Bulyanhulu. Napenda nisisitize tu kwamba mradi utatekelezeka kwa kipindi ambacho tumeahidi na kwa sababu mipango imeishafanyika taratibu zinaendelea. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza swali la nyongeza, napenda kwanza nichukue nafasi kwa namna ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Ngeleja kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii. Yeye ni jirani yangu, Jimbo la Sengerema na Nyang'hwale ni majimbo jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza kwa majibu yake mazuri sana na bila shaka wananchi wa Nyang'hwale, wa Karumwa wanasikia. Lakini hapa ningependa nimwulize. Je, kwa kuwa kuna mipango ya kutafuta hela, Serikali inaweza kuhakikisha kwamba mipango hii isichukue muda mrefu mpaka 2008, 2009, 2010! Waziri atahakikisha kwamba mipango hii itakamilika mwaka wa fedha ujao?

Kwa kuwa kabla hajateuliwa kuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ngeleja na yeye alikuwa na maswali yanayohusu Wizara hii, ataniruhusu sasa hayo maswali niyaulize mimi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza; naomba nimwahidi kwamba utekelezaji wa mipango hiyo tutaufanya hivi karibuni na kama alivyoomba kwamba Je, Serikali iko tayari kufikia mwaka wa fedha ujao kuona kwamba mipango hii inatekelezeka. Mheshinmiwa Spika, namwahidi yeye Mheshimiwa Mbunge na Wizara yetu tuwe karibu kumweleza matarajio ya utekelezaji wa mpango.

Mheshimiwa Spika, la pili, ninamruhusu Mheshimiwa James P. Musalika aulize maswalia ambayo vinginevyo ningeyauliza kabla sijapata nafasi hii. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize kama ifuatavyo:-

Serikali imekiri kwamba ina nia ya kupeleka umeme vijijini. Nia ipo na fedha ni kidogo. Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na tatizo la kuacha nguzo nyingi, mfano pale Kwimba Mjini za kupeleka umeme Jimbo la Sumve.

Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri anihakikishie nguzo hizo zitoke ili wananchi waone Serikali yao inawajali?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kutekeleza mipango yake ambayo imeweka kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizopo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge hili Tukufu kwamba tutahakikisha kwamba nguzo zinafanyiwa kazi ili kutimiza lengo ambalo lilikuwa limedhamiriwa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Bajeti ya Wizara hii ambayo tunaimalizia mwezi Juni, Waziri aliweka mpango kabambe wa kupeleka umeme vijijini *(Rural Electrification).* Lakini sasa hivi ni zaidi ya nusu ya Bajeti, bado mpango huu haujaanza mahali popote katika nchi nzima. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa ucheleweshaji wa uanzishwaji wa mpango huu kabambe ambao wananchi wote nchi nzima wanausubiri kwa hamu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mipango ya utekelezaji wa mradi wa usambaji umeme vijijini unaendelea.

Mheshimiwa Spika, ambacho nasema tu na kuliarifu Bunge hili Tukufu ni kwamba sasa hivi mchakato wa kumpata Mtendaji Mkuu wa Mfuko huo unaendelea.

Wataalam walishapatikana na sasa hivi wanaendelea kufanya usaili wa kumpata Mtendaji Mkuu. Akishapatikana Mtendaji Mkuu kwa sababu Bodi tayari ilishaundwa, basi Mtendaji Mkuu kwa kushirikiana na Bodi wataanza mchakato wa kuwapata watumishi au wafanyakazi katika Mfuko huo ili utekelezaji wa mradi huo uanze.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge hili Tukufu kwamba utekelezaji wa mradi unadhamiriwa kutekelezwa kama ambavyo imepangwa. *(Makofi)*

Na. 57

**Maeneo Yaliyotengwa kwa Wachimbaji Wadogo**

**MHE. CHACHA Z. WANGWE** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya uchimbaji madini imebainisha maeneo yaliyotengwa kwa wachimbaji wadogo wadogo eneo la *North Mara Mine* hapo tarehe 14 Juni, 1996 ambayo hayaingiliwi na mtu yeyote; na kwa kuwa tarehe 30 Agosti, 1996 Kampuni ya *East Africa Gold Mine* ilipewa leseni ya utafiti ambayo imeonyesha kuwa maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo hayakuguswa na leseni hiyo lakini Kampuni hiyo ilipobadilisha jina na kuwa Afrika Mashariki *Goldmine Limited* na kupata leseni ya uchimbaji iliingia kwenye maeneo hayo ya wachimbaji wadogo wadogo chini ya hakimiliki ya vijiji saba vilivyozunguka eneo hilo na kuanza uchimbaji.

(a) Je, ni sahihi kutamka kwamba, kuingia kwa *AMGM* katika maeneo hayo ni kinyume cha Sheria?

(b) Je, Serikali itawarejeshea lini wachimbaji wadogo wadogo maeneo yao hayo ili waendelee na shughuli za uchimbaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si sahihi kutamka kuwa kuingia kwa kampuni ya Afrika Mashariki *Goldmine Limited (AMGM)* kwenye eneo la *North* Mara ni kinyume cha Sheria. Utafutaji na uchimbaji wa madini kwa Kampuni kubwa na kwa wachimbaji wadogo hufanyika kwa kupata leseni zinazowaruhusu kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo walipewa leseni za kuchimba madini eneo la *North* Mara mwaka 1995. Mwaka 1996 wachimbaji hao waliingia mikataba miwili na Kampuni ya Afrika Mashariki *Gold Mine Limited* iliyoruhusu Kampuni hiyo kufanya utafutaji wa madini ya dhahabu katika maeneo yao kwa kutumia teknolojia na vifaa vya kisasa. Sheria ya Madini haikatazi mchimbaji mdogo kumweka mkandarasi wa kigeni kufanya utafutaji wa madini katika maeneo yake ya uchimbaji.

Makubaliano baina ya kampuni hiyo na wachimbaji wadogo yalikuwa kwamba, iwapo matokeo ya utafutaji madini katika maeneo yao yataonyesha kuwapo kwa kiasi cha madini ambayo yanaweza kuchimbwa kwa faida katika maeneo hayo, wachimbaji wadogo hao wataingia mikataba ya uchimbaji wa dhahabu na kampuni ili kuiachia kampuni hiyo kuendelea na uchimbaji.

Mkataba kati ya wachimbaji wadogo na kampuni ya Afrika Mashariki *Gold Mined Limited* ni kuwa wananchi waliokuwa na leseni za madini na vijiji ambavyo viko ndani ya mgodi huo watapata asilimia moja (1) ya dhahabu itakayozalishwa katika maeneo yao.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kuwarejeshea wachimbaji wadogo maeneo yao ya uchimbaji kwa vile wachimbaji hao kwa hiari yao wenyewe waliingia mkataba na kampuni ya Afrika Mashariki *Gold Mine Limited* na kuiruhusu kampuni hiyo kuendesha shughuli za uchimbaji katika maeneo waliyokuwa wanayamiliki kisheria na wao kupata mgao wa asilimia moja (1) ya dhahabu itakayozalishwa.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatambua ya kwamba wachimbaji wenyeji ndiyo wanaogundua migodi mingi hapa Tanzania ikiwa ni pamoja na wachimbaji walioko Mkoa wa Mara. Lakini mara wanapogundua maeneo hayo yanachukuliwa na makampuni makubwa:

Je, Serikali ina mpango gani kulingana na ahadi ya Rais kwamba itawatafutia maeneo mengine ambayo wanaweza wakaendelea kuchimba na kuendeleza uchumi wa nchi kwa njia hiyo, ni lini na ni mkakati gani uliopo wa kuwapatia maeneo hayo ili wasiranderande nchi nzima wakigundua maeneo na kunyang'anywa? (*Makofi*)

**NAIBU WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza sana kwamba si kweli kwamba kila inapotokea wachimbaji wanapopata mahali ambapo kuna madini wananyang'anywa na wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba wachimbaji wakubwa na wadogo wote wanaongozwa na sheria za nchi. Katika hilo wana hiari ya kuingia mikataba na wachimbaji wakubwa.

Lakini niongezee kwamba ni nia ya dhati ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wakiwemo wachimbaji wadogo wananufaika zaidi kuliko pengine ilivyo sasa. Mikakati hiyo ipo na mipango ipo na mmojawapo ni kama vile ambavyo iliwasilishwa na Wizara yangu wakati wa Bajeti ya mwaka huu wa fedha mwaka 2006/2007 kwamba tunafanya kuzipitia upya sera na sheria za madini kubaini maeneo ambayo yana upungufu ili tuweze kuyaboresha zaidi lakini hiyo ni kuhakikisha kwamba Watanzania wakiwemo wachimbaji wadogo tunanufaika.

Lakini pia, wawekezaji waliopo hapa ambao tunashirikiana nao kama nchi tunaendelea kunufaika kwa viwango kwa mujibu wa sheria na Kanuni ambazo zinaongoza.

Lakini jingine ni kwamba pia kuna maeneo mengine ambayo inaendelea kuyatenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Tunaendelea na mikakati ya kuwezesha wachimbaji wadogo wapatiwe maarifa mapya ya uchimbaji wa madini lakini pia tunahamasisha waingie katika vikundi vya uzalishaji ili Serikali iwe na namna bora zaidi ya namna ya kuwasaidia.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imesema kwamba hawa wachimbaji wakubwa wanatoa asilimia moja ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo. Je, Serikali inaridhika na asilimia hii? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa inaridhika na kiwango ambacho wanapata. Lakini niseme tu kwamba katika hili na katika shughuli ambazo Serikali inafanya shughuli zote zinaongozwa na sheria pamoja na taratibu zilizopo.

Sheria inatoa fursa kwa mtu mwenye shughuli yake ama kwa hili sasa kwa sababu tunaongelea suala la madini kwa watu wenye leseni za uchimbaji wa madini kuingia mikataba na wawekezaji.

Hili, suala la kiasi gani wagawane katika mapato yanayopatikana kwa kweli ni hiari ya washiriki katika makubaliano yanayohusika lakini sababu jambo hili ni suala ambalo linatokana na uhuru wa kisheria ambayo inayotoa kwa wananchi wake. (*Makofi*)

Na. 58

**Uchafuzi wa Mazingira**

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wengi wa Jiji la Mwanza, wamejenga milimani ambako ujenzi wa vyoo ni wa shida; na kwa kuwa, baadhi ya maeneo hayo hayana miundombinu ya maji na barabara:-

(a) Je, Ziwa Victoria linaathirika vipi kitaalam kutokana na ujenzi holela wa milimani wa karibu na ziwa hilo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, watu hao wanasababisha uchafuzi wa mazingira kwa watu wanaoishi chini ya milima hiyo katika kipindi cha msimu wa mvua?

(c) Kama ndiyo: Serikali ina mpango gani wa kuwahamisha wananchi hao ili kudhibiti uharibifu wa mazingira na milipuko ya magonjwa kama ya kipindupindu, homa za matumbo na kadhalika katika Jiji hilo?

**SPIKA:** Kilichoongezeka ni na kadhalika basi kwa sababu mstari wa nne una maneno ya kipindupindu na homa za matumbo. Majibu pamoja na masahihisho.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa maeneo ya ufukwe wa Ziwa Victoria, yanaathirika na maji kutoka makazi ya milimani na maeneo mengine kupitia mito na vijito mbalimbali vya Jiji la Mwanza.

Aidha, hali inakuwa mbaya zaidi pale baadhi ya wananchi wanapotumia mvua kutiririsha majitaka kutoka kwenye vyoo ambayo huingiza ziwani. Athari, zinazotokea ziwani ni pamoja na upungufu wa hewa ya oksijeni, uoto wa mwani uliokithiri, kujaa tope, magonjwa yanayoambatana na maji na wakati mwingine vifo vya samaki. Vyanzo vingine vya uchafuzi wa Ziwa Victoria, ni pamoja na majitaka kutoka Viwandani, pia na vyombo vya usafiri majini na mito inayoingia ziwani. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba watu waishio milimani wanasababisha uchafuzi wa mazingira kwa watu wanaishio chini ya milima hiyo, hasa

kipindi cha mvua. Uchafuzi huo siyo kwamba waishio chini yao tu, bali pia ni kwa Ziwa Victoria lenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo, Serikali kwa kupitia Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria, Mradi wa *Lake Victoria Environmental Management Project (LVEMP)* na Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Jiji la Mwanza, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uharibifu wa mazingira na uwezekano wa milipuko ya magonjwa ya kipindupindu na homa za matumbo, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Ujenzi holela umezuiwa na hakuna mwananchi anayeruhusiwa kujenga nyumba mpya katika maeneo hayo. Aidha, umeanzishwa mpango wa uboreshaji wa makazi holela kwa kuweka miundombinu kama vile barabara, mfumo wa majisafi na majitaka.

(ii) Chini ya Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, (*LVEMP*) upembuzi yakinifu wa mradi wa ukusanyaji wa majitaka katika Kata ya Igogo, umekamilika. Ujenzi wa mradi huo unategemewa kutekelezwa kwenye Awamu ya pili ya Mradi wa *LVEMP* utakaonza mwezi Desemba, 2007.

(iii) Wizara yangu kwa msaada wa *EU* inatekeleza mradi wa majisafi na majitaka maeneo ya Kirumba, Nyamanoro na Mkuyuni Viwandani. Pia, upanuzi wa mtandao utafanyika maeneo ya Mabatini. *(Makofi)*

(iv) Mradi mpya wa kupima viwanja vya bei nafuu umeanzishwa na utekelezaji wake unaendelea vizuri. Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanja hivyo ni sehemu za Ilemela, Nyegezi, Kiseke na Nyamhongole. *(Makofi)*

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi holela umeshasimamishwa katika milima hiyo, lakini bado kuna wananchi ambao tayari wanaishi kwenye milima hiyo na wanaendelea kuleta madhara wakati wa mvua kama alivyosema.

(a) Je, kwa nini Halmashauri ya Jiji la Mwanza, haipewi majukumu ya kuwahamisha wananchi wale na kuwajengea nyumba ili watoke kwenye milima hiyo na kuyaachia nafasi mawe yale kuonyesha hali nzuri ya mazingira katika milima hiyo.

(b) Kwa kuwa ujenzi holela umeshasimamishwa, lakini wananchi bado wanaendelea kuwepo. Je, ni hatua zipi sasa za ziada za kujenga mifungo ya maji taka na maji safi na baadaye kuyaunganisha kwenye michirizi ya mfumo wa maji. Je, ni lini hatua hiyo itatekelezwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba maradhi hayo hayaendelei zaidi? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji halafu utasaidiwa na Naibu Waziri wa Ardhi. Nimemwona akinipa ishara anataka kuongezea jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza ningependa kumfahamisha ya kwamba hatua zilizochukuliwa ni kwamba kuzuia wananchi wengine wasiongezeke kule na wale waliopo wanajengewa miundombinu ikiwemo barabara na njia za majitaka.

Mheshimiwa Spika, mradi huu kwa sasa unashughulikiwa na Wizara yangu ya maji pamoja na *project* inayoitwa *Lake Victoria Environmental Management* ambapo kwa hatua na hatua sehemu mbalimbali zinazohusika zitawekewa miundombinu hiyo.

Lakini pia hapo ningependa kumfahamisha ya kwanza zaidi ya hiyo ni kwamba sehemu zile ambazo zinaanza kupimwa za viwanja ambavyo ni vya bei nafuu wananchi hawa watashawishiwa kwa wale ambao wataona viwanja hivi ni vizuri watahamia huko. Mpaka hivi sasa tayari viwanja 10,000 vimeshapimwa katika sehemu mbalimbali ikiwemo Nyegezi, Kiseke, Bugarika, Busolwa na hali kadhalika. Pia hata hivyo ni kwamba Wizara yangu imeamua kwa kushirikisha kikamilifu maji safi na maji na ofisi yetu ya mabonde itafanyakazi hii sio kwa Ziwa Victoria peke yake ni kwa nchi nzima yenye mabonde tunashughulika tukishirikiana kwa pamoja na Wizara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa kwa kuwa linahusu mipango miji nadhani ndiyo maana Naibu Waziri wa Ardhi alitaka kuongezea majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (k.n.y. WAZIRI WA MAJI):** Mheshimiwa Spika, majibu mazuri yamekwishatolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, isipokuwa nilitaka kuwatoa wasiwasi wananchi kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi peke yake alitembelea eneo lote la Mwanza la watu waliojenga kule milimani na akaomba subira kwamba haitakuwa vema kuwaondoa wananchi hao kama hatuna pa kuwapeleka na ndiyo sababu Serikali imetoa mkopo kwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ili waweze kupima viwanja ambavyo kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, kwamba tayari viwanja 10,000 vimeshapimwa na wakatakapoanza kuviuza tutatoa mkopo zaidi ili viwanja vingi viendelee kupimwa na tunashukuru sana Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Na. 59

**Matatizo Yanayokikabili Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, miongoni mwa matatizo mengi ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi, kilichopo Wilaya ya Iramba ni pamoja na ukosefu wa umeme, gari, maji safi na vitendea kazi vingine:-

(a) Je, kwa kuwa Shirika la Umeme Tanzania lilishapima gharama za kuvuta umeme toka Kinampanda (km. 4) kwa gharama ya shilingi 83.0 milioni mwaka 2001, Serikali

itasaidiaje katika kuhimiza mradi huu utekelezwe pamoja na kwamba kunaweza kuwa na ongezeko kidogo la gharama?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa gari kwa ajili ya chuo hicho ambacho kipo mbali na Kiomboi na Singida ambako ndiko mishahara na mahitaji mengine ya lazima hupatikana?

(c) Je, ni lini Serikali itatoa *pump* mpya na kukarabati mabomba ili wanachuo waanze kupata maji ya uhakika wasiendelee kukosa masomo kwa kufuata maji zaidi ya kilomita tatu (3)?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jumla ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hamsini na nane (58) na vyote viko katika hali isiyoridhisha kimajengo, kimiundombinu na hata kwa upande wa vitendea kazi. Aidha, kutokana na hali halisi ya uchumi, Wizara yangu inapata Bajeti ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi. Suala hili linafahamika vyema. Waheshimiwa Wabunge, walilizungumzia sana wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2005/2006 na mwaka 2006/2007. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Msindai kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na Bajeti ndogo, Wizara yangu, Wizara imeshindwa kugharamia mradi wa kuvuta umeme kutoka Kinampanda kwa gharama ya Tsh. 83 milioni mwaka 2001. Badala yake Wizara imekiwekea Chuo mitambo ya umeme utokanao na nishati ya jua. Kwa sasa Wizara imekamilisha kujenga mitambo hiyo iliyogharimu kiasi cha shilingi 35.0 milioni kwa chuo hicho kimoja.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, Wizara yangu bado ina uwezo mdogo kifedha kuweza kuvinunulia vyuo vyombo vya usafiri. Badala yake Wizara imeendelea kuvifanyia ukarabati vyombo vilivyopo. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi, kina pikipiki mbili ambazo zitaendelea kufanyiwa matengenezo hadi tutakapoweza kununua vyombo vipya. Vile vile, katika mwaka 2005/2006, Wizara imenunua baiskeli kwa kila chuo ili zitumike kuwaendea wananchi na kutoa mafunzo nje ya chuo. Chuo cha Msingi kimepatiwa baiskeli tatu (3) na zinaendelea kutumika.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua tatizo kubwa la upatikanaji wa maji kwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msingi. Kwa sababu hiyo, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara ilituma kiasi cha shilingi 1,000,000/= kwa chuo hiki kwa ajili ya ukarabati wa mashine ya maji. Hata hivyo, kutokana na kukauka kwa chanzo cha maji pamoja na uchakavu wa mabomba ya kusambaza maji chuoni, menejimenti ya chuo iliamua kutumia fedha hizo kujenga tanki la kuvunia maji ya mvua lenye ujazo wa lita 10,000. Aidha, baadaye tanki lingine lenye ujazo wa lita 20,000 lilijengwa kwa ushirikiano kati ya Chuo, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na Shirika rafiki la

Janakala/Haud la nchini Finland kwenye eneo la chuo. Wakati huo huo chuo pamoja na wadau wengine wamebuni chanzo kipya cha maji ambacho hakihitaji pampu.

Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mbunge, pamoja na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, kwa kushiriki kikamilifu katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya Chuo cha Msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgana Msindai nilidhani jibu la Mheshimiwa Waziri lilikuwa la makini kabisa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri amesema hapa ndani kwamba Wizara yake inatengewa fedha kidogo kuliko Wizara zingine na kwa kuwa sasa hivi Bajeti ya mwaka unaokuja inaandaliwa:-

(a) Je, atakuwa tayari kuishawishi Serikali ili apate fedha za kutengeneza Chuo cha Msingi na vyuo pengine vyote nchini? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa Chuo cha Msingi, tulihitaji umeme na sasa hivi tumepata umeme wa jua na sasa hivi, Serikali ina mpango wa kusambaza umeme vijijini katika njia ambao umeme wa vijijini utapita na Chuo cha Msingi, kitakuwa mojawapo kuongezewa ipate umeme wa uhakika? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kuishawishi Serikali, ni kweli tumekuwa tukiishawishi Serikali, lakini Serikali inaangalia vipaumbele na kwa bajeti inayokuja tunaamini kuna matatizo mengi makubwa kama vile miundombinu ambayo imeharibika hasa katika Mkoa wake inahitaji matengenezo makubwa. Lakini bado tunaamini kwamba Serikali inaiangalia hii Wizara vizuri sana ili kuhakikisha vyuo hivi vinaendelea kama malengo yake yalivyo. Swali la pili kuhusu umeme, ule umeme ambao unapatikana wa jua tuliufanya hivyo kwa sababu *program* ya kupeleka umeme vijijini ilikuwa bado haijawafikia kwa hiyo, tunaamini wakati utakapofika na wao kule watapata na sisi tutajitahidi kuhakikisha kuwa umeme vijijini unapatikana. Lakini kwa sasa umeme wa jua unatusaidia zaidi kwa sababu hauna gharama kubwa.

Na. 60

**Muongo wa Afrika wa Watu Wenye Ulemavu (1999 – 2009)**

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa inafahamika kuwa Muongo wa Afrika wa Watu wenye Ulemavu ni kipindi cha miaka kumi, kati ya 1999 – 2009 ambacho kilipitishwa na viongozi wa uliokuwa Umoja wa Nchi za Afrika (*OAU*) na baadaye kuridhiwa na Umoja wa Afrika (*AU*) kwa nia ya kuboresha hali ya maisha na haki za watu wenye ulemavu hapa Afrika, ikiwa ni pamoja na Tanzania.

(a) Je, nini malengo makuu yaliyoainishwa ndani ya mkakati huo wa *AU* kwa ajili ya watu wenye Ulemavu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzindua na kuendesha mradi wa watu wenye ulemavu hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoridhia tamko la Muongo wa watu wenye Ulemavu, katika Afrika. Kufuatia tamko hilo nchi za Afrika zilipitishwa Azimio rasmi na kutangaza Muongo wa Afrika wa watu wenye ulemavu 1999 – 2009. Malengo makuu ya muongo huo ni pamoja na:-

- Kuwezesha kuwepo kwa sera ya watu wenye ulemavu ambayo itatoa mwongozo wa huduma kwa watu wenye ulemavu.

- Kutunga/kurekebisha sheria ambazo zitakidhi mahitaji na kuzingatia haki za watu wenye ulemavu.

- Ushirikishwaji/ushiriki wa watu wenye ulemavu katika nyanja mbalimbali za maisha ikiwa ni pamoja na uongozi wa ngazi mbalimbali fursa ya kushiriki katika maamuzi na masuala yote yanayohusu maisha ya kila siku ya jamii.

- Kuwepo na dawati la huduma kwa watu wenye ulemavu katika kila Wizara.

- Kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki na fursa sawa na wasio na ulemavu katika masuala yanayohusu jamii.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa malengo yaliyoainishwa yameanza kutekeleza na Serikali. Malengo yaliyotekelezwa ni pamoja na kuwepo kwa sera ya Taifa ya Maendeleo ya huduma kwa watu wenye ulemavu. Aidha, sheria zinazosimamia huduma kwa watu wenye ulemavu (Na. 2 na 3 za 1982) zinafanyiwa mapitio kwa lengo la kuwa na sheria moja inayotoa haki na kulinda ustawi wa watu wenye ulemavu.

Sanjari na hatua hizo, Serikali imeridhia Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Fursa Sawa kwa watu wenye ulemavu. Kadhalika ushiriki wa watu wenye ulemavu umeboreshwa na wanapata nafasi ya kujumuika katika masuala mbalimbali ya kijamii. Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya mikutano ya mashauriano kuhusu utekelezaji wa muongo. Mikutano hii imepangwa kufanyika kabla ya mwisho mwaka wa fedha 2006/2007. Lengo ni kuwa na mkakati kabambe wa kutekeleza malengo ya Kitaifa kuhusu watu wenye ulemavu.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kipindi cha Muongo ni kati ya mwaka 1999 hadi mwaka 2009 na kwa kuwa utekelezaji wake umebaki miaka mitatu tu.

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuna haja ya kutangaza Muongo wa Afrika kitaifa hapa nchini Tanzania baada ya kumalizika Muongo wa Afrika mwaka 2009? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa watu wenye ulemavu ni wananchi wa nchi hii. Je, Waziri yuko tayari kutueleza ni kwa nini Serikali imechukua muda mrefu kutekeleza Muongo wa Afrika wa watu wenye ulemavu hapa nchini Tanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali inaendelea kufanyia kazi ili kuweza kuhakikisha kwamba mkakati kabambe unaendelezwa ili kuweza kuona kwamba haya yote yaliyokuwa yamezungumzwa yanatekelezwa.

Swali la pili, Serikali sio kwamba imeshindwa kutekeleza yale ambayo yamezungumziwa katika Muongo. Ni kweli nakubali kwamba kuna haja ya kutangaza lakini kama nilivyozungumza katika swali langu la msingi ni kwamba kama nilivyozungumza mambo ambayo yameshafanyiwa kazi hii inaonyesha wazi kabisa kwamba Serikali haipuuzii na kwamba tunaendelea ili kuweza kuona kwamba tunaitangaza, baada ya Muongo 2009 lakini tutaendeleza nchi yetu ya Tanzania ili kuhakikisha kwamba zile haki na fursa zote zinazohusu walemavu zinatekelezwa na kushughulikiwa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa moja ya malengo makubwa ya Muongo huu, ni kuwawezesha walemavu washiriki katika shughuli za Taifa na kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Kazi, imejitahidi kufungua vioo mbalimbali kwa kuwafunza walemavu na kwa kuwa kikwazo kikubwa kwa ajili ya walemavu ni sheria Na. 2 ya mwaka 1982. Je, ni lini sasa Serikali itafanya marekebisho ya sheria hiyo ili kikwazo hiki kwa walemavu kwa ajili sasa kiweze kiondoka na hasa kwa kuwa Serikali ndiyo mwajiri mkuu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba hizi sheria ziko katika mapitio kwa lengo la kurekebisha. Lakini sio hilo tu sheria zote ambazo zinagusa masuala yote ya walemavu zitafanyiwa mapitio ili kuhakikisha kwamba sheria zinakwenda sambamba na zile huduma ambayo Serikali, inatakiwa kutoa kwa wale walemavu walioko sio Tanzania tu, lakini katika Afrika nzima.

Na. 61

**Unyanyasaji wa Wajane**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna baadhi ya familia zina tabia mbaya ya kuwanyanyasa, kuwatenga na kuwanyang'anya mali wajane wanawake wanaofiwa na waume zao na kwa kuwa mateso hayo yanayowapata wanawake wajane ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa sababu ni haki yao kurithi mali ambazo walizichuma wakiwa pamoja na waume zao na ndizo zingesaidia katika matunzo ya watoto.

(a) Je, ni wajane wangapi wametelekezwa na kunyang'anywa haki zao toka mwaka 2005 – 2006?

(b) Je, ni hatua gani zimeshachukuliwa kwa wale wanaofanya vitendo hivyo vya unyanyasaji wa wanawake wajane?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jamii yetu ya Watanzania, zipo baadhi ya familia ambazo huwanyanyasa, kuwanyang'anya mali na kuwatenga wajane. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba vitendo hivyo vinaashiria ukiukwaji wa haki za binadamu hususani haki ya kurithi mali. Tabia hii inasababisha wajane wengi kushindwa kujihudumia na pia kuwahudumia watoto walioachiwa na marehemu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya utafiti kuhusu majibu ya swali hili nimebaini kuwepo kwa ugumu wa kupatikana takwimu halisi za wajane waliotelekezwa na kunyang'anywa mali zao. Hii inatokana na ukweli kwamba siyo matukio yote hutolewa taarifa kwenye vyombo vya habari. Aidha yale yanayowasilishwa kwenye vyombo vya sheria huwahusu wadaawa wenyewe na masuala yao huishia mahakamani. Pia walalamikaji huweza kufikisha malalamiko yao kwenye Ofisi mbalimbali za Serikali, Taasisi zisizo za kiserikali pamoja na taasisi za kidini. Mahakama zimekuwa zikitoa maamuzi kwenye kesi zinazofikishwa mbele yake kwa kuzingatia ushahidi unaotolewa.

Kwa watuhumiwa wanaotenda makosa ya jinai kama vile kuwapiga na kuwadhalilisha wajane hawa huwadhibiwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe rai kwamba sote kwa pamoja tushirikiane kuelimisha wananchi wetu kuachana na tabia ya kuwanyanyasa na kuwanyang'anya mali wajane kwa kuwa inakiuka misingi ya haki za binadamu. Mjane na watoto walioachwa na marehemu wanastahili kuendelea katika nyumba ambayo imejengwa na marehemu peke yake wakati wa ndoa au nyumba iliyojengwa kwa ushirikiano kati ya mjane na marehemu. Aidha, wanastahili kufaidika na mali nyingine zilizoachwa na marehemu.

Tuwasaidie wajane kwa kuwashauri, kuwaongoza na kuwaelekeza mahali ambapo wataweza kupata haki zao. Njia ya elimu kwa umma itasaidia sana tukiitumia vizuri. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiw Spika, pamoja na majibu mazuri ya a Naibu Waziri. Naomba kuuliza, kwa kuwa mbali na kuwanyang'anya mali wanawake hawa wajane, lakini kibaya zaidi ni kule kuwanyang'anya hata na watoto waliowazaa pamoja. Je, thamani ya wanawake iko wapi?

Swali langu la pili. Kwa kuwa baadhi ya wanawake wanaofiwa na wanaume zao hunyang'anywa mali lakini wanaume wanaofiwa na wake zao hawanyang'anywi mali. Je, Serikali haioni kuwa huko ni kuendeleza mfumo dume na utakomeshwa lini?

**SPIKA:** Lo, swali zito sana hili. Mheshimiwa Naibu Waziri! Aha, Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa majibu mazuri sana ya msingi. Vile vile napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Faida Bakar kwa kuweza kuuliza swali la nyongeza na kunipa nafasi ya kuweza kuhamasisha jamii kwanza kwamba watoto ni wa baba na mama. Anapotokea mmoja anakufa basi yule anayebaki ndiye wa kwanza kuangalia watoto hawa na wana ndugu basi wasaidie yule aliyebaki siyo kuwanyang'anya watoto na kadhalika. *(Makofi)*

Na kuhusu swali lake la nyongeza la pili, ni kweli wanawake ndiyo wanaopata adha kubwa inapotokea waume zao wamefariki na ni mara chache sana wanaume wanapata adha hiyo wake zao wanapofariki. Tunajaribu kujenga jamii ya kistaarabu, tunajaribu kujenga jamii ambayo amani inapewa kipaumbele sana. Na kunyanyasa watoto wa marehemu ni njia moja ya kuleta migogoro na kuvunja amani Tanzania. Kwa hiyo, ningeomba jamii kwanza isiwanyang'anye mali, wake wa marehemu badala yake iwasaidie kuweza kumudu au kuhimili matatizo walioachiwa na waume zao. Lakini kwa nyongeza tu ningesema kwamba wanawake nao wachangamke wanaume zao wanapofariki wasimamie mirathi badala ya kuwaachia wengine kusimamia mirathi. Kwa sababu mara nyingi wale wanaosimamia mirathi wanaamini kama wao sasa wameachiwa ile mali. Kwa hiyo, inakuwa vizuri zaidi wanawake nao wasaidiwe kusimamia mirathi badala ya kuwaachia wana ndugu ambao baadaye ndio wanaamua kwamba ile mali ya marehemu inakuwa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa tuwasaidie wajane, kwa sababu kwa kweli wanapata adha. Naipongeza Mahakama ya Tanzania kwa sababu wametenga *desk* maalum kwa ajili ya mirathi na napenda waendelee kuwasaidia wajane ili basi watoto wa marehemu wasipate matatizo na wajane wenyewe. *(Makofi)*

Na. 62

**Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Mbeya**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mbeya kuna fursa nyingi zikiwemo kitovu cha kilimo cha kisasa, upatikanaji wa Nishati ya Makaa ya Mawe - Kiwira, Madini ya *Phosphates* na kuna barabara nzuri, reli ya *TAZARA* kwa ukaribu na nchi za Malawi, Zambia na *Congo DRC:-*

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa wakati umefika wa kujenga kiwanda cha mbolea Mkoa Mbeya?

(b) Je, Serikali itaanza lini kutengeneza *Mini Tiger Plan 2020* katika Mkoa wa Mbeya?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwilugula Mpesya Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Mkoa wa Mbeya unazo fursa nyingi zikiwemo za kuwa kitovu cha kilimo cha kisasa, upatikanaji wa nishati ya Makaa ya Mawe – Kiwira, madini ya aina ya *phosphates* na nyinginezo ambazo zinatoa fursa nzuri ya uwezekano wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea Mkoani Mbeya kwa kutumia *phosphates* zilizopo humo. Kwa kutambua hivyo, Wizara yangu kupitia Shirika la Maendeleo ya Taifa *(NDC)* inakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi waweze kuwekeza katika ujenzi wa kiwanda cha mbolea Mkoani Mbeya kitakachohudumia Mikoa ya Kusini ambayo ni maarufu kwa kilimo. Mpaka sasa *NDC* imekwishauza wazo hili la ujenzi wa kiwanda cha mbolea kwa makampuni ya *Heavy Oil Field Services* ya *USA* na *PCC – AG* ya Ujerumani ambayo yote yanapendelea kuwekeza katika viwanda vya madawa *(Chemical industries). NDC* pia itaendelea kuuza wazo hili kwa wawekezaji wengine watakaoonyesha nia ya kuwekeza katika kiwanda cha mbolea huko Mbeya.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilitengeneza mpango wa *Mini tiger plan 2020* tangu mwezi Desemba 2004 kwa ajili ya Mikoa yote nchini. Mkakati huu utatekelezwa kwa kutumia dhana ya kanda maalum za kiuchumi *(Special Economic Zones).* Aidha, Sheria ya kuanzisha maeneo maalum za uwezekezaji rasilimali *(Special Economic Zones Act. 2006)* iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili mwaka jana inatoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji rasilimali katika maeneo hayo ya *SEZ* watakaokuwa wanazalisha na kuuza bidhaa katika soko la ndani na nje. Hivyo basi, jukumu la kila Mkoa kubaini na kutenga maeneo maalum ya kuendelezwa kwa mpango wa *SEZ.* Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kuhamasisha mpango huo katika Mkoa wake wa Mbeya. Jukumu la Serikali ni kusaidia kuwekeza miundombinu muhimu kama ile iliyotajwa kwa Mkoa wa Mbeya na hatimaye haitegemewi kuwekeza moja kwa moja katika uzalishaji au biashara. Hilo ni jukumu la wawekezaji wa ndani na nje.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa ridhaa yako kabla sijauliza swali dogo la nyongeza, tutumie nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali na kumpongeza Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Katibu Mkuu wake Dr. Tax Bamwenda, kwa kutoa idhini ya kutumia maeneo ya *SIDO* kwa ajili ya wafanyabiashara wa soko la Mwanjelwa lililoungua. Mimi kama Mbunge nimefarijika sana na kasi ya Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mbeya, Mbeya Mjini, pamoja na Mbeya Vijijini wamehamasika vilivyo kutaka kujenga kiwanda cha mbolea na tayari sasa hivi wamechanga zaidi ya shilingi milioni 8 kwa ajili ya azma hiyo. Na kwa kuwa kazi ya Serikali ni kuwa mwezeshaji. Je, Serikali itawawezesha vipi wananchi hawa ili kutimiza azma yao hiyo ya kutaka kujenga na kumiliki kiwanda cha mbolea?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda na mimi nimshukuru na kumpongeza kwa jitihada zake za kusimamia wananchi wapiga kura wake wa Jimbo la Mbeya Mjini ambao wengi ni wafanya biashara na ndiyo maana Serikali nayo inaitikia mwito wa yeye kama Mbunge kuweza kushirikiana naye.

Nataka nimhakikishie kwamba Serikali siku zote itaendelea kushirikiana naye katika kuwahudumia wananchi wa Jimbo lake. Sasa swali la kwamba wananchi wameshahamasika na wameazimia kwamba waanzishe kiwanda kile na hatimaye kuweza kumiliki wenyewe. Napenda nipongeze juhudi hizo za wananchi ambazo zimefikiwa. Lakini kama nilivyokuwa nimejibu katika swali la msingi kwamba kuna baadhi ya makampuni ambayo sasa hivi yamekwishajitokeza kutaka kuwekeza katika ujenzi wa kiwanda kile cha Mbeya. Ushauri wangu ambao naweza kuutoa ni kwamba ni vizuri pengine kuwe na utaratibu wa ubia kati ya wananchi hao wa Mkoa wa Mbeya ambao wako tayari ili waweze wakashirikiana katika kukimiliki kiwanda hicho. *(Makofi)*

Kwa upande wa Serikali katika shughuli za uwekezaji za kuwezesha nadhani fursa ziko nyingi ambazo Mheshimiwa Mbunge anaweza akazifuatilia kwa sababu Serikali imeshatoa vipaumbele vingi kwa ajili ya kuwawezesha wananchi.

Na. 63

**Uuzaji wa Nyumba za Serikali**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliuza nyumba za Serikali kwa watumishi wake kati ya mwaka 2001 na 2005 kwa kilichoitwa Maamuzi ya Serikali na kwa kuwa, wananchi wengi wakiwemo Wabunge walilalamikia zoezi hilo na kwa kuwa hivi karibuni

kumetokea tuhuma nyingi kwenye vyombo vya habari na Serikali haijatoa taarifa wala tamko rasmi kuhusu tuhuma hizo na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa:-

(a) Kwa kuwa nyumba za Serikali ni mali ya Watanzani wote, wananchi wana haki ya kufahamu ni nyumba ngapi zimeuzwa tangu zoezi lilipoanza hadi Desemba 2005, na ni watumishi gani kwa majina na kwa cheo gani waliuziwa nyumba hizo na ziko kwenye *plot* namba zipi na eneo gani kwa kila nyumba?

(b) Je, kabla ya wahusika kuuziwa, nyumba hizo zilikarabatiwa lini na kwa gharama gani na ziliuzwa kwa kiasi gani kwa kila nyumba na ni fedha kiasi gani kwa kila nyumba?

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya tuhuma zilizojitokeza magazetini siku za hivi karibuni hasa gazeti la Rai na kama tuhuma hizo ni za kweli. Serikali iko tayari kuunda Tume ya Bunge kuchunguza uuzaji wa nyumba hizo ili kuondoa malalamiko na manung'uniko mengi yaliyosababishwa na zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ufafanuzi na kuweka kumbukumbu sahihi kuwa, Serikali ilianza kuuza nyumba zake kwa watumishi wa Serikali mnamo mwezi Mei 2002 na sio mwaka 2001 ingawaje mchakato mzima wa zoezi hilo ulianza mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo, naomba sasa nijibu swali la msingi la Mheshimiwa Dr. Wilbroad Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nyumba zilizouzwa tangu zoezi hilo lianze hadi Desemba, 2006 ni nyumba 7,921. Nyumba hizo zimeuzwa kwa watumishi wa umma waliokuwa wanaishi katika nyumba hizo bila kujali vyeo wala nyadhifa zao. Aidha, kutokana na uwingi na ukubwa wa kumbukumbu zenye majina ya mitaa na namba za viwanja husika, imekuwa vigumu kuvitaja/kuvionyesha/kuvilea mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa vile suala la kuuza nyumba limekuwa la kisheria kwa maana ya kuwepo mikataba baina ya mtumishi (mtu binafsi) na Serikali, katika hatua hii haitakuwa sahihi kuyataja majina ya watumishi hayo hadharani bila ridhaa yao. Hata hivyo, Wizara yangu iko tayari kumwonyesha kumbukumbu hizo Mheshimiwa Mbunge akifika katika Ofisi zetu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kabla ya maamuzi ya kuuza nyumba zake ilijiwekea utaratibu wake wa kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara nyumba hizo kila ilipowezekana. Mara baada ya Serikali kufikia maamuzi ya kuuza nyumba kwa watumishi wake, lilitolewa agizo lililokataza kufanyia matengenezo nyumba zote zilizokuwa zimeainishwa kuuzwa. Hata hivyo, wakati wa uuzaji wa nyumba hizo utaratibu uliotumika na unaoendelea kutuimka ni kufanya uthamini wa kila nyumba na

kuiuza kwa  kuzingatia thamani halisi ya nyumba hiyo inayozingatia pia ukarabati uliofanyika kabla ya zoezi la uuzaji kuanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sababu nilizozitoa katika kipengele (a) hapo juu, imekuwa vigumu kutoa takwimu za bei ya kuuzia kila nyumba, lakini kwa ujumla wake kufikia tarehe 31/12/2006, nyumba 7,921 zilizokwishauzwa; ziliuzwa kwa shs. 59,559,174,879/= ambapo kati yake shs. 29,145,360,913.53 zilikwishalipwa na shs. 30,413,813,965.47 bado zilikuwa zinaendelea kulipwa na watumishi husika.

(c) Mheshimiwa Spika, hata kabla ya tuhuma kutolewa na baadhi ya vyombo vya habari na kama tulivyojibu kwenye Bunge hili katika Mkutano wa Tano wa Bunge, Serikali ilikwisha chukua hatua za awali kwa kufanya uchunguzi ili kubaini kasoro zilizojitokeza katika zoezi hili na pale ilipoonekana kuna kasoro au mapungufu, mikataba ya nyumba hizo ilisitizwa. Aidha, Serikali kwa kutambua kuwa zoezi hili ni kubwa ambalo linaweza kuwa na mapungufu wakati wa utekelezaji wake, iliamua kuunda Kamati ya Uchunguzi inayoongozwa na Bibi A.H. Nyondo (Mkurugenzi wa Maadili, UTUMISHI). Madhumuni na lengo la kufanya uchunguzi ni kuainisha mapungufu yaliyojitokeza wakati wa zoezi zima la kuuza nyumba za Serikali.

Hivyo, ninashauri Bunge lako Tukufu livute subira hadi hapo Kamati hiyo itakapokuwa imekamilisha kazi yake na kuwasilisha ripoti yake Serikalini ambapo Serikali itaamua hatua za kuchukua kulingana na yatakayokuwa yamejitokeza kwenye ripoti hiyo. Kamati hiyo inatarajiwa kukamilisha uchunguzi wake mwisho wa mwezi huu wa Februari. Kwa sababu hiyo Serikali haioni haja ya kuundwa kwa Tume ya Bunge kuchunguza suala hili.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu yasiyoridhisha ya Naibu Waziri. Kwanza nilitaka kujua pamoja na masahihisho ya Waziri kwa vile mwaka 2001 tayari tulikuwa na Sheria ya Manunuzi yaani *Public Procurement Act* inayotaka manunuzi yote ya mali ya Serikali yafanyike kwa njia ya tenda iliyo wazi. *(Makofi)*

Ni Sheria gani ilitumika kuuza nyumba hizi na ambayo haikufuata taratibu za kawaida za tenda. Je, Serikali inasema nini katika utaratibu huu uliokiuka taratibu za tenda?

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwamba imekuwa vigumu kuleta taarifa ndani ya Bunge kama swali lilivyotaka, na kwa kuwa taarifa zingine amesema ni ndefu na kwa utaratibu wa kawaida taarifa inapokuwa ndefu inaandikwa kwa maandishi na kupewa Mbunge mhusika ili atimize wajibu wake wa kuisimamia Serikali kupitia Bunge. Je, Waziri sasa anaeleza nini Bungeni kwamba taarifa zinazotakiwa Bungeni zinapowekwa siri je, Serikali inasema Bunge isitimize wajibu wake wa kusimamia Serikali kupitia kifungu cha ibara ya 63(b) Kifungu cha pili cha Katiba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hili la pili, nadhani hakusema ni siri kwa maana hiyo. Alisema mkitazama ni viwanja na nyumba 7,000 na uliuliza *plot* namba, mahali zilipo, taarifa hii

ingekuwa mzigo mkubwa. Lakini ameruhusu Waheshimiwa Wabunge mkaione huko Wizarani, nadhani inatosha tu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. anajua vile vile kwamba mimi ni mtaalam wa *procurement* na kwa hiyo katika nyanja hiyo siwezi kubabaika. Nataka nimhakikishie kwamba katika Sheria hiyo ya *Public Procurement Act* vile vile kuna *single sourcing* ambayo unaweza kununua au kuuza kwa mtu mmoja. Serikali iliamua kuwauzia wale walioko kwenye nyumba hizo na kwa hiyo, kulikuwa hakuna sababu ya kufanya *tendering* kwa sababu haikuwa ni *public you no sale,* ni kuwauzia wale walioko ndani ya nyumba hizo. Kwa hiyo, kulikuwa hakuna sababu ya kufanya *tendering. (makofi)*

Lile la pili umelijibu nashukuru sana Mheshimiwa Spika.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilikuwa naomba nifahamu kwa kuwa sasa tumeshajifunza matatizo mbalimbali ambayo yalikuwa yamejitokeza katika uuzaji wa nyumba zilizopita. Na kwa kuwa bado kunahitaji watumishi kuweza kupewa nyumba, yaani kuuziwa nyumba ili wasiwe na vishawishi vya rushwa kwa kuwa wanakuwa wanatafuta hela za kujengea nyumba. Je, Serikali haioni kuwa ni muhimu kutengeneza utaratibu nzuri ili kuendelea kuwawezesha watumishi hao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, tumeeleza katika Bunge hili na nataka niweke wazi na hili lisiendelee kuonekana kuulizwa mara nyingi kwamba katika Sera ya Serikali ya sasa Serikali haitatumia tena bajeti yake kwa kujenga na kuuza sio kwamba lile suala la kujenga na kuuza kama Serikali. Kwa kutumia bajeti yake Serikali itaendelea kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi wake wale wanaostahili kupewa nyumba kwa mujibu wa ajira zao. Tutaweka Bajeti kila mwaka na tutaongeza na hizi pesa tunazopata kutoka kwenye mauzo ya nyumba tulizokwisha uzwa kwa ajili ya kujenga nyumba kwa watumishi na hizi nyumba zitabaki kuwa mali ya Serikali yaani *tied quorters.*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watumishi wa umma na hata Watanzania kwa ujumla wanahitaji ku-*own* nyumba zao. Kumiliki nyumba zao wenyewe. Kwa hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi, lakini vile vile kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupitia Shirika la Nyumba litaendelea kuweka utaratibu wa kuwezesha Shirika hilo na Sekta binafsi kuingia katika uwekezaji wa kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi na Watanzania wengine ili waweze kuzinunua au kwa mkopo wa muda mrefu au kwa fedha taslimu. Hiyo Sera ipo na Serikali ita-*support* juhudi kama hizo ambazo zitawekwa na sekta binafsi na Shirika la Nyumba. *(Makofi)*

Na. 64

**Uchakavu wa Barabara ya Makambako – Songea**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k.n.y. MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa kiwango cha tabaka la lami katika barabara ya kutoka Makambako hadi Songea kwenye eneo kati ya kijiji cha Kifanya (Njombe) na mji wa Songea imechakaa sana na kusababisha viraka vya lami na udongo; na kwamba kama hali hiyo itaachwa bila kufanyiwa kazi itaendelea kuharibika na kupunguza usalama kwa watumiaji wa barabara hiyo na pia gharama za ukarabati zitazidi kuwa kubwa kadri inavyoendelea kuharibika:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka za kuikarabati barabara hiyo kwa kuiongeza lami hususani katika eneo la Kifanya hadi Songea?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makambako – Songea yenye urefu wa kilomita 295 ni brabara kuu iliyojengwa kwa kiwango cha lami nyepesi *(surface dressing)* tangu mwaka 1986. Kwa hiyo, barabara hii imefika muda wa kuifanyia ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa fedha za ukarabati mkubwa ndiyo unasababisha tufanye matengenezo ya hapa na pale ili barabara hiyo iendelee kutumika hadi hapo fedha za ukarabati mkubwa zitakapokuwa zimepatikana. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* kuanzia mwaka 2002/2003 imekuwa ikiboresha barabara hiyo kila mwaka maeneo yale ambayo ni korofi ambapo hadi kufikia mwaka huu wa fedha 2006/2007 jumla ya Tshs. bilioni 4,404.640,000 zimetumika kwa matengenezo hayo. Kati ya fedha hizo, Tshs. bilioni 1,265.210,000 zimetumika kwa matengenezo ya kawaida na Tshs. bilioni 3,139.430,000 zimetumika kwa matengenezo maalum. Juhudi zinaendelea kutafuta fedha za kukarabati barabara hii kwa kiwango cha kutosheleza. Kwa vile fedha za matengenezo kutoka Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* hazitoshi, Serikali inaangalia uwezekano wa kutenga fedha za maendeleo kwa miaka ijayo ili kugharamia matengenezo makubwa ya barabara hii.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kwa kweli hali ya barabara hiyo, ambayo ni kiungo muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, kujifungua na mikoa mingine ya jirani iko katika hali mbaya sana. Na kwa kuwa amekiri kwamba sasa Serikali inafikiria kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo hayo. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwahakikishia wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwamba katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 angalau Serikali ianze kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo hayo?

Pili, kwa kuwa barabara hiyo, inaunganisha pia na barabara nyingine kubwa sana ambayo imeanza kutengenezwa toka mwaka jana inayounganisha nchi ya Tanzania na Msumbiji kutoka barabara hiyo kuingia barabara ya Mitomoni na barabara hiyo kwa sasa pia hali yake imeanza kuwa mbaya sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutenga pia fedha za matengenezo ya barabara hiyo ya Songea-Mitomoni sambamba na matengenezo hiyo ya Makambaku-Songea?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi Serikali katika Bajeti ya miaka inayokuja kuanzia mwaka huu, itaendelea kutenga fedha za kutosha ili barabara hiyo ya Makambaku-Songea iweze kujengwa kwa kiwango kikubwa. Lakini upatikanaji wa fedha hizo itategemea sasa Bajeti itakayokuwa imeidhinishwa kwa sababu tunaweza tukaomba fedha kama Wizara lakini kulingana na mahitaji ya ujumla ya Serikali nzima tukawa tumeshindwa kupata fedha tulizoomba. Lakini sisi tunaahidi kwamba tutafanya hivyo mwaka huu na miaka mingine ijayo ili barabara hiyo muhimu sana ijengwe kwa kiwango kikubwa.

Kuhusu barabara ya Songea kwenda Mitomoni, kama yeye anavyojua mwaka jana nilitembelea barabara hiyo mpaka kwenye daraja la *Unity Two Bridge* inayounganisha nchi yetu na Msumbiji kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma. Ni kweli barabara hiyo inahitaji kutengenezwa. Na kwa kweli sisi kama Wizara tumeanza kazi hiyo. Katika mwaka 2005/2006 tulitenga milioni 551 kuikarabati na zilitumika na mwaka huu wa fedha unaoendelea tumetenga milioni 114 za kuendelea kutengeneza barabara hii ili iweze kupitika. Lakini vile vile daraja la *Unity Two Bridge* ambalo linaunganisha nchi mbili tumetenga fedha mwaka huu milioni 85 kwa bahati mbaya hazikutosheleza kwa sababu mahitaji ya kujenga tu daraja kwa maana ya nguzo ni milioni 167 tunaendelea kutafuta fedha zingine ili kazi ile mkandarasi aweze kuianza. Ni kweli barabara hii ni muhimu na kama nilivyomuahidi wakati fulani, kwa sababu ni barabara ambayo itaunganisha nchi mbili, tunafikiria kuipandisha ili iwe *trunk road*. Lakini ujenzi wake kwa kiwango cha lami itategemea upatikanaji wa fedha na wenzetu wa Msumbiji wanaionaje hii barabara. Maana yake huwezi kufikisha lami kwenye mto pale darajani na wenzenu kule hawana barabara. Kwa hiyo, tutafanya mawasiliano kabla ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 65

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi – Magoma, Danira na Bungu**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu katika Jimbo la Korogwe Vijijini wananchi wengi wana simu za mkononi na kwa kuwa kwa muda mrefu Kampuni za *Vodacom,, Celtel* na *Tigo* zimekuwa zikifanya utafiti ili ziweke mitambo yao katika Taarifa za Magoma na Bungu; lakini tafiti hizo hazijaonyesha matunda kwa wananchi wa maeneo hayo:-

Je, ni lini huduma hiyo itafika katika taarifa hizo hasa ikizingatiwa kuwa hali ya uchumi katika kilimo na madini ni nzuri katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Tuondoe tu basi. Tuondoe tu?

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, naomba liondolewe, lifutwe hili neno Dindira.

**SPIKA:** Sawa sawa! Nadhani sasa swali limekuwa jepesi.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Kampuni za *Vodacom, Celtel* na *Tigo* zimekuwa zikifanya utafiti ili ziweke kuweka mitambo yao katika Tarafa za Magoma, na Bungu. Matokeo ya tafiti au tathimini hizo yamewezesha kuweka mipango yao ya kazi katika programu za maendeleo za kila kampuni. Aidha, Kampuni ya *Vodacom* tayari inao mpango wa kujenga mnara Msamaka ambao utatoa huduma maeneo yote ya Magoma na Dindira, naomba niseme na Dindira. Maeneo ya Bungu yatapata huduma kutoka Mnara wa Korogwe – Namba 2. Serikali kwa kushirikiana na watoa huduma itaendelea kubuni, kupanga na kuteleza programu za maendeleo ya sekta ya mawasiliano ili huduma ziwafikie wananchi wote nchini.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa mnara wa *Celtel* katika Tarafa ya Magoma unaendelea katika kijiji cha Maheza – Nguru ambapo huduma itaanza kutolewa ifikipo mwishoni mwa mwezi Julai mwaka huu. Aidha tathimini ya soko katika Tarafa za Dindira na Bungu inatarajiwa kufanyika wakati wowote kuanzia sasa. Ni kweli kampuni ya *Tigo* imekuwa ikifanya utafiti wa uwekaji mnara katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, na imeamua kuweka mnara katika kijiji cha Magoma. Kazi ya kuweka mnara huo itaanza kabla ya mwezi Mei mwaka huu. Mnara huu utasaidia wananchi wa Magoma, Dindira na wale wanaoishi katika vijiji vilivyopo karibu na Taarifa hizi.

Kwa upande wa *Zantel,* Mheshimiwa Spika, huduma za mawasiliano zitaanza kutolewa mara tu mnara wa *Vodacom* utakapokamilika kujengwa. Utaratibu huo ni kwa mujibu wa makubaliano yaliyopo baina ya kampuni hizo mbili.

Na. 66

**Meli za Kivita kufanya ziara za Kirafiki nchi kwetu**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya nyuma meli za kivita kutoka nchi za kigeni zilipofanya ziara za kirafiki nchini mwetu zilitia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam

na ya Zanzibar, lakini inavyoonekana utamaduni huo umetoweka sasa na badala yake ziara hizo hulishia Bandari ya Dar es Salaam:-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili, ni kwa nini ziara hizo zinaishia kwenye Bandari ya Dar es Salaam tu?

(b) Je, Jeshi letu la majini *(NAVY)* linashirikisha vipi Kikosi Maalum cha Kuzuia Magengo KMKM katika masuala ya taaluma inapotokea nafasi za masomo katika nchi za kigeni?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singkh Hoogan, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limekuwa likipokea ugeni wa wanajeshi kutoka nchi mbalimbali. Ugeni uliowahi kutembelea Jeshi letu ni pamoja na Jeshi la majini *(NAVY)* kutoka Ufaransa, Ujerumani, India, Pakistan, Kenya na Afrika ya Kusini. Lengo la ziara hizo ni kuimarisha uhusiano baina ya majeshi yetu na yale ya nchi rafiki pamoja na kujionea na kujifunza mambo mbalimbali yakiwemo yakimaendeleo na ya kitalii. Majeshi hayo ya majini *(NAVY)* wanapotembelea nchi yetu huja na meli zao za kivita. Baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kutia nanga katika bandari ipi Tanzania kwa meli za kivita za nchi rafiki hutolewa na jeshi la nchi inaotutembelea. Jeshi linalotutembelea huomba kutia nanga katika bandari ambayo wao wanaona inatosha kwa ziara yao. Historia inatuonyesha kuwa baadhi ya meli za kivita za nchi rafiki ziliwahi kutembelea Tanzania na kuomba kutia nanga bandari ya Dar es Salaam na ile ya Zanzibar. Baadhi vilevile ziliwahi kututembelea na kuomba kutembelea bandari ya Dar es Salaam tu na baadhi zilitutembelea bandari ya Zanzibar tu. Sababu kubwa inayopelekea hali hii ni lengo la ziara, ukubwa wa meli yenyewe na gharama ya ziara hiyo.

(b) Jeshi la *(Navy)* ni chombo cha Muungano kina ushirikiano mzuri sana na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ambacho sio chombo cha Mungano. Ushirikiano huo upo katika masuala mbalimbali yakiwemo yale ya taaluma. Jeshi la Majini haliwajibiki kwa KMKM, lakini kutokana na ushirikiano huo, linaendesha mafunzo mbalimbali ya ubaharia katika chuo chake kilichopo Kigamboni ambapo askari kutoka Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) wanashiriki katika mafunzo hayo. Kwa upande wa mafunzo nchi za nje, maafisa wa KMKM na wale wa *NAVY* wanapelekwa nchi za nje kwa mafunzo pale msaada unapopatikana. Siku hizi vyuo vingi duniani vinajiendesha, kwa maana hiyo nafasi za msaada zimepungua sana. Hata hivyo kutokana na majukumu kuwa tofauti sio kila nafasi ya mafunzo itamhusisha askari wa KMKM.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kumwuliza Naibu maswali mawili madogo tu, naomba nieleze ni mara ya mwisho ilikuwa meli gani na ilitoka nchi gani na ilitia nanga wapi.

La pili kwa kuwa masuala haya ya NAVY na meli za kivita zinahusiana sana na masuala ya rada na sasa hivi kuna sakata la rada katika nchi yetu. Je, Mheshimiwa Waziri anaeleza nini kuhusu hili?

**SPIKA**: La kwanza itabidi liandikwe swali, ili Wizara hii iweze kujiandaa, kwa sababu takwimu za mwaka mzima lini iliingia meli bandari ipi na hakika Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami linahitaji maandalizi, kwa lile la pili majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, tarehe 24 mpaka 27 mwezi wa Aprili, 2006 meli mbili kutoka Kenya za *NAVY* zimefunga gati Zanzibar na tarehe 8 hadi tarehe 12, meli moja ya *NAVY* kutoka Ufaransa imefunga gati Zanzibar peke yake.

Mheshimiwa Spika, na kwa hili la pili nachoweza kusema ni tamko ambalo Mheshimiwa Rais amekuwa akilitoa katika vikao, katika mikutano mbalimbali. Timu kutoka Uingereza inachunguza sakata la rada, kama alivyosema Mheshimiwa Rais na mimi naomba ninukuu, ikibainika kwamba rada ile tumeuziwa kwa bei ya juu kuliko bei yake, Serikali ya Tanzania tutalazimika kuidai Serikali Uingereza fedha za ziada.

**SPIKA**: Waheshimiwa kwa kuzingatia muda naona tuendelee, Wizara ni hiyo hiyo swali linaulizwa na Mheshimiwa Ali Said Mbunge wa Mgogoni. Nilisahau kutangaza kwamba tunaendelea kidogo kama mnavyofahamu tulivyoanza kulikuwa na taarifa kadha za kuwasilishwa ambazo zilichukua muda uliohusu maswali.

Na. 67

**Hali ya Askari wa Mgogoni Kaskazini Pemba**

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza-

Kwa kuwa, Askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wanaoishi katika Kambi ya Makuwe Jimbo la Mgogoni, Kaskazini Pemba, wanaishi katika mazingira magumu sana ambapo nyumba zao nyingi za kuishi zimebomoka na zilizobaki zimechaa sana; na kwa kuwa, hata barabara iendayo kambini hapo ni mbaya sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwajengea Askari hao nyumba za kuishi kambini hapo?

(b) Je, ni lini barabara iendayo Kambini hapo itafanyiwa ukarabati ili kupunguza uharibifu wa mara kwa mara wa magari ya Wanajeshi hao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyoko Makuwe katika Jimbo la Mgogoni, Kaskazini Pemba ni Kiteule *(Detach)* cha Kikosi cha 14 cha Jeshi la Wananchi la Tanzania. Kikosi Mama cha Kiteule hicho kipo eneo la Wawi. Askari hupelekwa kwenye Kiteule bila familia zao na hukaa huko kwa kipindi cha kati ya mwezi mmoja hadi miezi sita. Makazi ya kudumu ya Askari wa Kiteule cha Makuwe yapo katika kikosi mama Wawi.

Wizara ya Ulinzi hivi sasa inajenga nyumba 100 za kuishi askari kwa gharama ya Tshs.2.5 bilioni. Nyumba hizo zinajengwa Wawi na zinalenga katika kuwapatia Askari na Maafisa makazi bora. Aidha, Wizara kwa kutumia fedha za Bajeti kila mwaka pia inaendelea na Mpango wake wa kuzifanyia ukarabati nyumba za Askari na maafisa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa haraka wa kuwajengea askari na maafisa nyumba bora za kuishi unaendelea katika kikosi mama kilichopo Wawi na hivi sasa nusu ya nyumba hizo ujenzi wake unakaribia kukamilika. Aidha, nyumba zilizopo Makuwe kama mpango wetu unavyoelezea pia zitafanyiwa ukarabati hali ya Bajeti itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara inayoelekea katika Kiteule hicho cha Makuwe ambayo pia inatumiwa na wananchi wa vijiji vya karibu, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wananchi katika kuiomba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili waone umuhimu wa barabara hii na kwa kutegemea hali ya uchumi waweze kuiweka katika utaratibu na kurekebisha hali hiyo.

**SPIKA:** Nimeshawishika tu nitamke kwamba nishukuru sana Serikali kwa kuonyesha kutobagua majimbo kwa maana ya kwamba inatumia shilingi bilioni 2,500,000,000 katika Jimbo la Wawi ambalo ni la kiongozi wa Upinzani - Bungeni. *(Makofi)*

Na. 68

**Uhaba wa Vyuo vya Kilimo**

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya kwanza chini ya Hayati Mwalimu J. K. Nyerere aliwafundisha Mabwana Shamba ambao walisambazwa katika kila kijiji nchini ili kuhimiza kilimo; na kwa kuwa, hivi sasa mabwana shamba hao hawapo katika maeneo mengi; na kwa kuwa, baadhi ya vyuo vilivyotoa elimu ya kilimo na mifugo kwa sasa havipo tena, na vile vilivyopo ni pamoja na Ukiriguru-Mwanza, Ilonga-Morogoro, Naliendele-Mtwara, Tengeru-Arusha na Mlingano Tanga ambavyo havitoshelezi:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kurejesha Vyuo vya Kilimo katika Wilaya na Kanda kuliko kutegemea mafunzo ya taaluma hiyo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)* kwa kiasi kikubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali iliwahi kufunga vyuo viwili tu vya kilimo ambavyo ni chuo cha kilimo Maruku, Mkoa wa Kagera na Mubondo Mkoani Kigoma. Kufungwa kwa vyuo hivi kulitokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali. Vyuo vilivyobaki alivyotaja Mheshimiwa Mbunge vya Ukiriguru –Mwanza, Ilonga-Morogoro, Naliendele-Mtwara, Tengeru-Arusha na Mlingano-Tanga, vinaendelea kupokea wanafunzi na kuendelea kutoa mafunzo ya kilimo kwa wataalam na wakulima.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka wa fedha 2006/2007 vyuo hivyo vinao wanafunzi kama ifuatavyo; Ukiriguru (120), Ilonga (187) Naliendele-Mtwara (80) Tengeru (331) na Mlingano (23); Vyuo vingine ambavyo vinatoa mafunzo kama haya ni Igurusi-Mbeya (53), Uyole-Mbeya (209) na Tumbi-Tabora (89). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizi ni dhahiri Serikali inaona umuhimu wa kuendelea kutoa mafunzo ya kilimo kwa kutumia vyuo hivyo pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ili kupata wataalam wanaohitajika kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Aidha, Wizara yangu sasa inaandaa Mpango wa Huduma za Ugani nchini. Mpango huo unalenga kusomesha na kuajiri Maafisa Ugani na kuwapa vitendea kazi kama vile usafiri na nyumba katika sehemu zao za kazi. Hivi sasa kuna maafisa ugani 3379 tu ikilinganishwa na jumla ya Maafisa Ugani 15000 wanaotakiwa. Kufuatia hali hiyo ni dhahiri kwamba tunahitaji kuchukua hatua za makusudi kufundisha maafisa ugani kwa kuvitumia vyuo vilivyopo ambavyo hivi sasa havipati wanafunzi wa kukidhi mahitaji kutokana na wanafunzi wengi kushindwa kujigharamia.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nilikuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania na kilimo ndio kinategemewa kwa asilimia kubwa katika mikoa mbalimbali hapa nchi Tanzania na utafiti unaonyesha kwamba maafisa ugani, mabwana shamba wengi sasa hivi hawafiki katika yale maeneo ya uzalishaji yenyewe, kule mashambani kwa ajili ya kwenda kutoa elimu ambayo wameisomea kwa wananchi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kutoa tamko kwa wale mabwana shamba ambao ndio maafisa ugani, maafisa kilimo tunaoambiwa ambao wanakaa sana ofisini na kushindwa kwenda huko mashambani kwenda kutoa elimu ipasavyo?

Swali la pili, kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuna upungufu wa asilimia 70 ya maafisa kilimo nchini kwetu. kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameonyesha na hii inatokana na wanafunzi wengi kushindwa kulipa gharama, yaani ada ya mafunzo katika hivi vyuo vya kilimo tulivyonavyo.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa ipo haja ya Serikali kuwafundisha wanafunzi hawa bure halafu waje wawakate baadaye katika mishahara yao watakapokuwa wanatumikia nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba hatukubali wala hatupendi mabwana shamba na mabibi shamba wakae maofisini, tunaendelea kuwahamasisha na tunawataka watoke maofisini waende mashambani kuwafundisha wakulima. Pamoja na hayo tunaelewa pia kwamba mabwana shamba wetu huko waliko wana matatizo ya vitendea kazi, na ndio maana katika jibu la msingi tumesema tunataka kupeleka mapendekezo Serikalini, kuomba tuongeze idadi ya mabwana shamba watakaofundishwa na tuwape vitendea kazi kusudi waweze kufanya kazi yao kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema pia kwamba mabwana shamba wetu hivi sasa hali zao ni mbaya ukiangalia pamoja na lawama tunazowapa lakini pia yako matatizo ambayo lazima tuyarekebishe, wao kule vijijini mabwana shamba wenye nyumba ni 156 tu, ukilinganisha na idadi hii ya mabwana sahmba ambayo tunasema tunahitaji. Kwa hiyo, tunalo jukumu la kuwapa vitendea kazi pamoja na kuwataka watoke maofisini waende mashambani.

Mheshimiwa Spika, swali la pili pia linafanana na hilo kwamba katika jibu langu la msingi nimesema Serikali na Wizara yangu sasa inapeleka mapendekezo ili tuweze kuwafundisha mabwana shamba hawa ikiwezekana kwa gharama za Serikali. Kwa sababu wengi wanashindwa kutokana na kuweza kujigharamia maana hivi sasa kuna mtindo ya kwamba baadhi ya mabwana shamba lazima wajigharamie na ukifiria bwana shamba kujigharamia halafu aajiriwe na Serikali tu akawe bwana shamba na *private sector* haipo ya kumwajiri basi wengi wamekuwa wanashindwa.

Kwa hiyo, ni lengo letu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kuwafundisha, kutaka kuwafundisha Mabwana shamba hawa kwa gharama za Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa makusudi tu naliacha swali la mwisho lingeweza kuulizwa lakini kwa kukuwa linagusia korosho, pamba, kahawa najua ziko nyongeza. Kwa hiyo, tutalisogeza mbele ili liulizwe siku nyingine. Muda wa maswali umekwisha, wageni ningependa kwanza tutambue uwepo wa mzee wetu, Sir George Kahama, ambaye amekaa pale kwenye S*peakers Gallery,* tunaendelea kuuthamini mchango wa Mzee wetu, huyu tangu akiwa Waziri kwenye *Cabinet* ya kwanza ya uhuru mwaka 1961 hadi sasa mambo mengi sana amefanya katika ushirika, viwanda, biashara, utalii na tu kuwa kiongozi mwadilifu katika maisha yake na anaendelea kutoa ushauri kwetu, ahsante sana Mzee George tunakutakia maisha marefu.

Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi anao wageni wake, hawa ni wageni kutoka jimbo hilo la Masasi, ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Uuguzi, *Ndanda Hospital,* kadri nitakavyowataja wageni naomba msimame, yupo William Richard, Evarestus Makota, Guido Mtila, Bonifance Mrope, hapa haisemi wanahusiana vipi labda jina tu, Mathias Mnonje na Abdul Chilala, karibuni sana na poleni kwa safari ndefu kutoka Ndanda.

Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mbunge wa Tarime ameniomba niwatambulishe wageni wake ambao ni Mheshimiwa huyu anamwita ni Mheshimiwa sijui ni Mheshimiwa kweli Augostino Neto. Sasa ni kiongozi wa Upinzani Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, nadhani ni diwani kwa hiyo ni Mheshimiwa yule pale karibu sana Mheshimiwa, na mwingine ni Bwana Koroman mfanyabiashara ambaye ni shabiki wa Mheshimiwa Wangwe, karibu sana. *(Makofi)*

Kamati, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati yake hiyo ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kuanzia saa tano asubuhi katika ukumbi 428 gorofa ya nne, jengo la utawala.

Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, ameniomba nitangaze kuwa anaitisha kikao cha Kamati hiyo ya Mambo ya Nje, saa saba mchana leo chumba Na. 219. Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Sophia Simba, ameniomba nitangaze kwamba leo katika ukumbi wa Pius Msekwa, saa saba mchana wajumbe wote wa *Tanzania Women Parliamentary Group* na Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, watakutana kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge kuna funguo hizi, nadhani ni za kabati au magari ya siku hizi inawezekana huu mmoja ni wa gari sijui. Lakini kwa vyovyote vile umesahauliwa na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ni kwenye *chamber* hapa, ataukuta kwa Katibu wa Meza. Waheshimwia Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 126 ninaouwezo wa kuchomekeza jambo ambalo pengine halikupangiwa utaratibu, na jambo hili nalifanya

kwa sababu mwenzetu Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Benard Membe, ni kwa nadra kulingana na kazi yake hii mpya ataonekana hapa. Sasa leo nimemwona na nikaona ni vizuri asije pengine anasafiri leo asubuhi, basi nimpe nafasi aje kwenye *Ministrial rostram* aweze kutusalimia, karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

**MHE. BENARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, kwanza nimshukuru tu tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani na heshima aliyonipa ya kujaribu kuisemea nchi yetu kule duniani. Ni kazi kubwa ambayo inahitaji ushauri, ushirikiano wenu, ni kazi ambayo haiwezi kufanywa na mtu peke yake. Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wale wote wananchi ambao walinipa pongezi, si rahisi kwangu kumjibu kila mtu, labda nichukue ukumbi huu kuwashukuruni kwa pongezi zote, Watanzania mlizonipatia kwa imani yenu. (*Makofi*)

Napenda pia nishukuru jimbo langu la Mtama sikupata nafasi ya kuwaona wote, lakini kama wananisikia sasa hivi, ninawapenda wazidi kuniombea tufanye shughuli hizi kwa pamoja ili wanichague tena mwaka 2010. Lakini ili niweze kufanya kazi vizuri napenda pia nimshukuru mke wangu, Dorcaus Membe, yuko Dar es Salaam pale, aendelee kunipikia ugali ili niweze kulitumikia taifa langu vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuruni sana na Wabunge nawashukuru sana tuzidi kuombeana tuifanye kwa pamoja kazi ngumu hii, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ndugu yetu Mheshimiwa Benard Membe, niseme tu kwamba na sisi Wabunge wenzio tunakukumbuka katika sala zetu katika dua kwa sababu huu ni wajibu mzito sana kwa nchi yetu. Nimeona umetaja ugali nadhani tatizo ni kwamba huko unakokwenda huwezi kupata ugali. Kwa hiyo inabidi usisitize ugali.

Waheshimiwa Wabunge ninazo shuhguli mbalimbali za kufanya ofisini. Kwa hiyo, nimemwomba Mwenyekiti Job Ndugai aweze kushika kiti kwa sasa ili kuniruhusu kuangalia hayo mengine yaliyoko ofisini, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI – MHE. JOBYUSTINO NDUGAI:** Naomba kutangazia Kamati ya Maliasili na Mazingira kwamba tutakutana saa saba kamili chumba Namba 133 kwa kazi maalum.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari wa mwaka 2006 (*The Deep Sea Fishing Authority (Amendment) Bill, 2006)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maelezo yangu, naomba nikutakie wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, heri ya mwaka mpya na mafanikio katika mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linajumuisha nchi kavu, maji ya maziwa na ukanda wa bahari wenye upana wa maili za bahari 200 ukipimwa kuanzia Mashariki mwa Visiwa vya Pemba, Ugunja na Mafia na eneo la Pwani ya mikoa ya Lindi na Mtwara.

Eneo la bahari limegawanyika katika sehemu kuu tatu, kwanza ni bahari ya ndani *or internal waters* ambalo hutumiwa zaidi na wavuvi wadogo wadogo. Eneo la pili ni bahari ya kitaifa, au *teritorials sea* ambayo upana wake ni maili 12 na eneo hili hutumiwa na wavuvi wenye vyombo vinavyomilikiwa na Tanzania na vyenye uzito usiozidi tani 150, vyombo vya wageni haviruhusiwi kuvua kwenye ukanda huu. Eneo la tatu ni bahari kuu au *Deep Sea* na ni eneo ambalo upana wake ni maili 188, vyombo vikubwa huvua kwenye eneo hili ikiwa ni pamoja na meli zinazomilikiwa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uvuvi katika bahari ya ndani na kwenye bahari ya kitaifa zinasimamiwa na mamlaka mbili tofauti, kwa upande wa Tanzania Bara ipo sheria ya uvuvi ya mwaka 2003 na kwa upande wa Tanzania Zanzibar iko sheria ya uvuvi ya mwaka 1988. Hadi sasa hakuna mamlaka ya pamoja inayosimamia shughuli za uvuvi kwenye eneo la Bahari Kuu na leseni za kuvua katika eneo hilo hutolewa na pande zote mbili za Muungano, yaani Tanzania Bara wanatoa leseni na Tanzania Zanzibar pia wanatoa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika eneo la Bahari Kuu ipo rasilimali kubwa ya uvuvi ambayo hatuitumii ipasavyo, baada ya Tanzania mwaka 1985 kuridhia mkataba wa umoja wa mataifa kuhusu sheria ya bahari ya mwaka 1982, nchi yetu ilichukua hatua ya kutangaza ukanda wake wa uchumi kupitia sheria ya *territorial Sea and execlusive economic zone* ya mwaka 1989 na iliwajibika kutunga sheria ya kusimamia na kudhibiti uvuvi kwenye eneo hilo. Hata hivyo uvuvi sio miongoni mwa masuala ya muungano, hivyo mwaka 1987 Wizara zinazosimamia masuala ya uvuvi katika Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zilikubaliana mambo mawili ya kimsingi:-

La kwanza ni kuanzisha chombo cha pamoja kitakachojulikana kama *The Deep Sea Fishing Authority* yaani Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika eneo la bahari kuu.

Pili kuwepo na utaratibu wa pamoja wa kila upande wa muungano kutoa leseni kwa vyombo vya uvuvi kuvua katika eneo hilo kwa kutumia sheria zilizopo hadi hapo mamlaka itakapokuwa imeanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia makubaliana hayo, wenye meli zinazovua katika eneo la bahari kuu wameendelea kuchukua leseni kutoka Tanzania Zanzibar, au Tanzania Bara hali ambayo imesababisha ugumu wa kuratibu uvuvi katika eneo la bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu wa Sheria ya Mamlaka ya kusimamia uvuvi kwenye eneo la bahari kuu ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania tarehe 11 Februari, 1998. Hata hivyo hadi sasa sheria hiyo haikuweza kutekelezwa kwa Sababu ya mambo yafuatayo:-

Kwanza katika muundo wa mamlaka, hapakuwa na uwiano mzuri katika uwakilishi kwenye Kamati na vyombo vya uongozi.

Pili Sheria haikumtambua Waziri anayesimamia uvuvi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kama mwenye mamlaka na sheria hiyo.

Tatu haikuweka bayana mfumo wa mgawanyo wa mapato, yatakayotokana na shughuli za uvuzi kwenye eneo la Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo, kumefanyika mashauriano ya ndani katika ngazi za Wataalam, Wanasheria, Wachumi, yamefanyika mashauriano baina ya Wizara zetu katika ngazi ya Makatibu Wakuu katika ngazi za Mawaziri na mapendekezo yaliyotokana na mashauriano hayo yalipelekwa kwenye Vikao kati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ningeeleza kwa kifupi mapungufu yaliyopo kwenye Sheria ambayo ipo sasa.

Kwanza, Sheria hiyo inamtambua Waziri anayehusika na masuala ya uvuvi katika Serikali ya Muungano na haimtambui Waziri anayehusika na uvuvi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Pili, uwakilishi wa pande zote mbili haukuwa wa kuridhisha kwenye Kamati za Uendeshaji na Kamati za Kitaalam za ushauri.

Tatu, Sheria haikuonyesha kuwa mapato ya Mamlaka yatagawanywa namna gani kati ya Serikali zetu mbili.

Nne, kutoitambua Taasisi muhimu ya *KMKM* kama mmoja ya wasimamizi wa sheria hiyo.

Aidha, Sheria hiyo haikutaja Mahakama Kuu ya Zanzibar kama mmoja ya Taasisi ya kusimamia Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mashauriano na wadau mbalimbali kutoka pande zote mbili za Muungano pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hatimaye marekebisho yafuatayo yamependekezwa:-

(a) Kuongeza *KMKM* kwenye orodha ya wasimamizi wa Sheria;

(b) Kutambua Mahakama Kuu za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika sheria hii;

(c) Kuwatambua na kuwapa majukumu Mawaziri wa pande zote mbili za Muungano wanaohusika na masuala ya uvuvi;

(d) Kuwa na uwakilishi wa kuridhisha kwenye Kamati za Utendaji na Kamati ya Ushauri kwa kuboresha Muundo wa Kamati hizo, sifa na majukumu ya wahusika; na

(e) Kurekebisha mgawanyo wa mapato kama ifuatavyo:-

(i) Asilimia 50 ya mapato ya Taasisi hiyo itatengwa kwa ajili ya shughuli za Mamlaka;

(ii) Asilimia 30 ya mapato ya Mamlaka itatengwa kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(iii) Asilimia 20 itatengwa kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu kutaleta faida zifuatazo:-

(i) Malipo ya ada za leseni yataongezeka na kufikia takriban *dollar* milioni 20 kwa mwaka, ifikapo mwaka 2011 ikilinganishwa na kiwango cha sasa cha Dola za Kimarekani milioni 2.84 kwa mwaka;

(ii) Leseni, vyombo vya uvuvi, zana za uvuvi, uharibifu wa mazingira na rasilimali za uvuvi zitadhibitiwa na kusimamiwa ipasavyo;

(iii) Tutaweza kujiunga na Mashirika ya Kimataifa kama vile *the Indian Ocean II* na *Commission* ambayo yanasaidia kutupatia masoko, kupata takwimu sahihi za meli na kuwezesha kuwa na nguvu ya pamoja katika kushughulikia meli korofi katika eneo la Bahari Kuu;

(iv) Tutaweza kutekeleza kikamilifu Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia; na

(v) Tutaweza kuingia Mikataba ya Uvuvi kwa pamoja na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Bunge lako Tukufu litapitisha mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika eneo la Bahari Kuu, Mamlaka itaanzishwa na kuendeshwa kwa kuchangiwa na fedha iliyotengwa katika Mradi wa *Marine and Coastal Environmental Management Project* kuanzia mwaka 2007 hadi 2011.

Aidha, jumla ya Dola za Kimarekani milioni 16,150,000 zimetengwa kuchangia gharama za uendeshaji, ujenzi wa Makao Makuu, ujenzi wa Ofisi za Idara za Uvuvi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, vifaa pamoja na meli ya doria katika Bahari Kuu, mafunzo na ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zitatolewa kwa awamu katika kipindi cha miaka mitano. Baada ya Mamlaka kujiimarisha, Mamlaka hiyo inatarajiwa kujiendesha yenyewe kutokana na mapato yatokanayo na ada za uvuvi katika Bahari Kuu pamoja na mapato yaliyoainishwa katika Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitishwa kwa marekebisho hayo na kuanzia kutumika kwa sheria ya Kuanzishwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu, itakuwa ni hatua makubwa ya mafanikio kwa wananchi na Taifa kwa ujumla kuleta usimamizi endelevu wa rasilimali ya Bahari Kuu, ongezeko la pato la Taifa na ajira kwa wananchi na hatimaye kupunguza umaskini, jambo ambalo litawezesha maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kilichoko mbele yetu ni Muswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu ya Mwaka 2006. Kwa nafasi hii basi, namwita Mwakilishi wa Kamati ya Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Raynald Mrope kwa ajili ya kutoa maoni ya Kamati.

**MHE. RAYNALD A. MROPE (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu wa Mwaka 2007. *(The Deep Sea Fishing Authority (Amendment) Act, 2007.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2004 niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu Muswada wa kuanzisha Mamlaka ya kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu wa mwaka 2007 unaokusudia kuifanyia marekebisho Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu ya Mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Wabunge, familia, ndugu na wapigakura wote wa Tunduru kwa kifo cha Mbunge mwenzetu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu aliyekuwa akishughulikia

masuala ya Bunge, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, kilichosababishwa na ajali ya ndege. Marehemu atakumbukwa daima kwa uchapakazi na uadilifu wake, kwa moyo wake wa kujituma na kwa uongozi wake uliokuwa wa mfano. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati kumpongeza Mheshimiwa Dk. Asha Rose Migiro, Mbunge kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu na Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee na kwa kuwa Mheshimiwa Bernard Membe yupo humu ndani pamoja nasi, Kamati pia inampongeza sana kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Wakati huo huo tunawapongeza pia Mheshimiwa Batilda Burian kwa kuchukua wadhifa huo wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa William Ngeleja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilikaa tarehe 03 Februari, 2007 kujadili kwa kina Muswada huu kwa lengo la kuuboresha. Kamati iliwaalika Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kutoka Majimbo ya Tanzania Bara na Visiwani. Majadiliano hayo yalisaidia sana kuibua mawazo mapya, maoni na hoja nzuri za kuendeleza Muswada huu. Maoni na Ushauri wa Kamati ni matokeo ya mchakato huo wa kubadilishana mawazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba tarehe 11 Februari, 1998 Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hadi sasa Sheria hiyo ilikuwa haijaanza kufanya kazi kutokana na upande mmoja wa Muungano kutoridhishwa na mambo mbalimbali yaliyohusu Muundo wa Mamlaka, uwakilishi kwenye Kamati za Mamlaka hiyo, usimamizi wa uvuvi, mgawanyo wa mapato yatakayotokana na shughuli za Uvuvi kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za awali, Serikali ilionyesha dhamira yake ya kuanza kutumika kwa Sheria hiyo, lakini kwa kipindi hicho tayari Sheria hiyo ilishaanza kupata utata kuhusu utekelezaji wake.

Hadi sasa hakuna mamlaka yoyote inayosimamia shughuli za uvuvi kwenye eneo Kuu la Bahari na leseni za kuvua katika eneo hili zinazotolewa na pande zote mbili, yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano na makubaliano mbalimbali yamefanyika katika ngazi mbalimbali kutoka pande zote mbili za Muungano, hatimaye Muswada huu kuwasilishwa tena leo Bungeni baada ya miaka takribani tisa (9). Kamati imeridhika kuwa Muswada huu ukipitishwa utaleta mapinduzi makubwa katika Shughuli za Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inakubaliana na Serikali kwamba kuanzishwa kwa mamlaka ya kusimamia uvuvi kwenye Bahari Kuu kutaleta faida zifuatazo:-

- Kuongezeka kwa mapato hasa fedha za kigeni;

- Shughuli za uvuvi zitadhibitiwa kikamilifu;

- Kuingia Mikataba ya Uvuvi ya Kitaifa na Kimataifa;

- Nchi itafaidika kikamilifu na Mashirika ya Kikanda yanayohusu uvuvi wa Bahari Kuu; na

- Kuanza kwa tafiti mbalimbali za Kisayansi.

Hivyo basi, Muswada umeifanyia marekebisho Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu ya Mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika Ibara ya 5 ya Sheria inayohusu Wajumbe wa Kamati Kuu ya Utendaji, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Marekebisho ya Muswada kwa kuongeza Wajumbe katika Kamati hiyo, yaani Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa Mamlaka hawa wanapendekezwa kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo. Hata hivyo, Kamati bado inaona kuwa upo umuhimu wa kumwongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kupata mwakilishi, hasa katika kuwasiliana na vyombo mbalimbali vya uvuvi vya nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 8(d) ambayo inataja Wajumbe wawili (2) wa Kamati ya Ushauri watakaoteuliwa na Waziri baada ya mashauriano na Waziri mwenzake anayehusika na uvuvi. Katika Ibara hii inataja kwamba Wajumbe hao ambao watakuwa ni Wachumi wa Mambo ya Bahari *(Marine Economist)* mmoja kutoka katika Tume ya Mipango ya Serikali ya Muungano na mmoja kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni maoni ya Kamati kwamba Muswada usitaje kwamba mchumi wa Mambo ya Bahari lazima atoke katika Tume ya Mipango, bali mapendekezo yaseme tu kwamba atoke katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilijadili kwa kina kuhusu mgawanyo wa mapato yatakayopatikana katika Mamlaka hii. Mgawanyo kama ulivyopendekezwa katika Muswada ni kwamba Mamlaka itapata asilimia 50, Serikali ya Jamhuri ya Muungano asilimia 30 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itapata asilimia 20. Aidha, mjadala ulijielekeza zaidi katika kujua vigezo vilivyotumika katika kuweka viwango hivyo. Kamati ilikubaliana na maelezo yaliyotolewa na Serikali ya kwamba mgao ulizingatia mapato ya uandikishaji wa leseni za Meli na mapato yanayopatikana kutokana na meli zinazovua katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililojadiliwa ni kuhusu Makao Makuu ya Mamlaka, ambapo katika mapendekezo ya Muswada huu haukutaja Makao Makuu yawe wapi? Kamati ilikubaliana kwamba Mamlaka zinazohusika kuamua Makao Makuu yawe wapi, zitumie vigezo vinavyostahili katika kuamua ni wapi yatakuwepo Makao Makuu ya Mamlaka. Serikali ijiandae kikamilifu kwa kujenga Makao Makuu hayo na

kuweka nyenzo na vitendea kazi muhimu ili kuiwezesha Mamlaka kufanya kazi zake kwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililojadiliwa ni kuhusu Waziri kutengeneza Kanuni katika kutekeleza Sheria hii. Kamati ilibaini kwamba kuna Sheria nyingi hapa nchini ambazo zimepitishwa kwa miaka mingi, lakini Mawaziri wamechelewa kutayarisha Kanuni zake. Katika Muswada huu, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuchukua uzito wa pekee ili kuhakikisha utengenezaji wa Kanuni unakamilika mara moja baada ya Muswada huu kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Maoni na Ushauri wa Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004 kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Job Y. Ndugai - Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Riziki O. Juma Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Emanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Lucy Mayenga na Mheshimiwa Mariam Mfaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdukarim E. Shah, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Mohamed R. Soud, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Juma S. N'hunga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na mimi Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Damian Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Makatibu wa Kamati Ndugu Lawrence Makigi na Michael Kadebe kwa kuihudumia Kamati vizuri sana wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Jumanne A. Maghembe, Naibu Waziri - Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Katibu Mkuu wa Wizara, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kushiriki kikamilifu katika kuandaa na kuboresha Muswada huu ikiwa ni pamoja na ushirikiano waliouonyesha kwa Kamati wakati wote wa kuujadili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kutoa Maoni kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu wa mwaka 2007 *The Deep Sea Fishing Authority (Amendment) Act, 2007.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, kwanza natoa rambirambi zangu kwa ndugu, jamaa wa Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, pamoja na Marehemu wote waliofariki katika ajali ya ndege iliyotokea Mkoani Mbeya. Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu na awalinde jamaa na ndugu wa Marehemu katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu Tanzania na kwa akinamama wote wa Tanzania, amezidi kutujengea ujasiri, kwamba hakuna lisilowezekana, kinachotakiwa ni juhudi. Aidha, nawapongeza Waheshimwa wote waliopata nafasi za Uwaziri na Unaibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe shukrani kwa kupata fursa hii kutoa maoni yetu kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu ya mwaka 2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(c) na 70(2) Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa marekebisho ya sheria hii ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Serikali za pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa ukitilia maanani kuwa Tanzania imekuwa ikipoteza mabilioni ya fedha kutokana na uvuvi haramu unaoendeshwa na vyombo vya nje katika eneo letu la bahari kuu.

Mfano ulio hai, ni pale nchi yetu ilipopata msaada wa kikosi cha Askari wa Majini kutoka Afrika Kusini ambapo walifanikiwa kuzikamata zaidi ya meli 60 zilizokuwa zikivua kinyume cha sheria. Meli hizo ambazo zenyewe ni viwanda, zina uwezo wa kuvuna sio chini ya tani 500 kwa kipindi cha siku zisozidi 60. Ukichukua kwa wastani wa tani 300 tu kwa kila meli (300x60=18000Mt.) kama kila kilo moja tunapata mrahaba wa Dola moja tu, maana yake ni Dolla Milioni kumi na nane ($18,000,000).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi, tunalipwa, kwa hizo meli zinazolipa leseni tu $18,000 kwa mwaka mzima. Serikali yetu inasifika kwa ukarimu kwa gharama ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa marekebisho haya yanayofanywa katika sheria yenyewe ni ya muhimu, lakini Kambi ya Upinzani bado inadhani sheria nzima bado haijawekwa sawa kwa manufaa ya Watanzania wa pande zote mbili ili kuweza kuvua katika bahari kuu. Hii inatokana na ukweli kuwa uvuvi katika bahari kuu unahitaji mpango mkakati wa kuwawezesha wazawa kumiliki au kuwa na ubia katika vyombo vikubwa vinavyoweza kuvua katika bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuongeza ufanisi, lakini inatakiwa ufanisi huo uwaguse moja kwa moja wananchi wa nchi hii ili waweze kulipa kodi kutokana na mazingira mazuri yanayowekwa na Serikali. Kambi ya Upinzani inadhani *Technical*

*Advisory Commitee* pamoja na shughuli itakazozifanya suala la kuifufua *TAFICO* lipewe kipaumbele, kwani tatizo kubwa la kushindwa kutumia raslimali ya bahari kuu ni uchanga wa vyombo wanavyotumia wavuvi wetu.

Aidha, suala la kuwa na vyombo vya kufanya doria katika eneo la bahari kuu ni muhimu sana vinginevyo sheria hii haitakuwa na manufaa yoyote kwa nchi, kwani vyombo vya nje hufanya shughuli zake huko na kuondoka bila ya kuonekana, havihitaji Bandari ya Samaki, vinahuduma zote zinazopatikana katika Bandari za Samaki na hapo fedha nyingi hushindwa kuingia Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Serikali kukosa mapato mengi sana yatokanayo na uvuvi katika bahari kuu, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanzisha mamlaka itakayoshughulikia haraka uanzishwaji wa Bandari za Samaki katika nchi yetu, kwani kama raslimali ya baharini na maji baridi zingetumika vizuri, umasikini kwa Watanzania ungekuwa ni ndoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha tisa cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 10(b) cha sheria kinatoa mwongozo wa jinsi mapato yatakavyogawanywa kati ya sehemu mbili za Muungano. Kwa kuwa hivi sasa tayari kuna Tume ya Kusimamia mapato na matumizi ya mambo ya Muungano na kwa kuwa Tume hii kazi yake moja ilikuwa ni kuweka *formula* ya mgawano wa mapato: Je, sheria hii ikipitishwa haitagongana na *formula* iliyopendekezwa na Tume ya pamoja ya Fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo ni vyema tukaangalia vianzio vya mapato vya pande mbili za Muungano. Vianzio vikubwa vya mapato kwa upande wa Zanzibar ni biashara ambayo imeathirika kutokana na tatizo la mfumo na gati, karafuu ambazo bei na uuzaji wake haukui kwani bado umo katika mfumo wa ukiritimba (inapangwa na kununuliwa na Serikali), Utalii, ambapo mapato yake wanayafaidi zaidi wawekezaji kwani watalii huwalipa huko huko wanakotoka, sisi huambulia uchafuzi wa mazingira na mila na desturi zetu tu.

Mheshimiwa Spika, uvuvi ambao kama nilivyotangulia kusema kuwa tunalipwa leseni tu kwenye mrahaba tunatoa sadaka, hivyo hatupati kitu, kutokana na hali hiyo na kwa kuwa Bara kuna vyanzio vingi vya mapato tunashauri kuwa mgawanyo wa mapato uwe nusu kwa nusu kwa kila upande wa Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 10(c ) cha Muswada kinachokifuta, kifungu cha 11(5) cha sheria kimemtaja Waziri wa Tanzania kuwa ndiye apewe nakala ya bajeti mwezi mmoja kabla ya mwaka mpya wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna mapungufu, kwani bajeti hiyo inatakiwa pia iwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi kwani na Serikali ya Mapinduzi wanatakiwa wachangie katika uendeshaji wa mamlaka. Hivyo neno 'Waziri' liendelee kupewa tafsiri ya Mawaziri kama vipengele vingine vinavyosomeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 14(3) kinachosema kuwa fedha zote zitakazotokana na utaifishwaji wa vyombo vinavyokwenda kinyume na sheria hii pamoja

na faini kutokana na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa taratibu zinazoiongoza sheria kupelekwa Hazina, Kambi ya Upinzani inaona hili bado litaendeleza ukiritimba usiokuwa na maana, kwani kama ilivyopendekezwa kuwepo na mgawanyo baina ya pande mbili zinazohusika. Kambi inashauri mgawanyo katika hili uwe ni asilimia 25 kwa 25, badala ya asilimia 30 kwa 20 kama Muswada unavyopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria ndiyo inafanyiwa marekebisho, katika tafsiri iliyotolewa katika sheria, hakuna sehemu inayoongelea maana ya maneno *'Controller and Auditor General.'* Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni busara kwa kulitolea tafsiri yake, vinginevyo italeta utata kwani hii inatakiwa kuwa sheria ya sehemu mbili za Muungano hasa tukizingatia kuwa kuna *Controller and Auditor General* wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, nakubaliana na mabadiliko haya pamoja na mapendekezo tuliyoyatoa. Tunamwomba Waziri atakapofanya majumuisho alielezee Bunge lako Tukufu, ni kwa nini Mkataba wetu na *EU* juu ya kusimamia uvuvi wa bahari kuu na kuruhusu vyombo vya *EU*-40 kuvua umekwamia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wote kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru Waziri kwa kuwasilisha mabadiliko haya ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mambo matatu machache tu. La kwanza ni utumiaji wa rasilimali zetu Tanzania. Bahari au ukanda wa bahari unachukua Mikoa kama ya Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Tanga na Mikoa yote ya Zanzibar. Ukichukua *population* ya watu hao ni kubwa sana. Kama ukanda huu wa bahari ungetumika vizuri tokea tulipopata uhuru, leo tusingezungumza hata habari ya madini. Jambo ambalo linasikitisha ni kwamba bahari au mazao yaliyoko baharini ni tofauti kabisa na bidhaa au rasilimali zilizopo katika nchi kavu. Baharini kazi kubwa ni kutafuta vyombo na kwenda kuvua, yaani ni kuvuna. Lakini tumeshindwa kuitumia rasilimali hiyo vizuri na wageni wameendelea kuitumia rasilimali hiyo kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia meli zinazovua baharini sasa hivi za kigeni hazipungui 100 na meli hizi zina wastani wa tani nyingine 500 na kuendelea. Kwa sababu ya mavuno ya samaki, huwezi ukachagua samaki, pamoja na kwamba wanakuja kuvua *ton fish* lakini wanapotupa nyavu zinazokwenda kama kilomita tatu wanakokoa kila kitu kilichoko chini na wanachukua kile wanachohitaji, wasichokihitaji wanakitupa. Kwa hiyo uharibifu wa mazingira na upungufu wa rasilimali unakuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kipindi fulani nchi kama *Mozambique* ambao walikuwa na meli nyingi sana za Kirusi kuvua *prawns* waliadimika *prawns* kabisa *Mozambique*, kwa muda mrefu sana.

Sasa nasema, hili ni tatizo moja ambalo sisi kama Tanzania bado hatujasimama kidete katika kuzitazama hili, rasilimali zetu na vipi zitatupa faida na wananchi wetu. Matokeo yake hivi sasa wavuvi wetu wadogo wadogo hawapati tena samaki katika

*shallow water* kama walivyokuwa wanapata kutokana na vyombo hivi vikubwa vinavyokuja kuvua kinyume cha utaratibu, wanachukua samaki hata katika maeneo ambayo wavuvi wetu wa changu wadogo wadogo wangeweza kuwapata. Nasema na hii ni athari kubwa tunayoipata Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni ufuatao: Kwa kuwa eneo la uvuvi wa bahari ni kubwa na kwa kuwa hatuna rasilimali za kutosha za kulinda uvuvi haramu, jambo la msingi kabisa ni kuzitumia bandari zetu zilizopo hivi sasa kuzilazimasha meli hizi zinazovua angalau zifunge ghati kwenye bandari zetu katika kusafirisha mazao yao. Hizi *fish pots* ambazo ziko katika nchi nyingi ndizo zinazosaidia angalau kupata kiwango fulani cha mapato.

Kama tulivyosema katika taarifa ya Kambi ya Upinzani, kama tungeweza kutoa dola moja tu kwa kilo ya samaki wanaovuliwa kama mrahaba, basi nchi yetu ingekuwa inapata mapato kuliko hata tunayopata kutokana na dhahabu na mazao mengine. Nchi nyingi zinafanya hivyo, kwa mfano Namibia, Canada na nchi nyingi sana zinatumia utaratibu huo. Sisi tunazo bandari zaidi ya tano, hakuna hata bandari moja inayotumika ukiacha uvuvi wa *prawns* na ushahidi huu upo.

Mheshimiwa Spika, wale wanaovua kamba ndiyo meli zao zinakuja zinafunga ghati wanasafirisha kamba na kwa maana hiyo tunapata *levy* katika usafirishaji wa kamba, lakini kwenye *deep sea* hatupati chochote.

Sasa hii nasema ni kasoro kubwa ambayo inahitaji kuangaliwa kwa sababu ni mapato makubwa ambayo tunayakosa kutokana na uvuvi. Lakini nasema hasara nyingine tunayoipata ni kwamba hatuwezi kuwaratibu vizuri wanaovua kwa sababu wanavunja sheria wanavua kinyume cha sheria na hawafungi kwenye ghati zetu.

Kwa hiyo, mimi nafikiri hili tungeweza kuliangalia lingeweza kutusaidia kutupunguzia umaskini tulionao. Kwa mfano, kwa upande wa Zanzibar ingelikuwa hilo linafanyika, basi mapato yao yangeongezeka maradufu hasa ukiangalia kwamba sehemu kubwa ya *deep sea* ambayo wanayo ina samaki wazuri na wengi hawajavuliwa kwa muda mrefu sana. Sasa hili moja ambalo ningeomba Serikali iliangalie na ilifanyie kazi kwa haraka ili angalau tuanze kupata mapato yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la mgawano wa mapato. Nafikiri kama hotuba yetu inavyosema, kwamba Zanzibar vyanzo vyake vya mapato ni kidogo sana ukiacha karafuu na utalii kidogo halafu kuna biashara ambayo imepata matatizo na ghati yenyewe mbovu. Kwa hiyo, kuna matatizo makubwa sana. Eneo peke yake ambalo lingeweza kusaidia ni hili la uvuvi. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri, kwa sababu Bara kuna vyanzo vya mapato vingi likaangaliwa upya katika mgawanyo huu wa mapato.

Lakini vile vile la msingi zaidi, kuna hii Tume ya Pamoja ya Fedha, nayo inakuja na *formula* yake ya mgawanyo wa mapato. Sasa mimi nafikiri katika sheria kutakuwa na mgongano kwa sababu mapato yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatasimamiwa katika mfuko mmoja au Tume moja, halafu huku mnapitisha sheria ina utaratibu mwingine mbali. Mimi nafikiri kutakuwa na mgongano.

Mheshimiwa Spika, sijui kama kuna mawasiliano mazuri yamefanyika ya Serikali ya kujua kama *GFC formula* waliyoitoa ya mgawanyo wa mapato na matumizi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaoana na sheria hii inayopitishwa hivi sasa. Hili nafikiri linataka maelezo ya kina ili tujue kama hakutakuwa na mgongano hapo baadaye na tutategemea katika Bunge hili linalokuja la Bajeti pengine Serikali itatimiza Katiba kikamilifu ya kwamba mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yasimamiwe na Tume ya Pamoja ya Fedha.

Kwa hiyo, Tume hiyo italeta mapendekezo na Serikali italeta mapendekezo yao. Tunategemea haya yote yataingia katika mkondo huo wa mapato. Sasa sina hakika kama sheria hii haitogongana na *formula* itakayoletwa na Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni la Makao Makuu. Kwa kuwa Chuo cha *Marine Science* kiko Zanzibar. Nafikiri itakuwa ni wazo zuri kwa mamlaka hii kuwa na Makao Makuu Zanzibar kwa sababu tayari wana chombo kinachoweza kuwapatia taarifa sahihi. Nafikiri ni wazo zuri na itakuwa ni mara ya kwanza nafikiri kuwa na Makao Makuu ya chombo cha Muungano kuweko Zanzibar. Litakuwa ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango kidogo kwenye Muswada huu wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo machache tu ya kuchangia na hasa kwa ushauri zaidi. Ukiangalia katika Ibara ya Tano kifungu (f) ukurasa wa sita mpaka wa saba, halafu Ibara ya 7(d) hapa nilitaka; pengine *Attorney General* atatusaidia katika tafsiri ya Tanzania Bara kwenye Katiba ya Kiingereza ya mwaka 1998 imetafsiri Tanzania Bara kama *Mainland* Tanzania. Sasa ukiangalia katika vifungu hivi, vinataja Tanzania *Mainland*. Nadhani kingeangaliwa hiki ili tuendane na ile sheria kuu ambayo ni Katiba ya Kiingereza ya Mwaka 1998 japokuwa haichukuliwi kama rasmi, lakini ndiyo yenye tafsiri ya Tanzania Bara badala ya kuwa *Tanzania Mainland,* ni *Mainland Tanzania* litazamwe hilo.

Kwenye Ibara ya Tisa ukurasa wa nane mpaka wa tisa, sheria hii itakuwa na mgongano, itabidi itazamwe. Itakuwa na mgongano na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara 133 mpaka 134. Nitaomba niinukuu kidogo kwamba, katika Ibara hiyo 133 inaunda *Account* ya fedha ya pamoja ya Muungano halafu kifungu 134 kimeunda Tume ya Pamoja ya Muungano na katika Mfuko huo ni kwamba, fedha yote itachangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Sheria iliyotungwa na Bunge ni sheria sura ya 140 ya mwaka 1998. Nadhani Serikali ingetazama hii ni bahati mbaya kwamba Wapinzani ilibidi lazima watangulie kutoa maoni yao lakini nimekuwa nimejiandaa kutoa ushauri huu kwamba eneo hilo

lingetazamwa ili tusiweze kutunga sheria ambayo inakwenda kinyume na Katiba. Ikitungwa sheria, kwa kweli yale ya Katiba ndiyo ambayo yatafuatwa. Lingetazamwa hili.

Labda kwa faida tu ni kwamba, mimi ni Mwenyekiti wa Tume hiyo na kazi hiyo ya kutoa ushauri kwa mujibu wa Katiba na sheria sura namba 140 imeshafanywa toka mwezi Agosti, kwa hiyo ni shauri ya Serikali yenyewe kuangalia ushauri huo jinsi unavyoona utakavyoutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ile Ibara ya 20 ukurasa wa 20 suala la mashirikiano. Nadhani kama kuna eneo ambalo ningeweza kutusaidia kutatua matatizo mengi na kero nyingi za Muungano ni hili la kuimarisha Mawasiliano kati ya pande hizi mbili hasa mawasiliano ya Wizara na ngazi ya wataalam ingetusaidia sana kuweza kupunguza mambo ambayo kwa kweli hayahitaji kubadilisha sheria na mashauriano kuona utekelezaji wa mambo ya Muungano utakwenda vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nitoe mchango wangu huo na yaangaliwe kwa makini haya japokuwa kuna makubaliano, lakini makubaliano hayo lazima yaangalie Katiba na Sheria nyingine ambazo zipo. Nakushukuru na naunga mkono hoja pamoja na haya maangalizi ambayo nimeyatoa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wanajimbo wa Singida Kaskazini kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kulitazama suala hili la *Deep Sea Fishing* hizi maili 188 ambazo kimsingi ziko mbali sana na uwezo wa kawaida wa maboti yetu kuweza ku-*patrol*. Kilichotokea hapo nyuma ni kwamba, meli za kigeni zimekuja kama nyumbani kwao zikachukua samaki zote ambazo wangeweza kuzichukua na sana sana baadhi ya watu wa Dar es Salaam kwa kutumia rada iliyopo, wanaweza kuziona zile meli. Lakini hatujawa na uwezo wa kufanya kitu chochote kuzuia. Mashirika makubwa ambayo yamejihusisha na wizi huu ni Jumuiya ya Ulaya na nchi ya Mashariki ya mbali bila ya kuzitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni wezi wakubwa wanajiita wanademokrasia, wanajiita wanapenda haki za binadamu lakini hawa watu wa Ulaya na kama wananisikia wasikie vizuri ni wezi wakubwa. Hawana aibu kuruhusu meli zao na wanazifahamu na wanaziangalia kwenye *radar systems* hata kwenye *global position* wanaziona. Meli zinaingia katika nchi maskini zinawaibia watu maskini zinapeleka huko kwao wanaendelea kuuza kwa bei kubwa. Samaki zinazotoka Ziwa Victoria zinazopelekwa kwa halali wanasema kwamba hizo hazijafikia kiwango cha ubora. Haya yameendelea kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tathmini zilizofanywa thamani ya kipato au ya uchumi wa Kanda ya Pwani ya Tanzania ukianzia Mkoa mzima wa Tanga, Dar es Salaam hadi Mtwara na kwa Visiwa vile vya Pemba, Zanzibar na ukubwa wa bahari unaozifuata

wanasema ni Dola za Kimarekani milioni 50 kwa mwaka, ndio pato ambalo Tanzania ilitakiwa ipate sasa hivi kutokana na wavuvi tu wanaotumia *Deep Sea Fishing*. Tumeona kwamba sasa hivi nchi inapata Shilingi milioni 2.8 kwa mwaka.

Kwa hiyo, tunapoteza zaidi ya Shilling milioni 47 kama pato la Taifa. Nimeangalia matarajio ambayo Wizara inategemea ipate kutokana na hii sheria itakuwa ni Shilingi milioni 20 kwa mwaka kuanzia mwaka 2011. *Investment* ambayo nimeona Waziri anapendekeza iwekwe ni kuwekeza Shilingi milioni 116 katika kipindi cha miaka mitano. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano tutakuwa tunawekeza fedha kidogo kidogo wakati ule ule Tanzania itakuwa inaendelea kupoteza Shilingi milioni 50 kila mwaka *potentially* ambazo tungeweza kuzipata. Sasa angalizo la kwanza, ni kwa nini Serikali isiwekeza Shilingi milioni 116 kwa wakati mmoja kwa mkupuo ili tuweze kuokoa Dola milioni 50 ambazo tunazipoteza kila mwaka kutokana na kipato hiki ambacho hatukipati. Ukiendelea kuweka Shilingi 20 milioni kwa mwaka maana yake ni hii tunaendelea kupoteza kimsingi Shilingi milioni 50 kila mwaka ambazo kama nilivyosema tungeweza kuzipata kutokana na leseni ambazo hatuzipati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna tatizo la uwezo wa hiki kituo ambacho kinaandaliwa (*capacity*). Kinachotakiwa ni suala la nchi kuamua. Aidha, tunaweza kuamua kuwekeza kidogo na tukawa wanyonge ambao watu wote wanajua wakisimama wanasema Tanzania ni nchi ya wanyonge. Nchi ya wanyonge kwa sababu maamuzi yanayofanywa ni ya kinyonge. Ukiamua kuwekeza kinyonge utaendelea kuwa mnyonge mpaka wajukuu watajua nchi hii ya wanyonge, babu zetu walikuwa wanyonge. Lakini uamuzi ambao tunaweza tukaufanya ni kuwekeza kithabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, tuna uwezo wa kutumia. Hii Tume inayooanzishwa, sijaona popote ambako imeandikiwa watatua *radar system* ambayo tunayo. *Radar* iliyoko Tanzania ina uwezo wa kuona mbali sana, *capability* ya *radar* kumulika kule baharini tuna uwezo wa kuona maeneo makubwa sana. Hii *radar* inatakiwa itumike pamoja na uwezo wake kuangalia ni meli ngapi kwanza zimetoka, ziko umbali gani kufikia maili 188 za Tanzania tuzione kabla hazijafika. Tuone *direction* ya zile meli ni ngapi, *identity* yake, zimetoka nchi gani na zina *capacity* gani ya uvuvi, ni tani ngapi hizi meli zinakuja kuvua na wawasiliane na hawa watu wa meli kuwaambia karibuni, tunawaona. Nchi zote zinafanya hivyo, kabla hawajafika waambiwe tuko pamoja na ninyi tunawaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine zimetumia *unman planes* kwa sababu unapo-*deploy radar,* kinachotokea ni kwamba *radar* inakuwezesha kuona sehemu tu. *Unman Planes* sio bei kubwa. Zinaweza zikazunguka ukanda wa pwani yetu tukaweza kuona *activity* ngapi zinaingia Tanzania, watu wangapi wako mbioni kuja Tanzania na pia hizo zitasaidiwa na *fast boats*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona *function* ya Jeshi. Huwezi kulinda bahari bila kuongeza *function* ya *capability* ya Jeshi, kwa sababu hili ni suala la usalama wa nchi. Hili ni zaidi ya nia yetu ya ku-*control* mapato, ni suala ambalo linahusiana moja kwa

moja na usalama wa nchi. Kwa sababu *violators* wengine wanakuja na meli kubwa wakiwa wamebeba silaha ambazo zinakuwa kwenye *transit,* wengine wanakuja wakiwa wamebeba madawa ya kulevya na kama hujalihusisha Jeshi kwenye hili suala, mfumo mzima wa kuweza kudhibiti *Deep Sea* hautafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 1982 inazitaka nchi kujenga uwezo na sisi hatuwezi katika ile sheria yetu ya 1989, ile ya *Territorial Sea Exculsive Economic Zones* hatuwezi kabisa kuitekeleza ile sheria bila ya kuwa na uwezo wa kiutendaji ambao unalihusisha Jeshi na unahusisha vyombo mbalimbali vya kiusalama.

Kwa hiyo, Jeshi linahusika na *intelligence* ya nchi inahusika. Faida ambazo zitakuwepo tukihusisha vyombo vyote vya usalama, jambo la kwanza kuna tatizo kubwa la ujasusi unaendelea duniani na hili suala la *terrorism*. Kuna tatizo kubwa la watu kufanya *human traffic* wanawasafirisha tu wanadamu na sisi hatujui wanatolewa wanapelekwa wapi. Kuna tatizo zima hili la madawa la kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikuuliza ni kwa kiasi gani sisi tunaweza tuka-*control boat* inayoingia katika pwani kuanzia Mtwara mpaka Mombasa, ni vitu vingapi vinaingia, ni mara ngapi *boat* zitaingia sehemu ambazo hazina bandari usiku wakashusha watu, wakashusha zana na wakaondoka na sisi tunafanya nini katika kuokoa maslahi ya nchi? Nilitaka nijielezeshe sasa kuiomba Wizara iangalie ni jinsi gani hili *gimme* inayotengenezwa itataja maslahi ya nchi kwa masuala ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio tu sisi ku-*control* zile meli kwa sababu hatuwaamini hawa watu wanaokuja na hizo meli, hatujui wamebeba nini, hatujui nia yao ni kitu gani, wanakuja kuvua samaki wangapi, kuna hili suala la ujasusi wa kiuchumi wanaiba. Kama tutaendelea kuibiwa Dola za Kimarekani milioni 50 katika miaka mitano ijayo, wakati sisi tunawekeza milioni 116 kidogo kidogo tufikie ule uwezo, Dola 50 milioni tutapoteza kila mwaka, tutakuwa tumepoteza robo bilioni. Robo bilioni ya Dola za Kimarekani ni sehemu kubwa sana ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa kusikia katika hili *gimme* inayooanzishwa katika kuwekeza bilioni 116, ni lazima kuwepo uwezekano wa kuanzishwa viwanda vya ku-*process* mazao yote ya bahari, samaki wa aina zote ama Zanzibar, Dar es Salaam ama sehemu nyingine.

Naomba iwekwe kipengele cha sheria kama walivyofanya nchi nyingine, hawa watu wanaovua katika maji yetu walazimike kuweza ku-*process* na kuweka *value addition* kwa sababu viwanda hivi kwanza vitaweka ajira, hilo jambo la kwanza. Viwanda hivi katika ku-*process* hawa samaki hapa Tanzania vitatusaidia sisi kuongeza uwezo wa ufahamu na uwezo wa utaalamu katika suala zima la soko la samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine zinawataka wavuvi wasiondoke na samaki ghafi. Mimi sijaona kipengele kinachosema hawa watu wanaovua walazimike kuhakikisha kwamba samaki hao wanakuwa *processed* Tanzania ili tuweze kuongeza

thamani kwa kile ambacho kinakwenda kuuzwa nje. Hii narejea kusema Mheshimiwa Waziri kwamba thamani kwa wanachokilipa wao itaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru na narudia kusema tena kwamba naunga mkono hoja hii. Namwomba Mheshimiwa Waziri ajielekeze katika yale ambayo niliyasema ili tuone tutaboresha kwa kiasi gani Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitangulie kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, hali kadhalika wale ambao wamewasilisha Taarifa mbalimbali za Kamati kuanzia Kamati inayohusika na pia upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi niliyotaka kuyazungumza naona yamezungumzwa, sasa nitakuwa na muda mfupi sana wa kuzungumza yale machache ambayo yamebakia kwa maana ya kuupa nguvu zaidi Muswada huu. Bila ya kusahau basi, niseme kwamba na mimi kama walivyo wenzangu naunga mkono Muswada huu ili uweze kupita na kufanya kazi kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza kabisa nasema, kwangu mimi kwa mara ya kwanza nitoe shukrani sana kwa Wizara zote mbili ambazo zimeainishwa katika Muswada huu kwa maana wa ile Wizara inayohusika na mambo ya uvuvi kule Zanzibar na Wizara inayohusika na mambo ya uvuvi hapa Tanzania Bara katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuona kwamba baada ya muda mrefu kupita, Muswada huu huwa unakwenda, unarudi, sasa basi tuuangalie na kuujadili na pia kuutilia nyama pale ambapo tunahisi panafaa kufanya hivyo.

Nizipongeze Wizara hizi kwa sababu hiyo kubwa kwa sababu Watanzania hasa tunaoishi katika sehemu za bahari tuweze kufika pahali manufaa ya bahari ambayo sisi imetuzunguka tuweze kuyaona. Muda mrefu tumekuwa tukidhalilishwa na tukinyang'anywa sehemu zetu kubwa sana za bahari kwa sababu tulikuwa hatuna chombo hiki ambacho tunakizungumza hivi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nimpongeze vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uono wao wa kuona kwamba hivi sasa umeshafika wakati wa kuwa na mikutano katika kipindi cha mwaka, mikutano maalum ya kuondosha kero katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu moja katika kero ni hii.

Nashukuru Muswada huu leo umekuja, utakuwa umepitishwa na Bunge lako Tukufu na utakwenda kwa wananchi, itaundwa mamlaka, lakini ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Waziri mwenzao wa Zanzibar, Muswada huu utakapoanza kufanya kazi usije ukatoa changamoto ya kero nyingine, litakuwa ni jambo la aibu sana. Lakini Muswada huu uwe mfano wa Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba tumeujadili na tumeupitisha na unakwenda sambamba kama ulivyokubaliwa na Bunge lako Tukufu ambalo leo tunazungumzia Muswada huu. Kwa hiyo basi, mikutano yao imepelekea Muswada huu leo uwasilishwe kwetu na kwa kweli imechangia sana mikutano hiyo katika kufanikisha azma yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya ambayo yamezungumzwa hapa kuanzia kwenye Kamati na Mheshimiwa Waziri, hivi sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina 43 tumesikia hapa tumeambiwa. Ndani ya miaka hii 43 tuna Wizara mbalimbali zinazohusu mambo ya Muungano. Kuna vitengo vinavyohusu Muungano, kuna sekta zinazohusu Muungano. Katika kipindi cha miaka 43 Zanzibar tulikuwa tunazungumzia sana kuhusu Benki Kuu na katika kipindi hicho tukasema kwamba basi Benki Kuu ijengwe Zanzibar au iweko Benki Kuu Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fahari kubwa, napenda sana kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba wamesikia kilio chetu na Benki Kuu hivi sasa imejengwa Zanzibar. Ni kitengo cha mwanzo. Naanza na huko kwa sababu nataka nije niseme neno katika Mamlaka hii. Usije ukaniona labda nimetoka nje wa Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoonekana hivi sasa katika Benki Kuu ambayo imejengwa Zanzibar, kana kwamba kile kilio chetu labda kuna mtu amesukumiza tu basi, kama wanataka wapelekee. Maana yake lile jengo kubwa lina vitu vingi. Lakini nilichotaka kukisema hapa ni kwamba, na Watendaji nao basi wawe sambamba na aina ya jengo lililojengwa. Sasa kwenye mamlaka hii, wenzangu hapa wamesema Makao Makuu wanapendekeza yawe Zanzibar.

Mimi nasema Makao Makuu ya Mamlaka hii iwe Zanzibar kwa sababu maalum. Sababu ya kwanza niliyoieleza hapo mwanzo ni kwamba, Zanzibar imezungukwa na bahari, lakini ukiiangalia na hata hiyo ramani ambayo imeoneshwa katika Kamati mbalimbali ya hiyo bahari kuu, sehemu kubwa inaigusagusa Zanzibar.

Lakini kama hiyo haitoshi, Msemaji mmoja wa Kambi ya Upinzani alikuwa amezungumzia *Marine Institute* ambayo iko pale Zanzibar. Lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri atilie maanani na akaipa uzito kauli yangu hii au ombi langu hili kwamba hivi karibuni *Marine Institute* ile inakaribia kuwa ni Kitivo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sasa kwa sababu hiyo basi na kwa kuunga mkono Makao Mkuu au Benki Kuu kuwa tayari iko Zanzibar, basi hili liwe jambo la pili katika miaka 43 ya Muungano.

Mamlaka hii iwe Makao Makuu yake yako Zanzibar na ipewe uwezo unaostahili kama ulivyopendekezwa hapa. Wafanyakazi wafanye kazi kwa mujibu wa taratibu wa mamlaka inavyotaka wa pande zote mbili na wale watalamu ambao wako katika Jamhuri ya Muungano wasione uvivu au wasione taabu kuja Zanzibar. Kwa hiyo, Mamlaka iwe inaweka utaratibu maalum wa wafanyakazi tusije tukapata Makao Makuu yaliyokuwa hayana wafanyakazi, itakuwa hatujafanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano mdogo hapa, maswahibu zangu watakubaliana na mimi. Zamani pale Zanzibar mfanyakazi wa Serikali akipewa *transfer* kwenda Pemba, basi vita vyake havikamatiki. Yuko tayari kuacha kazi. Kwa nini? Anasema ameambiwa akafanye kazi Pemba. Maana anaona kama jehanam.

Lakini la ajabu ambalo lililokuwa linatokea akishafika Pemba kipindi cha miezi sita, mwambie rudi Unguja basi, anasema mnanionea. Sasa na wenzetu wasije wakaona kule Zanzibar kama jehanam, hapana. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makao Makuu ya Mamlaka hii iwe Zanzibar. Wataalamu waende Zanzibar kufanya kazi na vyombo vyetu vishirikiane katika kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kilio kikubwa cha Wazanzibar hasa katika masuala ya Muungano ni kuweka kweli kwamba tuko pamoja katika Jamhuri ya Muungano na Jamhuri ya Muungano haifanyi kazi kama Zanzibar haimo.

Kwa hiyo, pendekezo langu na ombi langu kubwa kwa Mheshimiwa Waziri watakapofika katika hatua ya kujadili suala la Makao Makuu kwa sababu humu bado halijajadiliwa, wajadili na kuchukulia kwamba mapendekezo haya yanayotoka upande huu wa Zanzibar yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nirudie tena kupongeza wale wote ambao wamechangia na wale wote ambao wameupitia Muswada huu na mimi niseme naunga mkono mia juu ya mia uweze kufanya kazi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kwanza nikushukuru wewe sana kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi nichangie machache ambayo mengi wenzangu wameshayazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukushukuru na kukupongeza hasa pale ulipoanza kuwakaribisha Wajumbe wengi katika Kamati yako ya Maliasili na Mazingira ambapo tulipata kuchangia kwa kirefu sana. Mfumo ule uliofanya umejenga demokrasia nzuri na umejenga hoja ya kuunganisha sehemu zetu zote. Maana uliwapa nafasi Wataalam, ukawapa nafasi Wabunge wa sehemu yoyote aje kwa uhuru, ruksa na ilikuwa ruksa kweli. Nakupongeza sana na nakutakia kila la kheri katika kazi yako nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianzie kwa kusema kwamba naipongeza kwanza hoja hii yote mia juu ya mia na siwezi hata siku moja kumwangusha rafiki yangu katika suala hili namuunga mkono rafiki yangu Waziri muhusika. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuileta hoja hii, hoja ambayo muda mrefu kama walivyosema walionitangulia ilikuwa inakwenda, inarudi, inakwenda inarudi. Kuna nini? Nchi moja kama hii, nchi imezaliwa baba mmoja mama mmoja, Wazee wakaona basi ni vizuri wakawa wamoja tu na imekuwa Tanzania moja. Lakini kwa nini masuala yetu yaende yarudi? Lakini kulikuwa kuna matatizo ya hapa na pale ambayo Wazee wameona na sasa yanaonekana yanaondoka na yataondoka haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa sababu amejaribu kuvitatua vipengele vyote ambavyo zamani vilionekana kuwa kero katika sehemu zetu mbili za

Muungano. Kwa maana hiyo, mimi nampongeza Waziri na kuipongeza hii na ndiyo maana nimeanza kutamka kwanza naiunga mkono hoja hii.

Katika kuchangia kwangu, nataka kuzungumzia huu uvuvi wa *Deep Sea.* Tumeingia kwenye kazi ambayo ni kubwa na ukubwa na ugumu wake utakaokuwepo kwa sababu ukweli bado hatujajipanga vizuri katika katika ulinzi, kila nikitizama hali yetu ya ulinzi. Tumesema hapa tuna vyombo vya *Navy*, tuna vyombo vya *KMKM,* tuna vitu vizuri vizuri lakini kwa kweli uvuvi wa *Deep Sea* tunaziona meli wakati tunapokuwa tupo nje. Meli zao kwa kweli ni kubwa, zinaweza kukabili hali yoyote ya hewa mbaya inayoweza kutokea kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli hizo ndani yake kunakuwa na viwanda vidogo vidogo. Wanatengeneza samaki ndani ya vyombo vyao kule. Yaani wanatia kwenye vikopo kule kule baharini. Kwa jinsi ya vyombo vilivyokuwa vikubwa, vina uwezo na wenzetu wamejiandaa vizuri. Sasa tujiuliulize, kweli tuna vyombo angalau vinavyoweza kufika katika hizo *mile* 200 hizo za uvuvi? Tunazungumza muda mwingi sana hapa, jamani samaki wetu wanachukuliwa, lakini sasa tunaweka sheria, hivi tutategemea *South Africa* watukamatie watu watuletee hapa? Hakuna hiyo.

Mimi namkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa kweli tunataka kujiandaa kupata mali yetu kikamilifu, basi tukubali kuweka ulinzi unaoweza kukabili hali hii. Tukubali kupata manoari za kuweza kufanya kazi hiyo, tukubali sasa hivi kugeuka pale tulipo, kuondoka kwenye *Coastal Patrol Boats* tuingie kwenye *Medium Ground Boats*, zitakazoweza kukabili hali ya huko.

Halafu nataka kueleza jambo lingine hapa. Katika meli za uvuvi nyingine wanakuwa na silaha, wanajiandaa hasa; tukipeleka hivi vyombo vyetu vidogo vidogo vitaweza kukabiliana na hali hiyo? Kwa sababu anajua anakwenda kutafuta shari kuvua kwenye bahari ambayo sio yake, anajua kabisa anachokifanya sicho na anajua akikamatwa atapata *penalty* kubwa. Sasa vipi mtu kama huyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wapo ndiyo kazi zao, wametoka huko na Meli zao wakaenda huko na kufanya kazi kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba niliongezee nguvu ambalo wenzangu wameshalizungumza. Ni kuhusu suala la mgao. Suala la mgao limewekwa vizuri sana na mimi sina pingamizi. Lakini naomba sana liangaliwe suala la uchumi wa Zanzibar. Hali ya uchumi wa Zanzibar ni mbaya na ngumu kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutafanya dhambi Bunge lako Tukufu likaonyesha kwamba basi hata kuwapa nusu kwa nusu sio mbaya ili tuunyanyue uchumi wao. Lakini sio kwa maana nyingine, ni kwa maana ya kuwasaidia, wenzetu wana hali ngumu, hiyo lazima tukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ambalo naomba nichangie, wenzangu wamezungumza kwa ufasaha zaidi, maana wote waliozungumza wanakijua Kiswahili

vizuri sana, wametamka Kiswahili cha ndani kabisa. Mimi sio mtaalam sana wa kuzungumza Kiswahili vizuri, lakini ninachotaka kuzungumza ni kwamba kweli umefika wakati tuonyeshe kwamba muungano wetu wa pande zote mbili na watu waondoe mashaka madogo madogo haya na hatutafanya kosa endapo kwa kweli tutafanya Makao Makuu yawe Zanzibar. *(Makofi)*

Tutafanya vizuri, kwa sababu yale maneno madogo madogo, mwenzangu mmoja akazungumzia Benki na wengine wamezungumza hapa namna ya kuonyesha kwamba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inahaki sawa katika mambo ya muungano.

Kwa hiyo, mimi naunga mkono hiyo na naomba sana ingawaje haimo na kwa sababu haya mambo tunaachia wazee, lakini wanatusikia tunachokizungumza. Ingekuwa vyema wakaliona hili na wakaweza kutengenezwa kama vile ambavyo yanatengenezwa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wamechangia mengi sana na unapochangia mwisho unakuwa huna pa kupita zaidi kuliko pale walipopita wanzako na Bunge letu wanasema usirejee yale yaliyozungumzwa na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa mara nyingine tena hasa kunipa nafasi hii ya kuwa msemaji wa mwisho. Natamka tena kwamba niunga mkono tena hoja hii, wananchi wangu wote wa Jimbo langu la Bumbwini pamoja na mimi mwakilishi wao hapa tunaiunga mkono hoja hii mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni kwa kuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Profesa Jumanne Maghembe kwa ajili ya kujibu hoja za wachangiaji. Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA MALIASIALI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kutupa fursa hii kutoa maoni kwenye hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo umezisikia asubuhi hii zilikuwa ni nzuri, zilikuwa zimelenga katika kuboresha Muswada ambao tunao na katika kutuweka sawa, ambayo kwa kweli ni magumu na ndiyo yalikuwa yamefanya kwa siku zote hizi Mamlaka ambayo tunataka kuiunda isiweze kuundwa. Kwa hiyo, leo nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Tumefurahi sana kuona kwamba kila Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza aliona hatua kubwa ambayo imefikiwa na kuunga mkono hoja ambayo tumeitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia hoja hii kwa kusema hapa ndania ya Bunge ni Mheshimiwa Raynald Mrope, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Mheshimiwa Hafidh Ali na Mheshimiwa Kanali Feteh Mgeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Castro Ligallama, Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Omar Yusuph Mzee, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna ambao nimewasahau katika orodha hii, naomba jinsi ninavyoendelea, basi waniletee nitatangaza majibu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Kamati ya Mazingira na Maliasili kwa mchango wao mzuri na kwa mawazo ambayo wameyatoa, mengi ni ya ushauri na tumeyachukua na tutayafanyia kazi kwa kadri inavyowezekana. Ushauri juu ya kuteuliwa kwa wachumi wawili tumeuzingatia na kuhusu mgao ambalo ndilo suala kubwa ambalo lizengumzwa na karibu kila Mheshimiwa Mbunge.

Kwanza ningependa niseme tu kwamba, suala la Uvuvi, Sekta ya Uvuvi sio moja ya Sekta za Muungano. Haiko katika zile Sekta za Muungano. Sasa baada ya kusema hayo na kabla ya *formula* ile mpya ya Kamati ya Shellukindo, haijatolewa *formula* ambayo ipo ni asilimia karibu nne ya mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, inakwenda kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika mgao huu ambao unapendekezwa hapa, asilimia 50 ya mapato yatakwenda kwenye mamlaka yenyewe ili iweze kuendesha mamlaka. Sasa asilimia 50 ile inayobaki itagawanywa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupata asilimia 20 ya fedha zote na Serikali ya Muungano asilimia 30.

Mimi nadhani tungealia vigezo ambavyo vimepelekea kule mwanzo tuwe na asilimia nne kwa asilimia 96 kulingana na ukubwa wa nchi, watu wengi na vigezo vingine ambavyo vimewekwa ili tuelewe kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepata mgao ambao unazingatia sehemu ya uvuvi katika uchumi wa Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezingatia ushauri kwamba kutokana na umuhimu wa Sheria hii, tutunge kanuni mara moja na hili litafanywa. Ni kweli kama tumekuwa na matatizo katika uvuvi kwenye Bahari Kuu kwa sababu ya uwezo wetu wa ku-*patrol* na kusimamia uvuvi kwenye Bahari hiyo. Lakini napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba hivi leo tuna uwezo wa kuziona meli zote ambazo zinaingia kwenye *exclusive economic zone* ya nchi yetu kwa maana pale kwenye Idara ya Uvuvi tuna rada ya kuona meli zote ambazo zinaingia kwenye Bahari yetu.

Hatua ya pili ambayo tunachukua ni hii ambayo tumetenga Dola za Kimarekani milioni 16 pamoja na mambo mengine kununua Boti za kuweza ku patrol na kuzifuata meli zile wakati zikiwa zinavua katika bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona katika azma hii tumeweka faini kubwa sana kwa meli ambazo zitakuwa zinaingia mle na kuvua bila kupata leseni. Tunao mradi wa

*Marine and Coastal Environmental Management Program* (*MACEMP*) ambao umetengewa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 61. Kati ya fedha hizo Shilingi milioni 21 zitatumika Zanzibar.

Fedha hizi pamoja na mambo mengine zitawawezesha wavuvi wetu kuweza kuwa na vifaa vya kuweza kuingia katika Bahari Kuu kutuongezea uwezo wa ku-*patrol* katika Bahari Kuu na kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi katika Ukanda wa Pwani na katika Mikoa iliyoko Zanzibar. Kwa hiyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge waupitishe Muswada huu na marekebisho haya ya Muswada huu kama sehemu ya kwanza ya kushughulikia matatizo ambayo yako kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Audit* katika Mamlaka mpya, Mamlaka hii inayoanzishwa itakuwa sawasawa na Mamlaka nyingine zote za Umma. Kwa hiyo, utaratibu wa *Audit* utafuata utaratibu ambao unatumika katika Mashirika yote ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kwa kiasi kikubwa na mapendekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid na kama nilivyosema hapo awali, kupitia Muswada huu na kupitia mradi wa *MACEMP* tutaweza kutatua matatizo mengi ambayo sasa yapo katika sekta ya uvuvi katika Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa William Shellukindo aliongea mambo ya msingi ya Kikatiba pamoja na Sheria hii. Lakini pale awali nilisema kwamba Sekta ya Uvuvi sio moja ya maeneo ya Muungano. Kwa hiyo, Sheria hii inatungwa ili kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tuweze kusimamia na kufaidika na uvuvi katika Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu alieleza mambo mengi muhimu na ambayo yanazingatia hali na matatizo ambayo tunayo katika Bahari Kuu. Hata hivyo kama nilivyoeleza hapo awali, hatua muhimu zinachukuliwa sasa katika kuimarisha ulinzi katika Bahari Kuu na suala la ulinzi wa Bahari yetu na nchi yetu ni jambo muhimu sana na liko chini ya Sheria nyingine. Hapa tunachotaka kusisitiza ni kutunga Sheria ambayo itatuelekeza nguvu zetu katika kufaidika na rasilimali tulizonazo katika *exclusive economic zone* ya nchi yetu. Masuala ya msingi yanayohusika na kudhibiti madawa pamoja na ugaidi yapo katika utaratibu ambao umo katika Sheria hizi na Sheria nyingine.

Ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Hafidh Ali kwa jinsi alivyoeleza suala hili kwa undani na alivyoliweka wazi suala la Makao Makuu ya Mamlaka hii. Suala hili pia limo katika michango yote ya maandishi ambayo tumeletewa. Napenda kusema kwamba Wizara yangu haina tatizo kabisa na Makao Makuu ya Mamlaka ya Shirika hili kukaa Tanzania Zanzibar. Kitakachotakiwa ni utaratibu tu wa Kiserikali ambao ni lazima tuufuate ili kutekeleza maombi haya ambayo naona yameletwa na Waheshimiwa Wabunge kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa kifupi, haya ndiyo mengi ya maswali ambayo yaliletwa na Waheshimiwa Wabunge na napenda tena niwashukuru sana kwa

mawazo mazuri kwa michango mizuri na katika kulenga kutusaidia katika kutekeleza shughuli zetu. Ninatumaini kabisa kwamba, Waziri mwenzangu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambaye nina uhakika alisikia michango hii atakuwa amefarijika sana kwa michango ambayo imetolewa hapa, jinsi gani ilivyolenga katika kujenga na kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutoa hoja na hoja imeungwa mkono. Katibu hatua inayofuata.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Kusimamia Uvuvi Katika Bahari Kuu wa Mwaka 2007 *[The Deep Sea Fishing Authority Amendment Bill, 2007]***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nipate uelewa, yale maneno yanayosema *'Mainland Tanzania'* kama limezingatiwa katika kurekebishwa. Kwa sababu hii inafuata na Katiba, tafsiri ya Kiingereza.

Katika Muswada mmoja uliopita, ilirekebishwa hiyo. Kwa hiyo, nadhani tungekwenda hivyo. Mahali popote inapokuwa:- *Tanzania Mainland,* iwe *Mainland Tanzania.*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya maneno *'Tanzania Mainland'* katika eneo ambalo limechapwa ni makosa. Usahihi ni *'Mainland Tanzania.'* Kwa hiyo, imezingatiwa na marekebisho yatafanywa. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu wa mwaka 2007 *(The Deep Sea Fishing Authority Amendment Act, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu, yaani *The Deep Sea Fishing Authority Amendment Act* 2007 pamoja na marekebisho yake na kuukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, saa 11:00 jioni tutaanza na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusiana na Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani kuhusu Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamalizia shughuli za hapa, Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro alikuwa ana wageni wake ambao aliomba niwatambulishe nao ni pamoja na Dr. Mkumbo, karibu sana.

Huyo ni mtumishi wa Mamlaka ya Ngorongoro, Ndugu Mrambo. karibu sana na Ndugu Metele, Meneja wa *PC* ya Ngorongoro. Tunawashukuruni, karibu sana kwenye Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hapa tulipofikia, naomba kusitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 6:35 mchana Bunge lilifungwa mpaka 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani Kuhusu Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku *(The World Health Organization Framework Convention on Tobacco Control)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niungane na wenzangu walionitangulia kuzungumza, kwa kutoa salam za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais na Serikali nzima na kwa Mheshimiwa Mwenyekiti, familia, ndugu, jamaa, wakazi na wapiga kura wote wa Tunduru kwa kifo cha Mbunge mwenzetu na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu akishughulikia Masuala ya Bunge, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, kilichosababishwa na ajali ya ndege. Marehemu atakumbukwa daima kwa uchapaji kazi na uadilifu wake na moyo wake wa kujituma, uongozi wake bora na namna alivyoweza

kujenga uhusiano mzuri na wabunge wenzake. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile nichukue nafasi hii pia, kupitia Bunge lako Tukufu, kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uteuzi wake ni heshima ya kipekee kwa wanawake wa Tanzania na Taifa letu kwa ujumla. Tunamtakia kila la kheri katika wadhifa wake huo na majukumu yake mapya.

Vile vile, naomba niwapongeze kwa dhati Mheshimiwa Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, Mbunge, Mheshimiwa Bernard K. Membe, Mbunge, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo na Mheshimiwa William M. Ngeleja kwa kuteuliwa kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Nawatakia kila la kheri katika majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, hoja ya Azimio la Bunge kuhusu Tanzania kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani unaohusu Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku *(The World Health Organization Framework Convention on Tobacco Control).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini pamoja na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Jimbo la Muyuni na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa kupitia Mkataba huu na kutoa maoni, ikiwa ni pamoja na kukubali Azimio husika liwasilishwe kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Mkataba huu ni kulinda afya ya binadamu katika kizazi cha sasa na kizazi kijacho kutokana na madhara yanayotokana na matumizi ya tumbaku na moshi wa tumbaku kwa wasiovuta. Mkataba huu umeweka utaratibu wa matumizi ya bidhaa za tumbaku na haupigi marufuku kilimo cha tumbaku. Hata hivyo, nchi zinahamasishwa kutafakari na kutafuta mazao mbadala ya kibiashara ili kutoathiri maendeleo ya nchi husika kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko na Madhumuni ya Mkataba, Ukirejea kumbukumbu za *Hansard* ya tarehe 7 Februari, 2003, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilijadili na kupitisha mapendekezo ya kutunga Sheria ya Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku nchini. Madhumuni ya Mkataba huu hayana tofauti na madhumuni yaliyosababisha kuwepo kwa Sheria ya Kudhibiti Tumbaku Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku ina aina 4,000 ya kemikali ambazo ni sumu kwa matumizi ya binadamu. Magonjwa yanayotokana na matumizi ya tumbaku kwa njia ya kuvuta sigara, kutafuna, kunusa na kubwia ugoro ni mengi ni zaidi ya 25 na madhara yake ni makubwa. Magonjwa hayo yanasababisha gharama kubwa za matibabu, kupunguza ufanisi na ubora wa maisha ya mvutaji na kufupisha maisha. Imekadiriwa

kwamba katika kila Sh. 7/= anazopata mkulima kutokana na tumbaku, Sh. 6/= zinakwenda kutibu madhara yanayotokana na tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ambayo yamethibitishwa kisayansi kuwa yanaletwa na uvutaji au kukaa karibu na mtu anayevuta sigara ni pamoja na magonjwa ya mapafu ya aina mbalimbali kama vile kukohoa mara kwa mara, saratani ya mapafu na magonjwa ya moyo na mishipa ya damu. Pia, utumiaji wa tumbaku husababisha shinikizo la damu *(high blood pressure)*, ambalo ni chanzo kimojawapo kikuu cha ugonjwa wa kiharusi *(stroke)*. Kwa wanaume, uvutaji sigara pia huchangia kupunguza nguvu za kiume na kwa mama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudie sehemu hiyo. Kwa wanaume, uvutaji sigara pia huchangia kupunguza nguvu za kiume na kwa mama wajawazito uvutaji na ukaaji karibu na mvutaji sigara huleta madhara ya kuharibu mimba au kujifungua kabla ya wakati, kuzaa watoto njiti na wenye maumbile yenye kasoro. *(Makofi)*

Mbali na athari za uvutaji, kuna matumizi mengine ya tumbaku ambayo huleta madhara kwa afya yetu. Ugoro ni mfano mmojawapo ambao unaweza kusababisha saratani ya kinywa kwa mtumiaji. Inakadiriwa kwamba vifo milioni tano vinatokea kila mwaka kutokana na matumizi ya tumbaku duniani na hii ni sawa na mtu mmoja (1) kufariki kila sekunde nane.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba kwa kila tani 1,000 za tumbaku zinazozalishwa, zinasababisha vifo vya watu wasiopungua 1,000. Katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwa mojawapo, utumiaji tumbaku unaongezeka. Hata wanawake ambao huko nyuma hawakujihusisha na tabia ya kutumia tumbaku, sasa wanafanya hivyo. Asilimia 10 ya wavutaji katika nchi zinazoendelea ni wanawake. Hali hii inachangiwa na matangazo ya bidhaa za tumbaku yanayolenga wanawake, vijana na watoto walio chini ya umri wa miaka 15 ambao ndiyo Taifa letu la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa makampuni ya kigeni yamekuwa yakikimbilia kuhamasisha jamii katika nchi maskini waongeze utumiaji wa tumbaku kutokana na ukweli kwamba matumizi ya bidhaa za tumbaku katika Mataifa yaliyoendelea unapungua kwa kasi kubwa. Mataifa tajiri yamejiwekea sheria kali ambazo zimechangia kupunguza matangazo ya bidhaa hizo pamoja na uvutaji wa sigara katika sehemu zenye mkusanyiko wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo hapo juu, pamoja na tafiti mbalimbali za kisayansi za muda mrefu kuhusu madhara yanayotokana na tumbaku pamoja na bidhaa zake, Shirika la Afya Duniani liliona ni jambo la busara katika historia yake na kwa mara ya kwanza, kutumia uwezo wake chini ya Ibara ya 19 ya Katiba iliyoanzisha Shirika hilo, kutayarisha Mkataba huu muhimu kwa lengo la kulinda afya za wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu wa kudhibiti Tumbaku, yaani una jumla ya vipengele 38. Baadhi ya vipengele muhimu katika Mkataba huu ni kama ifuatavyo:-

Kwa utangulizi inaelezwa kwa nini nchi wanachama wameamua kuwa na Mkataba huu, maelezo haya yanaendana na maelezo ya awali ambayo yanahusu Chimbuko la Mkataba.

Ibara 1 – 2 kama ilivyo kawaida, inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali kama yalivyotumika katika Mkataba. Katika kuelezea Mkataba huu, Ibara ya 3 – 5, madhumuni makubwa ni kulinda kizazi cha sasa na kinachokuja kutokana na madhara yanayotokana na tumbaku kiafya, kijamii, kimazingira na kiuchumi. Nchi wanachama zinaonyesha nia ya kisiasa *(Political Commitment)* katika kutekeleza azma hii. Kushirikiana baina ya nchi washirika wa Mkataba kwa ajili ya kubadilishana utaalamu mbalimbali katika kutekeleza Mkataba huu hasa njia na mikakati ya kudhibiti matumizi ya tumbaku ni mambo yaliyoelezewa katika sehemu hii.

Ibara ya 6 – 14 zinazungumzia masuala mbalimbali yanayohusu njia mbalimbali za kupunguza matumizi ya tumbaku. Njia hizo ni pamoja na kuweka bei kubwa kwa bidhaa za tumbaku, kuongeza kodi, kuweka sheria mbalimbali za kudhibiti tumbaku, kuzuia kupata moshi wa sigara kwa watu wasiovuta, kuweka viwango maalum vya tumbaku na kulazimisha watengenezaji kuelezea aina na kiasi cha sumu zilizomo katika bidhaa zao.

Vilevile, masuala ya ufungaji na maandishi kwenye pakiti za sigara hayatakiwi kuwa na matangazo yenye ujumbe potofu, bali yazingatie ukweli kuwa bidhaa za tumbaku ni sumu. Kwa mfano utakuta tumbaku inayoitwa *low-tar* au *light*, *ultra-light* au *mild*. Haya yote yanalenga kumshawishi mtumiaji aamini kwamba bidhaa hiyo ni salama na haya hayatakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika matangazo, onyo la kutahadharisha itabidi lichukue asilimia 50 ya upande mpana wa paketi na halitakiwi liwe chini asilimia 30.

Aidha, kuhusu suala la matangazo, nchi zimeshauriwa kukataza kabisa matangazo, udhamini na promosheni kulingana na sheria za nchi, kwani utafiti umeonyesha kwamba kukataza kabisa matangazo na promosheni kwa kiasi kikubwa kunapunguza ushawishi na matumizi ya tumbaku na bidhaa zake.

Vilevile, kwa kuruhusu matangazo na promosheni inakuwa ni kwenda kinyume na maadili ya afya kwani inakuwa tunaruhusu matumizi ya bidhaa ambayo kisayansi imedhihirika kwamba inaathiri afya ya binadamu na husababisha vifo.

Sehemu ya IV ambayo ina Ibara ya 15 – 17, imeainisha uzuiaji wa uuzaji wa magendo wa bidhaa za tumbaku, uuzaji wa bidhaa za tumbaku kwa watoto na vilevile nchi wanachama kuweza kusaidiana namna ya kutafuta njia mbadala kwa zao la tumbaku ili kuweza kuwasaidia wakulima wanaotegemea zao la tumbaku katika maisha yao. Hapa nchini Tanzania, baadhi ya Wilaya mfano Ludewa, Songea Vijijini, Mpanda, Kigoma Vijijini na kadhalika., tayari ziko katika hatua za awali za kutafuta mazao mbadala kama vile kahawa, soya, pilipilihoho, ufugaji wa nyuki na kadhalika. Aidha, mazao ya kilimo

cha korosho, maua, vanila na bustani za mboga yamependekezwa kutegemeana na hali ya hewa ya eneo husika.

Mkataba huu haupigi marufuku kilimo au biashara ya tumbaku. Kuna nchi kama Japan, Canada, China, Brazil, India, Bangladesh, Indonesia ambazo zinaongoza Duniani kwa kilimo na biashara ya tumbaku, lakini tayari zimeisharidhia Mkataba huu. Mategemeo ni kwamba tutaharakisha utafiti wa mazao mbadala kwa mtindo wa *phase in* and *phase out*. Tunapo-*phase in* zao mbadala na tumbaku nayo inatoka pole pole. Tumekubaliana na wenzetu Wizara ya Kilimo kwamba zao litakaloonekana kwamba linafaa katika eneo fulani, basi kutakuwa na mashamba ya mfano ili wakulima waweze kuiga.

Sehemu ya V, VI na VII inazungumzia habari za kulinda mazingira, masuala ya fidia na ushirikiano katika masuala ya kisayansi, kiufundi na mawasiliano kati ya nchi ambazo ni washiriki wa Mkataba huu.

Vifungu vya mwisho viko katika sehemu ya 11 ambavyo vina Ibara 30 - 38. Hapa kama ilivyo katika taratibu za mikataba ya kimataifa imeainisha namna nchi mwanachama inavyoweza kujiondoa, haki ya kupiga kura, namna ya kutengeneza Itifaki mbalimbali chini ya Mkataba huu, taratibu za kusaini, kuridhia, utunzaji wa Mkataba na itifaki zake, namna ya Mkataba utakavyoanza kufanya kazi na masuala yote yanayohusiana na hayo.

Mkataba wa *World Health Organization* wa Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku, umeweka historia katika Umoja wa Mataifa kuwa mmoja wa Mikataba ambayo imepata saini nyingi duniani. Mkataba huu ulisainiwa na nchi 169. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Mkataba huu tarehe 27 Januari, 2004. Hadi kufikia mwezi Januari, 2007 nchi 142 tayari zimeridhia Mkataba huu. Hii inaonyesha jinsi nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa walivyoweza kupokea malengo mazuri ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bara letu la Afrika, ni nchi 17 tu ambazo bado hazijaridhia na Tanzania ni mojawapo. Kwa Tanzania kuridhia Mkataba huu na kuutekeleza tutaweza kutekeleza Malengo ya Milenia, ambayo Tanzania imekubali kuyatekeleza. Malengo hayo yana lengo la kuinua afya, elimu na maendeleo ya uchumi kwa ujumla kwa nchi husika. Malengo hayo ya Milenia yanafanana sana na malengo ambayo tayari Tanzania imejiwekea, kupitia Dira yake ya Maendeleo ya 2025 na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tayari inayo Sheria ya Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku iliyopitishwa mwaka 2003, Sheria ambayo kimsingi ina malengo yaliyopo kwenye Mkataba tunaozungumzia leo. Sheria hii inahusu usimamizi wa matumizi ya bidhaa za tumbaku na inasimamiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ina lengo la kudhibiti matumizi ya bidhaa za tumbaku katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu, kuonyesha katika paketi na matangazo ya sigara madhara yatokanayo na tumbaku nakadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utaratibu wa Kuridhia Mkataba: Ibara ya 34 ya Mkataba ilitoa nafasi kwa nchi wanachama kusaini Mkataba. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 27 Januari, 2004 *New York,* Marekani na Balozi wetu wa Kudumu wa Tanzania, Umoja wa Mataifa Mheshimiwa A. Mahiga kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ilikuwa nchi ya 88 kusaini. Kimsingi, hii inamaanisha kuwa tumekubali kuheshimu malengo na madhumuni ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 35 ya Mkataba inaelezea bayana kwamba Mkataba huu utatakiwa kuridhiwa na nchi wanachama. Aidha, Ibara ya 63 (3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalitaka Bunge letu kuridhia Mikataba ya kimataifa ambayo masharti yake yanahitaji kuridhiwa. Hivyo, Azimio hili linalenga kutekeleza matakwa hayo ya kisheria na kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha; kwa kuwa faida za Azimio hili ni kubwa kwa maana ya kulinda afya za Watanzania na kwa kuwa tayari Tanzania ina Sheria ya Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku, ni vyema Tanzania ikaridhia mapema ili iwe mshiriki wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhia Mkataba huu kutaiwezesha nchi yetu kushiriki katika majadiliano yatakayosaidia utekelezaji, pamoja na tafiti mbalimbali za kutafuta mazao mbadala. Hivi sasa tumepewa hadhi ya *Observer Status*. Tafiti hizo zinahisaniwa na mfuko maalum chini ya Mkataba huu. Ni ukweli usiofichika kwamba, kutokana na kasi ya kusaini na hatimaye kuridhia na kutekeleza mkataba huu, zao la tumbaku litaondoka pole pole, inaweza ikachukua miaka 20, inaweza ikachukua miaka 30, lakini kama nilivyosema awali, mategemeo ni kwamba tutakuwa tuna-*phase in* mazao mbadala na ku-*phase out* zao hili ambalo tayari tunajua kwamba lina matatizo katika afya zetu.

Mwisho, kwa kuwa faida za Mkataba huu ni kubwa, naomba mtafakari na kukubali pendekezo la kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani wa Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku *(The WHO Framework Convention on Tobacco Control)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kusoma Azimio hilo.

**Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani Kuhusu Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku**
***(The WHO Framework Convention on Tobacco Control)***

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Afya Duniani ambalo lilianzishwa mwaka 1948 na Tanzania kujiunga mwaka 1962;

NA KWA KUWA nchi wanachama zimekuwa zikishirikiana katika kupanga mikakati ya kupambana na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza;

NA KWA KUWA Tanzania imekuwa ikishiriki kikamilifu katika kuendeleza malengo na madhumuni ya kuundwa kwa Shirika la Afya Duniani pamoja na kushiriki katika mikutano ya kila mwaka ya Baraza la Mawaziri wa Afya ulimweguni, *(The World Health Assembly*);

NA KWA KUWA Shirika la Afya Duniani lilianza kuchukua hatua dhidi ya uvutaji sigara kuanzia miaka ya 1970 baada ya kuona kwamba uvutaji sigara ni chanzo kikubwa cha magonjwa ya moyo na kwa kupitia Azimio la Baraza la Mawaziri wa Afya Na. 23:32 la mwaka 1970, iliamuliwa kwamba suala la udhibiti wa tumbaku liwe ni moja kati ya ajenda za vikao vya Shirika la Afya Duniani;

NA KWA KUWA tangu kupitishwa kwa Azimio hilo, Shirika la Afya Duniani lilichukua hatua mbalimbali ambapo mwaka 1978, Kamati ya Watendaji ya Shirika hilo iliazimia kwamba, suala la udhibiti wa tumbaku liwekewe mkakati wa pamoja ikiwemo kutungwa kwa sheria katika nchi husika kama sehemu ya mkakati huo wa kudhibiti tumbaku;

NA KWA KUWA mwaka 1986 Baraza la Mawaziri wa Afya kupitia Azimio lake la Tumbaku au Afya lilishauri nchi wanachama kuweka mikakati ya kudhibiti bidhaa za tumbaku kwa lengo la kulinda afya za wananchi wa nchi husika ikiwa ni pamoja na utungaji wa sheria mahsusi ya kudhibiti tumbaku, elimu ya afya, maonyo juu ya uvutaji wa sigara, kulinda vijana na watoto dhidi ya uvutaji wa sigara, kutafuta mazao mbadala na kadhalika;

NA KWA KUWA mwaka 1999, Shirika la Afya Duniani lilichukua hatua muhimu kupitia Bodi yake ya Utendaji, pamoja na kuazimia kutayarisha Mkataba wa kimataifa wa Shirika la Afya Duniani kuhusu kudhibiti Tumbaku ambao una lengo la kulinda wasiovuta sigara kupitia matangazo na maonyo, kuweka kodi kubwa zinazohusiana na sigara, kutoa elimu ya Afya kwa umma, na kadhalika;

NA KWA KUWA Mkataba huu uliidhinishwa na kukubaliwa rasmi kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri wa Afya katika kikao chake cha 56 cha tarehe 21 Mei, 2003 Mjini Geneva, Uswisi kupitia Azimio lake Na.56.1 la 2003;

NA KWA KUWA Ibara ya 34 ya Mkataba ilitoa nafasi kwa nchi wanachama kuweka saini katika Mkataba huo, Tanzania ilikuwa ni nchi ya 88 kuweka saini katika Mkataba huo, lakini hadi sasa Tanzania haijaridhia Mkataba huo;

NA KWA KUWA kuweka saini Mkataba huu na hatimaye kuuridhia na kuutekeleza, Tanzania itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Kupunguza na hatimaye kutokomeza madhara ya kiafya yatokanayo na bidhaa za tumbaku;

(b) Kushirikiana na nchi wanachama katika kutekeleza malengo na madhumuni ya Mkataba huu;

(c) Kubadilishana utaalam na wataalam ili kuweza kutafuta zao mbadala la tumbaku hasa ukizingatia kwamba Tanzania ni moja kati ya nchi zinazolima zao hili;

(d) Kushiriki kikamilifu katika Vikao vya wanachama *(Conference of Parties)*, vikao ambavyo vitasimamia utekelezaji wa Mkataba huu, ikiwemo kutafuta zao mbadala kwa nchi zinazotegemea zao la tumbaku kwa uchumi wa nchi zao na kuanzisha Mfuko maalum wa hiari kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Mkataba;

(e) Kuharakisha utekelezaji wa malengo ya Milenia, malengo ambayo Serikali imeyakubali na inayatekeleza; na

(f) Kupunguza na hatimaye kuondokana kabisa na madhara ya kimazingira yatokanayo na zao la tumbaku kama vile ukataji wa miti, rutuba duni ya ardhi yatokanayo na mbolea, uharibifu wa vyanzo vya maji kutoka kwenye sumu kali ya mbolea, madhara ya kiafya yatokanayo na mbolea na kadhalika.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa Sita na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani wa Kudhibiti Tumbaku, yaani *(The World Health Organisation Framework Convention on Tobacco Control)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JANETH B. KAHAMA (K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** MheshimiwaMwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa Maoni ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii uliyoipa jukumu la kufikiria Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kuhusu Udhibiti wa Bidhaa ya Tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii naomba kuchukua fursa hii kutoa rambirambi kwa Wapiga Kura wa Jimbo la Tunduru na familia ya aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge Hayati Mheshimiwa Juma J. Akukweti. Mungu ailaze mahali pema Peponi roho ya Marehemu.

Aidha, kwa niaba ya Kamati nampongeza aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Kamati inamtakia mafanikio mema katika nafasi hii ambayo ni adimu sana. Aidha, kwa niaba ya Kamati nawapongeza pia

Mheshimiwa Bernard K. Membe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Batilda S. Burian kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge. Tunampongeza pia Mheshimiwa Wiliam M. Ngeleja kuiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Vile vile, tunampongeza Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niendelee kuchangia**.** Kamati ya Huduma za Jamii ilifikiria Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani linalohusu udhibiti wa bidhaa za Tumbaku. Kamati ilipata maelezo ya Serikali kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitafakari maelezo ya Serikali kuhusu Azimio hili ilihoji masuala mbalimbali yanayohusu athari na faida za kuridhia Mkataba huo na baada ya kupata maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Kamati iliunga mkono hatua ya Serikali ya kutaka Bunge kuridhia Mkataba huu wa Shirika la Afya Duniani ambao unalenga kulinda afya za binadamu kutokana na athari za matumizi ya bidhaa za Tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti,pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii kuunga mkono hatua ya Bunge kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani unaohusu kudhibiti bidhaa za Tumbaku, Kamati imetoa maoni yafuatayo kwa lengo la kufanya utekelezaji wa masharti ya Mkataba huo kuwa na manufaa kwa wananchi.

Kwanza, Serikali ifanye juhudi za makusudi kuielimisha jamii hasa vijana kuhusu athari zinazotokana na matumizi ya bidhaa za Tumbaku, hasa moshi wa sigara, kwa kuvuta moja kwa moja au kuwa karibu na mvutaji, kutumia ugoro au tumbaku ya kutafuna maarufu kwa jina la *Kuber.* Aidha, ni vema wakaelimishwa magonjwa yanayotokana na matumizi ya bidhaa za Tumbaku kama vile saratani ya mapafu, saratani ya mdomo, shinikizo la damu, utasa wa wanaume, mimba kuharibika na kadhalika.

Mbili, Kamati inashauri Serikali isimamie vizuri utekelezaji wa Sheria ya *Tobacco Products Control Regulations Act 2003.* Kuhusu kuweka matangazo makubwa yanayotahadharisha jamii kuhusu athari za sigara hasa maandishi makubwa kwenye paketi za sigara kuliko utaratibu wa sasa wa kuweka maonyo kwa maandishi madogo madogo pembeni mwa paketi ya sigara yasiyoonekana kabisa. Pia mabango makubwa yanayowekwa kuhamasisha matumizi ya sigara yapigwe marufuku kabisa, ikiwa ni pamoja na kuzuia matangazo hayo kwenye luninga, makampuni ya sigara kudhamini mashindano na michezo mbalimbali na matukio makubwa ya Kitaifa na Kimataifa na yenyewe yapigwe marufuku. *(Makofi)*

Tatu, Kamati ina maoni kuwa mafanikio ya utekelezaji wa Mkataba huu yatapelekea kuleta athari za kiuchumi kwa wazalishaji wa zao la Tumbaku na hatima ya zao la Tumbaku litaendelea kuwa mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la Serikali ni kulinda afya za wananchi kutokana na athari za matumizi ya bidhaa za Tumbaku, ni vema pia Serikali ikatafuta jawabu la kisayansi kwa kufanya utafiti wa kupata zao mbadala la biashara ambalo litawaletea kipato cha uhakika badala ya zao la Tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali idhibiti mipaka ya nchi *(Entry Points)* ambazo husababisha bidhaa za tumbaku za bei nafuu sana kuingizwa nchini na kuendelea kuathiri afya za wananchi. Aidha, ipige marufuku uingizaji wa Tumbaku ya kutafuna iitwayo *Kuber* ambayo ilipigwa marufuku nchini India inakozalishwa na hatua kali zichukuliwe kwa wanaopatikana na Tumbaku hii. Serikali iongeze kodi kwa bidhaa zote za Tumbaku ili kudhibiti matumizi ya bidhaa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kwa kuwa uzalishaji wa tumbaku nchini unazidi kuongezeka wakati takwimu za Kimataifa zinaonyesha kuwa nchi wazalishaji wakubwa wa Tumbaku kama Marekani, Afrika Kusini, Ulaya Magharibi, unapungua sana, ni vema Serikali iache kufanya kampeni za kuhamasisha wananchi kuongeza kilimo cha Tumbaku, pia Serikali izuie wawekezaji wa nje kupanua kilimo cha Tumbaku ili nchi yetu iache kuwa chanzo cha uharibifu wa afya za binadamu duniani sambamba na uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii waliochambua Azimio hili la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani Kuhusu Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku, naomba nianze na Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Omar Kwaangw', ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, ambaye ni Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Hasnain Dewji na Mheshimiwa Meryce Emmanuel.

Wengine ni Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Sameer Lotto, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Usi Ame Pandu, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim na mimi Mheshimiwa Janet Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru hasa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, ambaye ni Naibu Waziri na pia naomba kumshukuru sana Katibu Mkuu Bi. Hilda Gondwe na watalaam wengine wote ambao wamefanyakazi kubwa kuhusu azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruksa yako naomba sasa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa hivi leo nikiwa nimo katika hali ya uzima. Baada ya haya, niungane na wenzangu wote kwa kutoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, pamoja na wengine waliofariki kufuatia ajali ya ndege. Nawaombea wafiwa wote wawe na moyo wa subira katika wakati huu mgumu.

Aidha, napenda nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Vilevile pongezi zangu nazitoa kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri katika nafasi mpya walizoteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5) (c) na 70(2) Toleo la mwaka 2004, napenda kutoa mtazamo wa Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani kuhusu kudhibiti bidhaa za Tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sote tunaelewa madhara makubwa yaletwayo na matumizi ya tumbaku kwenye moyo na mapafu. Tumbaku pia husababisha uwezekano wa kuongezeka kwa saratani, kuziba mishipa ya damu, kupata kiharusi, kuzeeka kwa ngozi, kupungua kwa nguvu za kiume, kuharibu mimba, kujifungua watoto njiti, kuleta matatizo makubwa ya kazi ya misuli, mifupa, viungo, uti wa mgongo na mengi mengine. Hivyo, tunalazimika, kwa nguvu zote kudhibiti matumizi ya tumbaku nchini na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2003, Bunge letu Tukufu lilipitisha Sheria ya Kudhibiti Tumbaku *(Tobacco Products Regulation Act 2003)*. Bahati mbaya ingawa sheria hii imebaki kwenye vitabu na hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kuifanya itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka uliofuatia, Shirika la Afya Duniani *(WHO)* liliidhinisha mkataba wenye lengo hilo hilo la udhibiti wa bidhaa za tumbaku duniani *(WHO Framework Convention on Tobacco Control 2004)*. Mkataba huu ulitiwa saini na nchi 169, Tanzania ikiwa ni ya 88 kuweka saini. Mpaka hivi sasa, nchi 142 zimesharidhia mkataba huu. Kwa kweli, Tanzania tumechelewa kuuridhia mkataba huu. Hivyo kuna kila haja ya kufanya hivyo sasa, ili nasi tujiunge katika safu za Mataifa yenye kudhibiti uovu huu wa kijamii *(social evil)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo muhimu yanayopendekezwa na mkataba huu ni haya:-

(i) Kuweka ushuru na bei na kuacha kuondoa misamaha ya kodi katika bidhaa za tumbaku ambazo zitafanikisha malengo ya kiafya katika kupunguza matumizi ya bidhaa hizi.

(ii) Kupitisha sheria ya kukataza uvutaji katika maeneo ya kazi, kwenye usafiri, kwenye maeneo ya wazi yanayotumiwa na jamii ili kujikinga na moshi wa sigara.

(iii) Kuhakikisha ya kuwa paketi za sigara hazitoi ujumbe usio sahihi na kupotosha kuhusiana na madhara ya afya kama vile kuziita sigara baridi.

(iv) Kuhakikisha ya kuwa kwenye pande zote za paketi ya sigara kuna onyo linaloelezea madhara ya kiafya kwa matumizi ya tumbaku.

(v) Onyo hili lionekane na kusomeka vyema na maandishi yatumie 50% ya paketi na kwa hali yoyote yasiwe chini ya 30% ya paketi.

(vi) Kutahadharisha na kuelimisha jamii juu ya madhara ya tumbaku na matumizi yake.

(vii) Kuwafundisha na kuwahamasisha wafanyakazi wa sekta ya afya, wafanyakazi wa jamii, wanahabari, walimu na viongozi umuhimu wa udhibiti wa bidhaa za tumbaku.

(viii) Kukataza aina zote za matangazo na udhamini wa bidhaa za tumbaku.

(ix) Kupiga marufuku utengenezaji na usafirishaji wa bidhaa za tumbaku kwa njia za magendo.

(x) Kukataza kuuza na kuwauzia bidhaa za tumbaku vijana wadogo.

(xi) Kuhifadhi afya za watu na mazingira na;

(xii) Kwa kushirikiana na wadau wengine wa mkataba huu, kujaribu kutafuta njia mbadala ya kiuchumi ili kuwasaidia wafanyakazi, wakulima na wauzaji wa tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ubaya wa tumbaku lakini ni muhimu kuelewa kuwa zao la tumbaku miongoni mwa jamii ya Kitanzania ni muhimu sana katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulihakikishia Bunge hili kuwa imeweka mkakati maalum kwa ajili ya kuwasaidia wakulima ambao wanalitegemea zao la Tumbaku katika kuendesha maisha yao ya kila siku kwa kuwapatia zao au shughuli mbadala na zao la Tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kambi ya Upinzani, haina pingamizi na uridhiwaji wa Azimio la Mkataba huu, ila inataka jamii inayotegemea zao hili ipatiwe zao au shughuli mbadala na tumbaku. Hii inatokana na hali halisi ya maisha na ukweli kuwa Azimio hili litasababisha wanunuzi wa zao hili kupanga bei ya chini kabisa tofauti na gharama za uzalishaji wa zao lenyewe. Hatima ya uridhiaji wa Azimio hili kwa maisha ya kila siku ya wakulima wa tumbaku ndio jambo ambalo Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iliangalie kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii alikuwa ameomba niwatambulishe viongozi wa Serikali za Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Umma na binafsi, kwa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani ambao wote ni Marais wa vyuo mbalimbali. Mnaweza mkasimama hapo mlipo ili muonekane. Karibuni sana kwenye Bunge lenu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu niliyonayo hapa ya wachangiaji wako kama 15 hivi. Kwa namna yoyote ile hatuwezi kuwafikia wote, kwa hiyo, nitawaomba wachache mtakaopata fursa hiyo basi moja kwa moja muende kwenye Azimio ili ikiwezekana dakika zinazobaki mchangiaji mwingine aweze kupata nafasi ili tupate wengi kadri iwezekanavyo. Atakayetuanzishia mjadala huu ni Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza jioni ya leo kuzungumza kwa sababu sijazungumza tangu Bunge lianze. Naomba niwatakie wote heri ya mwaka mpya na Mungu atujaalie ya kwamba mvua hizi ziende kwa kasi tunayohitaji bila kutuvurugia zaidi miundombinu. Ninaomba pia niwatakie wapiga kura wangu katika visiwa 38 vya Ukerewe heri ya mwaka mpya. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo nitagusia suala hili kwa ufupi tu kwa kuongezea yale ambayo hayajasemwa moja, ni vizuri tunaporidhia mikataba kama hii kupata takwimu za watakaoathirika na uridhiaji wa mkataba huu. Kwa mfano, tungepaswa kujua ni wakulima wangapi wa tumbaku ili tunapozungumza tujue ni watu wangapi wanahitaji kusaidiwa kupata ajira mbadala kwa sababu ni kweli kwamba tusijidanganye baada ya kuridhia mkataba huu na kama Mataifa yote yataridhia mkataba huu itakuwa ni wazi kwamba hata kama sisi tutatendelea kulima tumbaku hatutakuwa na mahali pa kuiuza. Kwa hiyo, ni vema tufahamu mapema na wala tusichukue miaka 30 aliyosema Mheshimiwa Waziri, hiyo tutakuwa tunawadanganya wakulima wetu.

Pili, ni kwamba tujue tumbaku inachangia kiasi gani katika Pato la Taifa na tutazibaje pengo hili wakati tukiendelea katika kupunguza ukulima wa tumbaku.

Tatu, tujue ni viwanda vingapi vitaathirika ili na vyenyewe vianze kubadilisha shughuli ambazo zinafanyika. Hili ombi naliomba makusudi ili tunaporidhia mikataba tuwe tunatoa matokeo yake. Kwa mfano, nchi za Umoja wa Ulaya katika Bunge lake wamepitisha sheria moja na wameandika matokeo yake kwa nchi zinazoendelea. Wamepitisha Muswada ambao utazuia kupokea mazao yoyote yenye kemikali ndani yake. Katika orodha ya nchi zitakazoathirika ni Tanzania kutokana na asimilia 80 ya dhahabu yetu ina kemikali kutokana na jinsi inavyokuwa *processed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya masuala ni vizuri kuyafahamu mapema na kuyafanyia mpango ambao utasaidia kwenda na wakati tusijikute tu wananchi wetu wanahangaika. Lakini mimi napenda niseme niungane kabisa na niunge mkono kwamba suala la tumbaku na mazao yake yana madhara makubwa ambayo mimi nisingependa niendelee kuyasema hapa. Wengi wameyasema na akina baba poleni sana acheni sigara, kwa kweli ni vibaya kabisa kuvuta sigara na tuna vifo vya akinamama na watoto vingi hatuhitaji tena kuongeza vifo vya watoto wetu kutokana na uvutaji wa sigara ambao sio wa lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ulitaka twende haraka niliacha haya mambo mwisho lakini siyo kwamba hayana umuhimu wowote. Ningependa niseme kwamba kifo cha Mheshimiwa Juma Akukweti kilitupa masikitiko makubwa na kwamba kwa sisi ambao ni wana CCM ni pengo kubwa alivyokuwa akifanya kazi yake vizuri ya kudhibiti Bunge na kuliongoza Bunge akimsaidia Waziri Mkuu. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Wale Mawaziri na Manaibu Waziri wapya, nimekutana na Mheshimiwa Bernard Membe kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiiano wa Kimataifa pale Addis Ababa anafanya kazi yake vizuri tumwombe aende na uzi ule ule. Ni mtu ambaye anaweza kweli kuchanganyika na kujenga hadhi ya Tanzania katika Mawaziri wenzake wa nchi zingine za Afrika. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Dr. Batlida Burian, nakutakia kila la heri ndugu yangu, hiyo kazi nilishaifanya wakati wa Waziri Mkuu, Marehemu Edward Sokoine ni kazi ambayo wewe ndiye utakayekuwa mhimili mkuu kwa Waziri Mkuu akiwa na kazi nyingi umsaidie kusimamia nchi hii na usaidie katika kila jambo ili aweze kufanyakazi yake vizuri. *(Makofi)*

Ningependa pia nimpongeze Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kuingia kwenye Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji nikiwa na matumaini ya kwamba ataongeza nguvu katika eneo hilo ambalo Tanzania tunalihitaji zaidi, mipango yetu inahitaji kuwa makini zaidi ili tuweze kuwa pamoja na wenzetu wanaosonga mbele katika ulimwengu wa sasa. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa William Ngeleja, ningependa nikupongeze sana mkwe wangu kwa utulivu ulionao na umakini ulionao, nina uhakika na uwezo wako wa kujifunza kwa waliokutangulia natumaini ya kwamba utajifunza mengi kutoka kwa viongozi wako wa Serikali Waziri Mkuu, pamoja na Rais ili uweze kusonga mbele kama kijana shupavu. Vijana siku hizi wanajiita *digital, analogue* ndiyo akinamama Mongella. Sasa hawa vijana wenyewe ni *digital*. Kwa hiyo, natumaini hawa vijana wapya ambao wameingia *with a digital system* watakuwa pamoja kwa sababu mimi bado natumia *analogue* na bado nawasiliana kwa hiyo, bado tutakuwa pamoja, tutawasaidia tu kuwapa uzoefu tulionao. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya ningependa tu niseme kwa kweli Azimio hili limepitwa na wakati, tumechelewa kuridhia na wala hakuna sababu ya sisi kutoridhia. Lakini nisisitize

tu ya kwamba wale wananchi watakaoathirika kuwe na mpango ambao utafikishwa Bungeni. *(Makofi)*

Mwisho ni kwamba mazungumzo kama haya yanachukua muda mrefu ni vema tunapokuwa tunazungumza Serikali na Wizara mbalimbali katika kuandaa mikataba hii basi wananchi tuwe tunawaeleza hatua kwa hatua ili na wao waendelee, wasistukie tu dakika za mwisho. Kampeni ya kutovuta sigara na tumbaku itahitaji muda mrefu. Kwa hiyo, ni lazima wote tujiandae kuwaelimisha wananchi wetu juu ya matumizi mabaya ya tumbaku. Nadhani hakuna mazuri na mabaya ya tumbaku. Kwa hiyo, naomba niunge hoja mkono nikomboe dakika zangu mbili nimpe mtu mwingine atakayenifuata. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Azimio hili. Awali ya yote naomba nitoe pongezi zangu kwa Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza miaka 30. *(Makofi)*

Lakini pia nitoe rambirambi zangu kwa ndugu na jamii wa Mheshimiwa Juma Akukweti na wale wote ambao alikuwa nao kwenye matatizo hayo na wale wote waliotangulia pamoja naye, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi. *Amin.*

Lakini pia niwapongeze wale wote ambao waliteuliwa kupata nafasi za Uwaziri na Unaibu Waziri. Mimi nakwenda moja kwa moja kuchangia Azimio hili kwa kusema kwamba yale ambayo yote yamechangiwa na walioanza kuchangia ni kweli yako madhara ambayo yako wazi yanajionyesha. Lakini kwa siku ya leo nilitegemea Mheshimiwa Waziri, atatuletea Azimio hili kuliridhia lakini bado atatueleza wananchi wanaolima tumbaku wameshatafutiwa zao mbadala. Lakini leo anatueleza tuweze kuridhia lakini bado utafiti unaendelea, mipango kabambe inaendelea, zao halijajulikana.

Kwa hiyo, mimi napata mashaka sana na wale wakulima wa tumbaku maeneo yote waliopo. Hata wao wanapata mashaka kwa sababu hii mipango kabambe iko mingi na inaendelea kila wakati na utekelezaji wake ni taratibu. Kwa hiyo, nilikuwa nahitaji Mheshimiwa Waziri atakaposimama atueleze hiyo mipango kabambe itakamilika lini. Lakini la pili, Mheshimiwa Waziri katika kueleza utafiti mdogo ambao umefanywa akaeleza kuwa zao la kahawa linaweza likalimwa kule kwa wanaolima tumbaku. Mimi nadhani Mheshimiwa Waziri yeye ni daktari, Naibu Waziri ni Daktari na hawa waliofanya utafiti na wapo madaktari. Nadhani zao la kahawa na lenyewe bado lina matatizo kama anavyoona ya tumbaku. Kama wanywa kahawa wanapokunywa ile kahawa na wanapata matatizo ya ugonjwa wa moyo. Nadhani anapokuwa na matatizo ya ugonjwa wa moyo hata zile nguvu za kiume na zenyewe zinapungua kama za kwenye Tumbaku. Sasa sijui anataka bado yale matatizo ya tumbaku na yale matatizo ya wale ndugu zetu wa kiume yaendelee kuendelea kuwepo kwa kiasi kikubwa tena kwa kasi. Sasa hili nadhni litakuwa ni tatizo kubwa zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini bado wakati wanazungumzia kuhusu matangazo mimi nilikuwa nategemea kilichonishangaza zaidi waliposema hata ku-*support* ile mipira wanapocheza kama *Taifa Star,* Yanga, Simba eti bado wakatazwe, hapo ndiyo nimepata shida kweli kusema hata

michezo yetu tunahitaji izidi kuendelea basi tupate wafadhili na kila wakati tunasikia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais, anasema tunaomba wafadhili mbalimbali waweze kujitokeza, lakini leo kampuni ya *TCC* tunawaambia wale wasiguse pale sehemu ya michezo, hili bado waliangalie vizuri. Kila mmoja anapovuta sigara, anapokunywa kahawa anapokula nyama ya ng'ombe vitu vingi ambavyo vina matatizo vilihitajika viletwe hapa tuweze kuviadhimia. Lakini kubwa walililoliona wao ni tumbaku tu kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri na udaktari wako utuletee na yale ambayo unaona yana matatizo tuje kuyaadhimia hapa. *(Makofi/Kicheko)*

La pili, kuhusu suala la mbolea nimeona humu kwenye Azimio amezungumzia kuhusu suala la mbolea inavyoathiri udongo, inavyoathiri wakulima, Mheshimiwa Said Nkumba, ni mkulima hasa wa Tumbaku, lakini bado yuko imara hajaathirika sehemu yoyote tena yuko imara zaidi. Mheshimiwa Vita Kawawa, ndiyo haisemeki. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nashangaa hapa kuambiwa wale wakulima wa tumbaku lakini bado hii hii mbolea tuangalie kwenye mazao mengine ambayo yanalimwa. Mazao asilimia karibu 80 au 90 yote yanatumia mbolea. Kwa hiyo, kama tunaona hii mbolea inaathiri udongo wetu na inaathiri wakulima ambao wanaishika basi tupige marufuku kabisa kuingiza katika nchi yetu. Kama tutapiga marufuku kwa hiyo, hasa kilimo cha mahindi na bidhaa nyingine ambazo tunalima hatutaweza kutumia mbolea sijui huu uchumi na nchi yetu tutaifikisha katika hali gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiangalie upande wa tumbaku, tuangalie sasa madhara ya hii mbolea wanayoisemea kuwa inaathiri udongo. Unapolima mahindi bado utaweka mbolea. Kwa hiyo, sehemu nyingi wananchi waelewe au waelezwe, wasikubali kutumia mbolea. Wanapotumia mbolea itaathiri ule udongo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali naomba Mheshimiwa Waziri akisimama watueleze watumie mbolea au wasitumie mbolea na kama kigezo kilikuwa ni mbolea basi wale hawana tatizo na sehemu wanayopanda tumbaku, labda Mheshimiwa Waziri nimfahamishe, sehemu wanayopanda tumbaku, wakishavuna tumbaku, wakija kuweka mahindi wala hawahitaji kuweka mbolea tena, ile mbolea inajitosheleza na mahindi yanastawi vizuri zaidi. Kwa sababu tumeona na ushahidi tunao. Ni kweli ina madhara, sikatai kuwa tumbaku haina madhara kwa watu, nasema kuwa tumbaku ina madhara na viko vitu vingi ambavyo bado vina madhara. Lakini pale pale nataka nieleze tumbaku katika nchi hii ni zao la pili, la kwanza ni kahawa lakini la pili ni tumbaku. Linaingiza shilingi bilioni 40 mpaka shilingi bilioni 45 katika nchi yetu. Lakini nchi jirani ya Kenya inalima kilimo cha mirungi, hawaambiwi wale mirungi. Lakini ni kilimo ambacho wanalima na wana-*export* nje na kinaongeza pesa katika nchi yao. Sasa sisi tumbaku waambiwe waendelee kulima lakini wakatazwe wasivute bado tuipeleke nje. Mwenye kuhitaji kuvuta anajua anavuta lakini ina matatizo. *(Makofi)*

Lakini sisi nchi yetu bado ni maskini na pale pale kwenye umaskini sasa tunaletewa mikataba na maazimio ya kuambiwa hiki msilime. Leo tutakatazwa tumbaku, tutaridhia mkataba, kesho kahawa, kesho kutwa chai. Kwa sababu chai nayo pia ina

matatizo. Kama tunavyoona kafenia kwenye kahawa bado kuna kafenia kwenye chai. Kwa hiyo, hii mikataba na yenyewe tuwe tunaiangalia zaidi. Leo tunaposema kweli kilimo cha tumbaku baada ya miaka 20 inaweza ikaisha. Lakini miaka 20 tunaona kwa hapa. Miaka 20 iko karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Alli Hassan Mwinyi tu katoka kutawala juzi miaka 10. Lakini hapa katikati ameshapita Mheshimiwa Benjamin Mkapa. Miaka 20 iko kesho kutwa. Tusifikiri miaka 20 bado ni karne. Kwa hiyo, tuelewe kuwa miaka 20 ni midogo. Kwa hiyo, tuangalie utaratibu wa kuweza kuwaandaa wakulima wetu na wale ambao wanaopata ajira. Tusiangalie tu, kuangalia Madaktari wamekaa, wameamua hivi wameamua hivi, je, pato la nchi linakuwaje? Sasa hivi tunahangaika na barabara, tunahangaika na viwanja vya ndege. Shule bado nyingine hazijakamilika huko, tunahangaika nazo. Leo vile vipato ambavyo vinaingizia nchi yetu bado tunavipunguza. Labda kuna njia nyingine ya kuweza kupata hela ya kuweza kutusaidia ambayo Serikali imeweza kuiandaa na kutuletea sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Azimio hili mimi nasema kweli tumbaku ina matatizo, lakini kama Mheshimiwa Waziri akijibu hapa na akasema kwamba bado mpaka miaka 20 ndiyo atakuja kututafutia utaratibu wa kuweza kutuambia kilimo cha tumbaku kitakatazwa lakini bado mtaendelea kulima kahawa kule Tabora na maeneo mengine. Mimi kwa kweli sitakuwa pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bunge Kuridhia kwa Mkataba wa Kimataifa Kudhibiti Matumizi ya Bidhaa za Tumbaku yaani *Framework Convertion on Tobacco Control* ya tarehe 21 Mei, 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze kwa kunukuu Kanuni za Majadiliano, Kanuni ya 49 Kifungu cha 7 kinachosema kwamba Mbunge hatazungumza jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi ya kifedha nalo, isipokuwa baada ya kutaja jinsi anavyohusika na kiwango cha maslahi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina maslahi ya kifedha, ila nina maslahi kama Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wadau wa tumbaku tunatambua umuhimu wa kulinda afya za Watanzania na mazingira yao ni suala la muhimu kabisa katika jamii yetu na kwa sababu hiyo, hatua zozote zinazopelekea kuboresha afya na mazingira ya Watanzania tunaziunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia *on the side of economic point of view* ili wana harakati wanaopiga vita zao letu la tumbaku waje waingize nguvu zao za kutosha katika kuhakikisha kwamba tunapata zao mbadala litakaloleta mapato sawa zaidi

ya tumbaku kwani nchi yetu ni maskini, hivyo tuna wajibu ya kuviangalia vyanzo vyetu vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunaifahamu dawa inayoitwa *asprine*. *Asprine* ni *pain killer* na pia hutumika kwa wale wenye *cadial problems* yaani wenye matatizo ya moyo. Lakini *asprine* vile vile ukinipa mie ninayeumwa vidonda vya tumbo, kesho siwezi kuja Bungeni na ukinilazimisha kunywa nitakufa. Kwa hiyo, sekta ya tumbaku kwa nchi yetu ina umuhimu mkubwa sana. Ina mchango mkubwa na mchango wake hauwezi kupuuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuzalishaji tumbaku inalimwa katika Mikoa kumi ya nchi yetu na Wilaya 22 zinazojishughulisha na wananchi wake hutegemea zao la tumbaku. Kutokana na uwepo wake umuhimu wa zao hili unajidhihirisha kwa kuajiri familia zisizopungua 92,000 katika maeneo hayo. Pia inaajiri watu wasiopungua 8,000, kazi za usimamizi, masoko na viwanda vya kusindika tumbaku. Kwa ajira hizo zote hufanya kutegemewa na wananchi wasiopungua 490,000, sawa na asilimia 1.14 ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunavyozungumzia kudhibiti bidhaa zinazotokana na tumbaku tuzungumzie na kuangalia nini faida Serikali na wananchi wake wanapata na nini tarajio la Serikali kiuchumi. Tarajio la Serikali kiuchumi ni kuinua kipato cha mwananchi wake na vile vile kipato cha Serikali ambacho kinakuza hali ya uchumi wa nchi yetu. Tumbaku ni zao linalochangia sana Pato la Taifa. *(Makofi )*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano halisi michache. Moja, kwa kipindi cha miaka mitatu, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 27,701 mwaka 2003 hadi kufikia tani 56,463 mwaka wa fedha 2005/2006. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 wakulima waliingiza bilioni 54.121. Halmashauri katika mapato yake *District Council Phase* ya 5% ziliingiza wastani wa shilingi bilioni 2.7. Serikali Kuu iliingiza shilingi bilioni 65 na mapato ya mauzo ya fedha za kigeni tuliingiza dola milioni 80.8. Kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu *quarter* inayoishia 2005 inasema hivi na naomba kunukuu: "Mazao makuu ya biashara yaani *traditional crops*. Zao la kwanza lilikuwa ni pamba, mwaka 2005/2006 liliingiza dola milioni 111.5. Zao la pili, lilikuwa ni tumbaku, limeingiza dola milioni 80.8 na kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2003/2004 na 2005. Mwaka 2003 sekta ya tumbaku iliingiza dola milioni 40.8. 2004 dola milioni 57.6. Mwaka 2005/2006 dola milioni 80.8. Hii ukijumlisha kuna mazao mengine ambalo zao la tatu lilikuwa ni kahawa, liingiza dola 74.3, korosho dola 46,000.6. Chai dola 25.6 na la mwisho lilikuwa katani dola milioni 7.3. Jumla yake yote ilikuwa ni dola milioni 346.1, sawa na zaidi ya asilimia 25 ya mapato ya mauzo yote ya nje kwa nchi yetu, ambayo yalikuwa ni dola bilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo ambalo linaonyesha dira tosha kwamba pato la tumbaku katika Serikali limekuwa likiongezeka na kusaidia mambo muhimu ya uchumi wa Taifa letu na kwa kuliona hilo Serikali kupitia Waziri Mkuu, tarehe 17 Mei, 2006 alitoa agizo kwa mpango uliopo kuboresha zao ili tuhakikishe

tunazalisha tani 100,000 ifikapo mwaka 2010. Kwa umuhimu wa zao nini maana yake, maana yake ni kwamba Pato la Taifa litaongezeka na hali ya uchumi itaboreka. *(Makofi)*

Hivyo uridhiaji utakaofanywa naomba uoanishwe na utekelezaji wa agizo hili ili wadau wa tumbaku waweze kujipanga ipasavyo. Kwa mfano mdogo tu wa *metaphoric colloration* unaoweza kutafsiriwa kwa kuzingatia bajeti ya ujenzi wa shule tulionao wa shilingi milioni 7 kwa darasa moja. Kwa kodi tuliyokusanya ya bilioni 65 tungeweza kujenga madarasa 9,286. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo pia lazima sisi kama nchi maskini tulitazame kwa kina suala hili. Dhana ya shughuli mbadala litazamwe kwa makini sana. Juhudi za karibuni kupelekea mazao mbadala yalikwama, yalikwama kutokana na kwamba mazao hayo kutokuwa na pato sawa na tumbaku, pili kukosa soko la uhakika ambayo tumbaku yote leo tani 54,000 yote imeshauzwa na haiko mikononi kwa wakulima tofauti na mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili lazima tuliangalie kwa mapana yake. Tulifanye kwa taratibu, tusije tukafanya kwa pupa. Matokeo yake tukaathiri familia nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba niseme kwamba asilimia 90 tunayozalisha tumbaku nchini yote inauzwa nje, ni asilimia 10 tu ambayo inazalishwa katika viwanda vyetu nchini na kufanya kupatikana kwa sigara. Lakini sigara hizo hizo pia zote hatuzitumii hapa nchini, zinakuwa *exported.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie pia Japan sasa hivi jamani wanalima tumbaku. Kwa hiyo, sisi tukiacha tu ghafla, ile *share* ya soko letu kule watalichukua. Naomba nimalizie kwa kusema nakushukuru sana Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mimi nawapa pole sana waliopatwa na msiba na kuwaombea huko mioyo inakokwenda iangaliwe angaliwe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawaombea wale ambao wamepata mafanikio ya hapa na pale, waendelee na juhudi iliyowafanya waonekane. *(Kicheko)*

Naomba nichangie habari ya tumbaku. Mimi umri wangu huu nimeanza kuona tumbaku kwetu nikiwa mtoto, ikiuzwa senti sita na hilo ndilo zao lililonisomesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule tumbaku Makao Makuu ya Ngara, Kibondo na Biharamlo yalikuwa Biharamulo. Lakini nikisoma historia ya tumbaku kule ilikotoka ni muda mrefu. Hivi ninyi wana sayansi mlikuwa hamjagundua kwamba ina matatizo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka mingapi Amerika wamegundua tumbaku, leo hii ndipo mmekaa, mmegundua kwamba tumbaku imeua. Nadhani kama tumbaku inaua, tumeshazika watu wengi, poleni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wanaoshikilia Serikali, kwanza kabisa maslahi ya wananchi. Muwe tayari kudharauliwa, msiuze sifa kwamba nchi yetu isifiwe kwa damu ya Watanzania. Nakumbuka kuna Rais aling'ang'ania zao baya linalosaidia wananchi mpaka akakamatwa. Nadhani mpaka leo hajatoka jela. Mbona ninyi mnaingia mambo kichwa kichwa tu hivi hivi? *(Kicheko/Makofi)*

Naomba niseme, kama tumbaku imeua kwa ajili ya kuvutwa, nadhani katika kipindi ambacho tumbaku itakuwa imekatazwa Watanzania watakaokufa wanazidi wale ambao wameshakufa kwa ajili ya tumbaku. Kwa sababu watoto wao hawatatibiwa, watoto wao hawatasoma, hawatajenga nyumba na mambo mengi yanayotarajiwa hayatafanyika na hicho ni kifo. Nilipokuwa nafikiria Muswada huu niliona kwamba inaweza ikafanana kabisa na mauaji ya halaiki angalieni sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu hawa wanaotuambia tumbaku inaua turidhie kuikataa. Hivi vinavyoua katika dunia ni tumbaku tu? Mbona mabomu yanatengenezwa yanamaliza watu? Hebu waambieni Waamerika waridhie kutengeneza mabomu kama watakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, silaha mbaya zinatengenezwa kila kukicha mbona hawajaridhia hizi. Lakini kibaya ni tumbaku tu kwa sababu inalimwa na maskini na nchi changa au nchi zinazoendelea. Hawataki tuwafikie. Kwa hiyo, mimi nafikiri mambo mengine tuwe tunayaangalia kwa makini lakini tukitanguliza maslahi ya watu wetu. Ni kweli, mimi nilitaka nione jumla ya Watanzania wanaokufa kwa tumbaku kila mwaka ni wangapi? Siyo tu unakuja sijui kuna kidonda huku laaa!! Tuambieni takwimu ya tumbaku inaua Watanzania wangapi kila mwaka. Lakini mbona takwimu za malaria

zipo. Nadhani malaria inaongoza. Mbona hatujaletewa mkataba wa kuipiga vita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaletewa mkataba wa kupiga vita malaria inayoua Watanzania, tunaletewa tu kwa sababu watu wameshafanya. Inayoua Watanzania, tunaletewa tu kwa sababu watu wameshafanya, *physibility study* kwa tumbaku kutuuza wajipatie mapesa ya dunia. Lakini UKIMWI mbona hatujafanya mkataba wa kuuondoa. Kifua kikuu mbona inamaliza watu? Hata safura kwa nchi changa mbona hatujafanya mikataba? Ubaya imekuwa tumbaku. *(Makofi/Kicheko)*

Nilikuwa naomba sana tuangalie, kabla kwa kweli mimi sina uwezo lakini ningekuwa na uwezo ningewaambia watu wa Biharamulo waendelee kulima tumbaku mpaka hilo zao mbadala lije na listawi tulinganishe ni kipi kinacholipa, ni tumbaku au ni hili zao mbadala. Msitufanyie usanii ndugu zangu kwa maisha ya watu. Msifanye usanii kwa maisha ya watu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima watu, kwa sababu mazao mengine kama yalivyo *tradition* ni tabia kwani Usukumani hakuwezi kustawi kahawa? Au Kagera hakuwezi kustawi pamba? Hapana! Ni tabia ya watu, ni utamaduni wa watu. Kwa hiyo, ukisema sijui unaleta *vanila* badala ya tumbaku, yule Mnyamwezi hana utamaduni wa *vanila* hawezi kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mkadirie madhara yatakayotokana, tukisharidhia hili hakuna atakayepambana na Serikali. Bunge Tukufu walilolichagua limekataa ni nani atakayelima zao hilo? Halafu watanyanyaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matembe ambayo tumeyatengeneza miaka nenda rudi. Je, hayo mtayanunua? Hayo matembe mabanio mtayalipa? Mashamba yamefyekwa muda mrefu sana, fidia itatoka? Mimi nadhani kama wenzangu walivyosema Serikali yetu Tukufu ikadirie kabisa kipato kinachopatikana basi kama kitafidiwa tuondokane na tumbaku hakuna kusema tutalima, tutalima, unalima kitu ambacho kimeshaalaaniwa? Kimelaaniwa na Bunge sasa tunataka kulaani tumbaku na ndiyo kuchimba kaburi na kulizika sasa nani ataendelea hayo na ni nani atanunua? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa kweli twende mbali, lakini pia unakimbilia tu, sijui kwa nini tumbaku. Hivi pombe haiui? Labda pombe haiui? Watu wengi wamekufa kwa pombe na yenyewe pengine kesho mtaleta turidhie. Lakini nadhani kwa kuwa na wakubwa wanagusagusa pale, itakuwa kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi sikutaka kusema mengi lakini naomba sana sana wote waliopewa dhamana ya kuongoza watu, maslahi ya wananchi yawekwe mbele. Mpaka leo kuna nchi nyingine hazitaki kuridhia hizi nchi 17 zimeshapigwa kiboko? Tangu tusaini imepita miaka kadhaa, tumeshapigwa? Kinachotukimbiza kimbiza ni nini? Watu wetu wana matatizo, hatujui ajira zilizoahidiwa zitatoka wapi? Hatujui maisha bora yaliyoahidiwa yatatoka wapi. Sasa na kale ambako kangeongezwa kidogo, basi nako tunafuta bila kuandalia watakuwa wapi. Nawaombeni sana, mnasema

mbolea inaua ardhi, wakati Waziri Mkuu karibu awamalize Wakuu wa Mikoa kwamba walete mbolea kijijini. Sasa wanaleta balaa kijijini kweli? Hii mbolea inayoua ardhi.

Mheshimiwa Rais wetu na Waziri Mkuu nadhani mnawaweka pabaya. Hakuna zao linaloweza likastawi bila mbolea. Kama ni kuharibu ardhi Wazungu wangekuwa wameshahama. Maana yake Wazuri hawalimi bila mbolea na zile *big four* zingekuwa zimeshakufa, lakini hakuna zao lisilohitaji mbolea.

Kwa hiyo, ndugu zangu yote haya ni kujaribu kuhalalisha kuonyesha ubaya wa tumbaku. Lakini mimi nilikuwa naomba kabisa hawa watu wetu mimi Bunge la mwezi wa nne nikijaliwa kuja nitakuja na orodha ya wakulima wa tumbaku na mali zao zote walizokwisha ku-*invest* hizo basi mkadirie kama mtanipa pesa niwapelekee nawaambia leo hii acha tumbaku. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kama walivyotangulia wenzangu napenda nitoe pole kwa niaba ya wananchi wa Sikonge kwa kifo cha Mheshimiwa Marehemu Juma Akukweti na wenzake waliopata ajali ya ndege kule Mbeya na nimwombe Mwenyezi Mungu wale ambao walinusurika kwenye ile ajali bado wanaendelea kupata matibabu, basi Mwenyezi Mungu awape nafuu ya haraka wapone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisoma Azimio hili vizuri na kama alivyosema Waziri, Azimio hili malengo yake siyo kusitisha kilimo cha tumbaku. Kwa maelezo hayo tu, mimi nashawishika kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Natambua umuhimu wa afya ya Watanzania na uhifadhi wa mazingira, kwa hiyo, naomba nichangie yafuatayo, kwanza, na mimi hapa niungane na Mheshimiwa Vita Kawawa. Yeye ni Mwenyekiti wa Bodi na mimi ni Mkurugenzi kwenye hiyo Bodi ya Tumbaku, siyo Mjumbe, tuna mabadiliko siku hizi. Mimi naitwa Mkurugenzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana vita dhidi ya kilimo cha tumbaku iendeshwe kwa tahadhari kubwa kwa sababu ni sekta inayotegemewa na Watanzania wengi. Suala hili lisiwe la watu wachache wa afya tu au vi-*NGOs* vinakutana kutana huko. Suala hili ni la wadau. Wadau wa kwanza wakubwa sana ni wakulima. Hawa ambao wamehangaika kwa miaka mingi sana na zao hili, wako wanunuzi wa tumbaku, viko viwanda vya kukaushia tumbaku, viwanda vya sigara, Bodi yenyewe ya Tumbaku na Halmashauri za Wilaya. Hawa wote ni wadau, lazima washirikishwe katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza lakini mimi bado yako mambo mengine yananichanganya maana unapokuwa na maelezo ya jambo ukawa na upande mmoja tu wa ubaya, huna faida unatiliwa mashaka. Sasa yako mambo mengi mimi yananichanganya na inawezekana na wananchi wangu yakawa yanawachanganya. Kwa mfano, tulikuwa na semina hapa imeitishwa na watu wakereketwa wanaojitahidi

kuelezea mabaya ya tumbaku. Baadhi ya mambo mimi yananichanganya. Sasa ni vizuri naomba katika hizo kampeni basi tuyaangalie. *(Makofi)*

Kwa mfano, unapozungumza kwamba 75% ya wakulima wa tumbaku nchini wanavuta tumbaku, si kweli. Mimi ni mkulima, sivuti tumbaku. Wako watu wengi tu lakini hawavuti, Dar es Salaam wako pale watu wengi tu wanavuta tumbaku siyo wakulima. Kwa hiyo, mambo haya yafanywe kwa utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, halafu tumbaku inaleta jangwa, si kweli. Mikoa ya Shinyanga na Mwanza siyo wakulima wa tumbaku, lakini kuna jangwa kule. Mahali inapolimwa tumbaku udongo haufai tena. Amesema Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally hapa, lakini nataka kuuliza waliofanya utafiti hapa ni wataalam wa afya au wa kilimo? Kama ni wa afya sawasawa. Lakini wataalam wa kilimo tunapotumia mbolea ya tumbaku mwaka unaofuata tunaendelea kutumia mbolea hiyo hiyo ambayo tuliitumia mwaka jana. Kwa hiyo, naomba sana utafiti unapofanyika watu wa afya na kilimo katika masuala ya kilimo muende pamoja mnapotupa maelezo sisi wakulima tujue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja zingine kwamba wakulima wa tumbaku ni maskini wa kipato na hawana chakula. Hizi hoja sijui wamezipata wapi? Sisi kwetu wakulima wa tumbaku ndiyo hasa wanaosomesha watoto kwenda shule za sekondari, wakulima wa tumbaku ndiyo wanaochangia miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye vijiji, wakulima wa tumbaku ndiyo wenye uwezo hata wa kujenga nyumba za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho ni hilo la tumbaku na madhara. Mheshimiwa Phares Kabuye amesema hapa na mimi nataka niwaulize ndugu zangu, hivi tumbaku wataalam juzi hapa wametuambia mtaalam mmoja wa afya ya jamii amesema tumbaku ina magonjwa 40, akasema pombe ina magonjwa 60. Sasa hata kwa hesabu ya chekechea hivi 60 na 40 ipi kubwa?

**WABUNGE FULANI:** Sitini.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tungetegemea tupate hapa maelezo ya mwanzo ya kupinga utengenezaji wa pombe lakini tunapewa maelezo tu dhidi ya tumbaku tu. Hapa kuna viwanda chungu mzima vya pombe mpaka Konyagi. Lakini mpaka pombe nyingine ukimwaga pale ukiwasha kibereti inawaka moto, lakini hakuna hoja hapa ya pombe ila tumbaku tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku na mazingira, na hili ndilo nataka nijikite kidogo nisema hapa. Zao hili lina uhusiano wa karibu sana na mazingira. Sisi tunakata miti lakini tunajitahidi sana kupanda miti. Mwaka 2003/2004 hekta 9,700 sawa na miti 32,000,000 zilikuwa zimepandwa kwa ajili ya wakulima wa tumbaku kutumia wakati wa ukaushaji wa tumbaku. Lakini kuanzia mwaka 2004/2005 hadi 2006/2007 upandaji upo kama ifuatavyo:-

Mwaka 2004/2005, tulipanda miti 2,200,000, mwaka 2005/2006 miti 2,500,000 ilipandwa. Lakini pamoja na huu upandaji wa miti teknolojia ya majiko ya kisasa na

mabani bora  yenye uwezo wa kupunguza kiasi cha mahitaji ya kuni kwa asilimia 40 imeanza kutumika. Hatufyeki miti yote sasa hivi tuna utalaam mzuri sana wa kutumia majiko ya kisasa katika kukausha tumbaku. Tunakata matawi na mti unaendelea kukua kama ilivyo kawaida. Sasa kama wengine bado mna mawazo ya teknolojia ya zamani sisi tumeshahama huko. Mpaka sasa tumeshajenga majiko 1,038 kwa ajili ya kukaushia tumbaku. Sasa suala la matumizi ya kuni limekuwa linapotoshwa kwamba tumbaku inamaliza kuni. Si kweli. Asilimia 95 ya matumizi ya kuni ni kuni zinazotumika majumbani ndizo ambazo zinatumika kwa kiasi kikubwa. Nataka niwape takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuni za kupikia vijijini hizi ziko kwa *metre cubic* kwa mwaka zinatumika *metre cubic 32,100,000* kwa matumizi ya kupikia vijijini. Matumizi ya kutumia miti mijini tunatumia 5,400,000, ukaushaji wa tumbaku unatumia 459,500, uchomaji wa matofali na chokaa 450,000, ukaushaji chumvi 350,000, ukaushaji samaki 28,000, pombe za kienyeji 210,000, uokaji mikate 150,000, mamalishe 108,000, ukaushaji chai 20,000 na ufinyangaji 840,000. Jumla kwa mwaka ni *metre cubic* 39,276,340 za kuni zinatumika.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya mahesabu hapo unapata mahitaji ya tumbaku yanaonyesha kwamba tumbaku inahitaji asilimia 1.1 ya mahitaji yote ya kuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya utafiti maana hatuendi tu hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao mbadala na hapa naomba nimalizie hapo. Mimi sitakubali wananchi wangu waache tumbaku sasa hivi waingie tu kwenye mazao ambayo hayana masoko, sijui tulime pilipili hoho, hapana. Sasa hivi wastani wa bei ya tumbaku wastani ni shilingi1,000. Ukiniletea zao hapa la shilingi 200, mimi siwezi kuwaambia wananchi wangu walime shilingi 200 kwa kilo moja. Tunataka zao mtakalolileta kwa wakulima lilingane na shilingi 1000 au lizidi hapo ndiyo wananchi wetu watalima.

Halafu mazao haya, kila zao ndugu zangu linamatatizo. Ukienda kwenye pamba kuna matatizo, korosho ndiyo hivyo mara wanunuzi waache, zao gani ambalo ni zao ambalo limekaa hapo liko kama mazingira ya peponi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa ndugu zangu nataka niseme wazi hapa. Lengo la Serikali itakapofika mwaka 2010 tani 100,000 ndiyo kazi ambayo ninaifanya sasa hivi nawahamasisha kweli kweli wananchi wangu, tufikie huko kwenye hizo tani laki moja mpaka pale nitakapopata zao mbadala, bila ya zao mbadala hatuelewani. *( Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Jimboni kwangu uje imara kweli kweli na nawaambia hawa watu wa *NGO's* mnapokuja kwangu mje imara mtanikuta nipo, nitawauliza, mnawaambia watu waache kulima tumbaku walime nini sasa hivi? Kama hakuna zao mbadala basi tutakutana kwenye majukwaa, lakini mimi naendelea kuwahamasisha wananchi wangu waendelee kulima tumbaku kama zao la biashara. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo naomba nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Said Nkumba na tunaipongeza Serikali kwa kuteua Wajumbe mahiri kiasi hiki. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Stella Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Manju Msambya, ambaye ameniambia atazungumzia habari ya zao mbadala baada ya hapo tutamsikia sasa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kabla ya kuendelea. Mheshimiwa Stella Manyanya, karibu.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mada hii ambayo ni *sensitive* sana hasa kwa wakulima wa Mkoa wa Ruvuma ambako mimi ndio natoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishiwa nguvu kwa kweli si kwa sababu nimevuta tumbaku, maana yake wamesema tunaathirika wanawake na wanaume. Lakini pia nawaasa ndugu zangu hasa wale ambao wanahitaji kuwa na uzazi wa mpango sasa hivi, tusije tukawapa sasa tumbaku nyingi wanaume zetu ili tusizae watoto wengi. Kimsingi naunga mkono suala la afya kuwa ni suala ambalo lazima litiliwe mkazo na tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Itifaki hii, ili kuwapa mwanga wananchi wetu, wale ambao wanahusika na zao hili, waweze kujua wanashughulikia zao la aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni ukweli usiopingika kama ambavyo wenzangu wameeleza zao hili tumelifahamu toka tunazaliwa na ndilo linalotusaidia, sasa hivi kuna kampeni za kujenga shule, kuna kampeni za kuhakikisha watoto wote waweze kupata elimu kwa kupitia nguvu za wananchi na kwa upande wa Namtumbo ambao ni wakulima wakuu wa zao hili la tumbaku, ndio zao pekee wanalolitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakuwa na wasiwasi na hao wenzetu wanaotuletea hizi Itifaki kila wakati kwa sababu sisi tumekuwa tukiridhia wakati wao wanakuwa labda wameshaifahamu siku nyingi wamekaa nayo huko, wanaanza ku-*phase out* taratibu taratibu halafu mwishoni tunaletewa sisi ili tusitishe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hazuii wakulima kulima tumbaku kwa sasa hivi, lakini ukweli ni kwamba kumharibia mtu soko sio lazima umwambie usilime, hata ukishazuia kwamba zao hili halihitajiki, punguzeni kuvuta, ridhieni mkataba moja kwa moja nikumkatisha tamaa na kumpunguzia nguvu huyu mkulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huzuni yangu kubwa zaidi ni kwamba aidha, kwa makusudi au kwa bahati mbaya au kwa upungufu wa uwezo wetu, wanasayansi wetu

wamekuwa kila wakati wanatuletea hizi mada zikiwa zimepitwa na wakati, wakati wananchi wameshamaliza nguvu zao nyingi, sasa mimi mtazamo wangu ni kwamba tuongeze bajeti ya wanasayansi wetu kufanya tafiti mbalimbali kwa sababu hata sasa hivi kuna zao linakuja kwa kasi sana, zao la Jetrofa, hatujaweza kulifahamu kwa kiasi kikubwa lina madhara gani mbele yake. Tutawahamasisha watu acheni sasa kulima tumbaku limeni Jetrofa, baada ya miaka ishirini tutaambiwa tena Jetrofa ina sumu, Jetrofa inaharibu ardhi, matokeo yake tutarudi tena kule kule tunakotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba hao wenzetu wanaokuja na viini macho kila wakati watufikirie na sisi wenzao, sasa hivi kwa mfano kwenye zao la kahawa kuna fomu zimeshaanza kutolewa huko kwamba kila mkulima lazima sasa ajaze aonyesha *inputs* zake ni zipi toka siku anaanza kulima mpaka anavuma. Kwa sababu wenzetu wakubwa hawataki vyakula ambavyo vina mbolea, lakini tumekuwa tukila kila siku na hata uvumbuzi wa hizo mbolea haukuanzia Tanzania, kulikuwa na mgunduzi ambaye alifanya hivyo, sasa tunasema hivi na yule aliyekuwa amegundua mwanzo basi labda hakufanya utafiti wake mpaka mwisho, inabidi kampuni kama hizo labda zifuatilie tena ili ziwe zinafanya *research* zinazofika mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu pia nawaasa wananchi wa mkoa wa Ruvuma ukisikia yanazungumzwa ujue yapo, kwa hiyo tusipuuzie, tuangalie uwezakano wa kuona pia hilo zao mbadala ni lipi katika maeneo yetu, ili katika heka tano tunazokuwa nazo au kumi angalau tutenge heka mbili au tatu za ziada kwa ajili ya zao ambalo ni la ziada ili kuanza taratibu wakati tukiwa tunaendelea kulishughulikia hili suala la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wakati wa bajeti yake ya mwaka 2007/2008 tafadhali tunaomba iainishwe wazi ile mikoa ambayo sasa hivi itaathirika na zao hili la tumbaku, kutakuwa na bajeti kiasi gani ya kuisaidia mikoa hiyo. Kwa sababu tatizo hili halina tofauti na tatizo la njaa kwa kuwa linaathiri uchumi wa maeneo hayo, tunaomba tusiletewe bajeti kwamba kuna shilingi milioni 20 zimetengwa ili mradi kiini macho kuonyesha kwamba kunavihela kidogo vimetengwa. Tuwekewe pesa za kutosha ili tuweze kuwahamasisha wananchi hao kuanza kujifunza hilo zao mbadala na hatimaye ili uchumi wa maeneo hayo usiathirike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa orodha yako ni kubwa, kwa heshima na taadhima, napenda kusisitiza kwamba wakulima wa zao la tumbaku kwa hali ya sasa isitukatishe tamaa, tuishi kwa matumaini, zao hili tuendelee kulima mpaka hapo tutakapopata zao mbadala, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya kuridhia mkataba huu, lakini pamoja na kutueleza kwamba tujikite tu moja kwa moja kwenye hoja, mimi nitakuwa sikuwatendea haki wapigakura wangu na vilevile nitakuwa sikuwatendea haki wapigakura wa Tunduru kama sitotoa rambirambi kwa kifo cha mwenzetu, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, mimi nilimfahamu vizuri tumeingia naye pamoja Bungeni mwaka 1990 na kumfahamu kwangu kwa zaidi, mimi na yeye tulipangiwa nyumba moja

ya kulala wageni na ndipo nilipofahamiana naye na tangu siku hiyo amekuwa ni rafiki yangu wa karibu mpaka Mungu amempeleka mbele ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachukua fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Kigoma Kusini kuwapa rambirambi wananchi wa Jimbo la Tunduru na familia ya marehemu na namwomba Mwenyezi Mungu awape Ithibati ya moyo waweze kukabili tatizo lililowakuta. Vilevile nawapa rambirambi wale wote waliokutwa na maafa katika ajali ile, lakini vilevile nimwombee mwenzetu ambaye amebaki hospitali ili aweze kupona haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo niwapongeze wale wote waliopata nyadhifa katika mabadiliko madogo yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika Baraza la Mawaziri, lakini nimpongeze kwa namna ya pekee kabisa na kumtakia kila la heri ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja, kwa nafasi aliyopewa na nadhani atakuwa anafahamu kwa nini nimesema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudie kusema kwamba mimi naunga hoja hii mkono na naridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa takwimu nyingi tu hapa na sina sababu ya kuzipinga takwimu hizo kwa sababu naamini waliotoa takwimu hizo wamefanya kazi. Lakini mimi nilipokuwa chuoni, mwalimu wangu alinifundisha alipokuwa ananifundisha somo la takwimu *(Statistics)* alisema *you can cheat with statistic,* sina sababu ya kuwaita Waheshimiwa Wabunge kwamba ni waongo, lakini tumeelezwa hapa kwamba tumbaku asilimia 90 tunayolima inakwenda nje na vilevile tumeelezwa kwamba wakulima wa tumbaku hawaathiriki na tumbaku ile, lakini uko utafiti wa kisayansi wa hizo *NGO* zinazopondwa ambazo zimefanya kuonyesha kwamba tangu unaposhika mbengu ya tumbaku mpaka unapovuma, wewe vilevile ni mvutaji wa tumbaku ile. *(Makofi)*

Sasa hivi wale waliotoa zile takwimu hili hawakulieleza hapa. Tumeelezwa vilevile takwimu za kwamba tunapanda miti, sasa hivi hatukaushi tumbaku kwa kutumia magogo, tunakata matawi lakini tuelezwe ni miti kiasi gani unachokata ili kukausha tumbaku uliyopanda kwenye ekari moja na msimu unaofuata utakuwa umekata miti kiasi gani na ni miti kiasi gani umepanda mpaka ifike kuota na kuziba pengo la miti uliyokata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka eneo ambalo athari ya kilimo cha tumbaku imejionyesha kuna jangwa na hao wenzetu wote takwimu walizotoa hapa, hawataki kueleza kwa udhati majangwa, ndio maana kila anayechangia anadhana ya mwaka 2010 akilini mwake, hana dhana ya athari hasa inayotokana na zao la tumbaku. Mimi ninafarijika sana pale Mheshimiwa Waziri wa Afya alipokuwa anatoa hoja ya kwamba tuanze kufikiria zao mbadala, mimi tayari nilikwishalifikiria hilo na nilifikiria si kwa nia ya kuondoa zao la tumbaku, binafsi silipendi zao la tumbaku tangu zamani, lakini nililifikiria zao hilo na nikilitamka watu watasema zao hilo lina matatizo hata Mheshimiwa Rais kalizungumzia sana. Ni kweli na baadhi yao waliokuwa wana-*support* tumbaku vile wamesema hakuna zao ambalo halina matatizo. Kwangu mimi nimefikiria zao la korosho, sasa mimi ningetegemea Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yao,

mtu atazame mazingira ya sehemu anayotoka, ni zao gani ikiwa tumbaku itaondolewa litashika nafasi yake.

Mimi nimekwenda hatua moja zaidi na ni kwa gharama zangu binafsi nimewasiliana na watu wa Bodi ya Korosho, nimewasiliana na kituo cha utafiti cha Naliendele na nikamgharamia mtafiti kutoka kule, *Mr. Mbunda* ametoka kule Naliendele amekuja Kigoma na nimekaa naye kwa muda wa wiki mbili kwa gharama zangu amefanya utafiti wa kutosha na akaniachia kazi, kazi ya kupata takwimu hizo ambazo wenzetu kwa upande mwingine wamezitoa, nimeshirikiana na taasisi ya utabiri wa hali ya hewa nawashukuru sana, wamenipa taarifa zote ambazo nilikuwa nahitaji na tayari nakaribia kuzifikisha kwa wahusika. *(Makofi)*

Sasa tunapuzungumzia kuondoa zao la tumbaku ni lazima sisi Wabunge vilevile katika maeneo yetu tuwe tayari kufanya utafiti na kuona ni zao gani litachukua nafasi ya tumbaku hasa baada ya kuelezwa madhara yale ambayo Mheshimiwa Waziri kayaeleza hapa hasa baada ya kuelezwa madhara na hiyo *NGO* inayopondwa ambayo imefanya utafiti, imefanya utafiti mkoa wa Ruvuma, imefanya utafiti mkoa wa Tabora hawakuja tu na takwimu za kuviringa viringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tuelewe kwamba ni jukumu letu vile vile kuja na zao mbadala, tumeelezwa faida kubwa sana inayopatikana kwa kilimo cha tumbaku, lakini wale waliokuwa wanatetea zao hili hawakutuambia mkulima wa tumbaku anapoathirika ni pesa kiasi gani anatumia kwa matibabu. Upo utafiti umefanywa kwa kila shilingi moja mkulima wa tumbaku anayoingiza anatumia shilingi sita kwa matibabu, sasa hili wenzetu wale na zile tumbaku hili nalo wangetueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile mimi nilitarajia yule aliyetueleza kwamba asilimia 90 ya tumbaku inapelekwa nje hakutuambia ikishakwenda kule nje ikiwa *processed* sio hiyo inayokuja kama *Kuber* na *Benson and Hedges* na *Marboro,* inarudi kwa sura nyingine kwa hiyo, vilevile inatumika hapa. Sasa tusifikirie kwamba tuna *export,* lakini ukisha-*export* ni kwa sababu sisi hatuna uwezo mkubwa sana wa kui-*process* hiyo tumbaku, ndio maana tunapeleka kule kama malighafi inakuwa *processed* kule inarudi kama *finished product* sasa hii waliotupa takwimu hapa hawakulieleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi uliyonipa na mimi nilitaka tu nielezee suala la zao mbadala lakini ningekuwa sikueleza vizuri kama nisingetoa na mimi takwimu zangu kama naye mtu mwingine atasema na mimi nimekuja hapa ku-*cheat* na *statistic* itakuwa ni hiyari yake. Lakini mimi naunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nadhani sitatumia zaidi ya dakika kumi itakuwa chini ya hapo. Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida, napenda kutoa salaam za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Juma Akukweti, pamoja na wengine ambao alipata nao ajali. Lakini pia napenda kuwatakia heri ya mwaka mpya Watanzania wote na kuwatakia baraka za Mungu wetu katika mwaka huu wa 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwapongeza Mawaziri wapya walioteuliwa pamoja na Naibu Mawaziri, Mungu awape hekima na nguvu za kuweza kulitumikia Taifa letu. Mimi sitakuwa na mengi sana ya kuzungumza kwa sababu wazungumzaji wameshaongea ambao wanatoka kwenye kanda zile ambazo zinalima zao la tumbaku. Napenda kuipongeza Wizara ya Afya kwa kuleta Azimio hili la kuridhia mkataba huu wa kudhibiti matumizi ya tumbaku, lakini pia nina maoni machache sana. Maoni yangu labda ningependa kuzungumzia suala ambalo limeshasemwa kwamba, je, Wizara imeshafanya utafiti wa kutosha kwa ajili ya viwanda ambavyo vinasindika zao hili la tumbaku kwamba vitaathirika kwa kiasi gani? Na je, itaathiri kiasi gani Pato la Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie suala la matangazo, hilo ndilo lililonifanya niweze kusimama. Katika nchi zilizoendelea ukipita huwezi kukuta tangazo linalovutia uvutaji wa sigara, lakini badala yake utakuta kuna tangazo linalomkatisha tamaa mvutaji pamoja na ambaye havuti. Tangazo lile linakuwa ni asilimia 100, lakini Waziri hapa amesema kwamba Wizara yake itachukua asilimia 50 kwa ajili ya tangazo la kuzuia uvutaji wa sigara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi napenda kuishauri Wizara, ichukue asilimia 100 na badala yake matangazo yanayovutia uvutaji wa sigara yapigwe marufuku iwe ni mabango au kwenye redio kwa sababu matangazo haya si kwamba yanamlenga au kumvutia mtumiaji wa sigara zaidi yanawalenga wale ambao hawatumii tumbaku au kuvuta sigara na zaidi ni watoto wetu ambao wanakua. Wanapoona tangazo lile linavyovutia na kuonyesha kwamba unapovuta sigara, ndio maisha halisi ndio maisha mazuri, ndio maisha matamu, basi vijana hao au watoto hao huvutiwa zaidi na kuanza kujaribu kutumia sigara, ili na wao waweze kuonja yale maisha ambayo wanaonyeshwa katika matangazo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaomba matangazo yanakuvutia sigara, ingekuwa ni vema yapigwe marufuku, anayejijua kwamba anavuta sigara atakwenda dukani atanunua, atavuta, lakini asivutiwe kwa tangazo lile ambalo si kweli kwamba linamlenga yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uhamasishaji wa uvutaji sigara au utumiaji wa tumbaku, nilikuwa naomba elimu iweze kupelekwa kila mahali. Tutumie na asasi zetu za kidini, misahafu, vitabu vitakatifu vinazuia na vinasema kwamba utumiaji wa tumbaku au kuvuta sigara ni dhambi, hivyo ninaomba wananchi wote waelewe kwamba ni dhambi kuvuta sigara au kutumia tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lao Tukufu, sikusudii kutumia dakika nyingi katika jambo hili kwa sababu ningependa kumpa mtoa hoja nafasi aweze kujibu hoja nyingi ambazo

zimeelezwa. Lakini nimekata shauri kutoa mchango kidogo kwa kuvutiwa na mjadala, mjadala umenivutia na kabla sijasema chochote labda niungane na Waheshimiwa Wabunge katika kutoa rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Juma Akukweti, ambaye alitutoka kwa wakati ambao hatukutegemea, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala umegeuka, Waziri wa Afya amesema katika taarifa aliyoitoa hapa Bungeni kwamba hoja anayoileta na Azimio tunalotaka kuridhia, halipigi marufuku kilimo cha tumbaku, alichosema Waziri wa Afya na ambayo dunia nzima inasema ni kwamba mazao ya tumbaku yana madhara kwa afya, sasa mimi sijui ubishi wetu nini hapa. Madhara kwa afya yanayotokana na madhara ya tumbaku ni jambo linalojulikana dunia nzima, lakini upo ubishi dunia nzima juu ya ku-*balance* kati ya uchumi wa tumbaku na afya za watu. Miaka ya 1980 nilikuwa Marekani na ubishi kama ulitokea hapa Bungeni uliwahi kutokea kwa zao hilo hilo la tumbaku na mazao ya tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ile nadhani ndiyo inayolima tumbaku nyingi sana duniani, wale wakulima wa tumbaku wa kule na mjadala ulitokea katika Bunge lao la *Congress* na kilichokuwa kinazungumzwa pale ni kukubaliana waandike maneno gani kwenye *packet* ya Sigara. Wale waliokuwa wanaiungana mkono hiyo hoja walitaka waandike maneno yanayosema *smoking causes cancer* na wale waliokuwa wanapinga wakawa wanasema waandike *smoking may cause cancer,* tofauti zao si kubwa. Wale wanasema madhara yaani uvutaji unaoleta madhara ya kansa na wale waliokuwa wanapinga walikuwa wanasema unaweza kuleta tu lakini siyo lazima. Lakini hawakuwa wanatofautiana sana katika jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukweli unabaki pale pale kwamba duniani hapa watu wengi wanakubaliana ya kwamba mazao ya tumbaku yana madhara kwa afya za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ndicho anachotwambia na dunia ndivyo inavyosema. Lakini mjadala tulioendesha hapa unasema tunapiga marufuku zao la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kama Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika nataka niwaambie, Serikali haijapiga marufuku kilimo cha tumbaku, Serikali inachosema inakubaliana na dunia kupitia *World Health Organization* kwamba mazao ya tumbaku yana madhara kwa afya za binadamu na dunia nzima bado wanalima tumbaku na wanajua hivyo. Lakini kuna hatua nyingi sana zimefanyika ukienda katika nchi zilizoendelea nyingi utakuta hata *Airport* wamesema kabisa mahali pa kuvutia sigara pamewekwa kando kidogo tu. Ndege nyingi siku hizi ukipanda dunia nzima ni *none smoking*. Lakini tumbaku wanaendelea kulima. Lakini na masharti wanayawekwa kwa ajili ya kinga ya afya ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme hayo, niwahakikishie wakulima wa tumbaku wa Mikoa kumi iliyozungumzwa na Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba

Serikali haipigi marufuku kilimo cha tumbaku kuanzia leo, hapana. Tunaendelea na programu ya kuzalisha tani 100,000 na hatujabadili Azimio hilo. Tunachosema mazao ya tumbaku yana madhara kwa afya za binadamu. Kwa hiyo, kwa kweli tunachowambia watu wetu jihadharini msitumie mazao ya tumbaku kwa sababu yana madhara kwa afya za binadamu. Sasa hilo kweli ni la ubishi, hilo halina ubishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkulima anayelima tumbaku siyo lazima awe anavuta kama alivyosema Mheshimiwa Said Juma Nkumba, kwamba yeye analima na ni kweli ni mkulima mzuri sana wa tumbaku na kuvuta havuti. Kwa hiyo, sisi tunamwambia kwamba soko bado lipo. Kwa hiyo, aendelee kulima tena kwa utaalamu kwa sababu hatuwezi kuzalisha tani 160,000 mpaka tutumie utaalam zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ndilo Azimio la Serikali. Narudia hatupiga marukufu ghafla kilimo cha tumbaku. Tutafanya makosa tukifanya hivyo kwa sababu kwa upande mmoja tunatekeleza MKUKUTA wa kuinua kipato cha watu wa nchi hii na watu wa nchi hii ni wakulima wakiwemo wakulima wa tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukisema tumbaku tuiondoe hatuwezi kuiondoa *overnight,* lazima tufanye utafiti wa zao mbadala na utafiti si kitu kinachochukua wiki. Ukianza utafiti leo itakuchukua miaka kadhaa kabla haujapata zao mbadala na ukilipata zao mbadala lazima uende ukalijaribie kwa wakulima wa tumbaku na wanaweza wakaanza kulilima hilo zao mbadala wakililima pamoja na zao la tumbaku. *Economics* zitawezesha kuacha tumbaku wataenda na lingine na mazao ya namna hiyo yapo siyo lazima wakulima wetu wawe watumwa wa tumbaku kwa miaka 50 inayokuja. Kwa mfano, maeneo yanayolima tumbaku kule Tabora yanafaa sana kwa zao linaitwa Jetrofa ambalo linatumika kuleta nishati mbadala na mnajua bei ya nishati ilivyo nzuri duniani. Ukiweza kulima Jetrofa tukipata viwanda na soko la uhakika na ukawa unalima na unauza kwa kiwanda kinachotoa nishati mbadala. Mimi nina hakika bei ya Jetrofa inaweza kuwa nzuri kuliko ya Tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaweza tu kufika hapo baada ya utafiti na baada ya kukubaliana na wakulima wa tumbaku juu ya mazao mbadala. Kwa hiyo, narudia kusema Azimio lililoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii haipigi marufuku kilimo cha tumbaku ghafla. Azimio linasema mazao ya tumbaku yana madhara kwa afya ya binadamu na dunia inakubaliana kwamba lazima tufanye kampeni ya kuokoa maisha ya watu. Sasa hilo mimi siamini kama lina ubishi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukienda tukasema kahawa nayo ina madhara inaweza kuwa ngumu lazima tuseme hili lililoko leo na kama litakuja la kahawa tutazungumza kahawa, lakini leo tunazungumza tumbaku. Inawezekana kahawa ikawa na madhara lakini pengine si makubwa kama yale ya tumbaku inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nilitaka niseme hivyo kwa sababu kama Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika nadhani mjadala huu unaosema sasa wakulima wa tumbaku waende wapi. Mimi nataka niwahakikishie kwamba tunaendelea kulima

tumbaku na kampeni ya kulima tumbaku inaendelea, lakini na kampeni ya kuwaokoa watu wasivute ovyo hizo sigara wakafa inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kutuwekea msimamo huo. Sasa moja kwa moja namwita Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ili aweze kutoa majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, karibu.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi mara nyingine tena kusimama hapa ili kuweza kuhitimisha hoja niliyoileta jioni hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika kuona kwamba hoja hii imewavutia wachangiaji wengi sana. Ningependa niwatambue ninao wachangiaji 11 waliopata nafasi ya kuzungumza humu ndani ya Bunge na wachangiaji 22 ambao wamechangia kwa maandishi. Nawatambua kama ifuatavyo waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni ni Mheshimiwa Janet Bina Kahama, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Felix Kijiko na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoileta hoja hii kwa niaba ya Serikali ni kupata ridhaa ya Bunge, lakini nadhani utawahoji. Lakini nimepata mawazo mengi zaidi na mazuri ambayo kama mtalipitisha Azimio hili yatatusaidia sana katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niwashukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa sababu jambo lililochukua muda mwingi katika majadiliano lilikuwa ni la zao mbadala. Mimi sidhani kama nitakuwa na mengi ya kuongeza kuhusu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyoona ni kwamba waliochangia ni wengi na katika muda niliopewa nitakuwa ninajidanganya kama nitapita kuzungumza kila hoja za kila Mheshimiwa Mbunge alivyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimejaribu kuweka katika makundi jinsi Waheshimiwa Wabunge walivyochangia. Kuna suala la elimu limejitokeza na wengi wamelizungumzia. Wengine wamesema kwamba ingekuwa bora kabla ya kuleta Azimio hili hapa Bungeni tungekuwa tumewaelimisha watu. Nakiri kwamba hiki ni kitu kizuri. Lakini elimu ni kitu ambacho hakina mwisho, tulianza na tutaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wametushauri kwamba hiyo elimu itolewe na wengine wamewataja wanafunzi ni kweli ni walengwa wa matangazo mengi na ni watu ambao wanajaribu vitu. Lakini vilevile tumeshauriwa kwamba twende mpaka vijijini mpaka kwa wakulima na mpaka kwa wananchi. Kwenda vijijini kwa maana ya kuwaambia matatizo ya moshi wa kutumia tumbaku. Lakini vilevile kwa suala la zao mbadala hao wakulima waeleweshwe kwamba hii tumbaku ina madhara na wakisharidhika kama mlivyoridhika hapa ni kwamba inakuwa rahisi kuwaeleza kwamba sasa tujaribu zao mbadala. Hilo tutaendelea kulifanya na niseme tu kwamba suala lililochukua muda mrefu lilikuwa la zao mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbusha kwamba tunazo Sheria zinazohusu Tumbaku hapa nchini. Kuna Sheria moja ya mwaka 2002 inaitwa *The Tobacco Industry Act* na hii inasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Imeunda Bodi ya Tumbaku ambayo kwa sasa Mheshimiwa Vita Kawawa ndiyo Mwenyekiti na inasimamia uendelezaji wa kilimo cha tumbaku na masuala yanayohusiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine iliyopitishwa mwaka 2003 inaitwa: *The Tobacco Products Regulation Act.* Hii inahusu usimamizi wa matumizi ya bidhaa za tumbaku na inasimamiwa na Wizara yangu na hii niliizungumza wakati ninatoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiridhia Azimio hili itabidi tuangalie tena hii Sheria yetu ambayo tuliipitisha mwaka 2003, kuna vipengele ambavyo itabidi vibadilishwe kuendana na jinsi tutavyoridhia Azimio hili kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wamesema kwamba hii sheria ilikuwepo lakini mengi ambayo tumezungumza leo na mengi yaliyoshauriwa ni kwamba yalikuwemo kwenye sheria hii. Nikiri kwamba utekelezaji wake haukuwa mzuri. Matangazo yameendelea ingawa yalizungumzwa katika hiyo sheria na mimi nitamke tu kwamba mkishatupa baraka zenu siku ya leo tutakuwa wakali na mtaona mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la takwimu na kwamba tumezungumza bila takwimu. Lakini tumepata takwimu nyingi hapa siku ya leo. Tafiti zimeanza kufanyika na hasa tumeanza kufanya tafiti kwa watoto wa shule ambao ndiyo walengwa wakubwa na tutaendelea hivyo hivyo na matarajio yetu ni kwamba tutaporidhia Azimio hili kama tulivyosema ni kwamba ukiridhia unakuwa mwanachama

halali na kuweza kuingia katika mikutano inayofanya maamuzi. Tukiwa wajumbe halali tutakuwa sehemu ya maamuzi tofauti na ilivyo sasa ambapo tumepewa *observer status*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa mwanachama wa chama fulani kuna michango na hii *Convention* ina mfuko na kitu kimojawapo ambacho mfuko huo unatumia ni tafiti ikiwa ni pamoja na tafiti za mazao mbadala. Hapa tumezungumza kwamba hata hapa nchini tumeshaanza na masuala ya mazao mbadala.

Nimezungumzia habari za Ludewa, kwa mfano, Ludewa tunajaribu zao la Kahawa, Songea Vijijini wanajaribu zao la mpunga, Mpanda wanajaribu zao la Jetrofa na Kigoma Vijijini korosho. Sasa tuna imani kwamba hapo tutakapokuwa wanachama kamili tukasaidiwa na utaalamu wa wenzetu, tukachukua na uzoefu wa wenzetu, utafutaji wa zao mbadala utakwenda kwa kasi zaidi ambayo najua ni *concern* ya Waheshimiwa Wabunge wengi walivyozungumzia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sina haja ya kuzungumzia zaidi kuhusu zao mbadala au kuhusu ku-*speculate* viwanda vitakwenda wapi. Lakini matarajio ni kwamba watu wakiridhika na kuelewa kwamba matumizi ya tumbaku yana athari kubwa katika afya, uvutaji utapungua. Ina maana basi kwamba zao litakosa soko si kwa siku moja itachukua muda mrefu. Nimetumia *phase in* na *phase out* mara mbili wakati natoa hoja yangu. Nina imani hata viwanda vyenyewe vitatafuta kazi nyingine. Hatuwezi tukaogopa kwamba viwanda vitafungwa huku watu wetu wanateketea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika kwamba hakuna aliyepinga kuhusu madhara ya tumbaku. Nia na madhumuni ya kuleta hoja hii ni kwamba Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba tumbaku ina matatizo na inaleta madhara katika afya za binadamu. Waheshimiwa Wabunge wakiamini na kulielewa hilo itakuwa rahisi hata kwa wananchi wetu kuweza kuelewa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wote nadhani watakuwa waumini wazuri kwa sababu tunajua kwamba zao la tumbaku linatuletea matatizo katika afya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Shirika la Afya Duniani kuhusu Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku liliridhiwa na Bunge)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile katika orodha ya Shughuli za leo, shughuli zote zimekamilika. Basi naomba kuchukua fursa hii kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.17 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 6 Februari, 2007 saa tatu asubuhi)*